

KANISA LA YESU KRISTO LA WATAKATIFU WA SIKU ZA MWISHO • APRILI 2019

# Liahona

**Ujumbe wa Matumaini  
na Ukombozi wa  
Mwokozi ukurasa wa 18**

Unapohisi Kusahaulika,  
Mkumbuke Mjane wa Naini,  
ukurasa wa 12

Muziki wa Pasaka: "Kwenye  
sehemu ya Bustani Takatifu,"  
ukurasa wa 24

Jinsi ya Kutafuta Amani na  
Kuepuka Uwongo,  
ukurasa wa 26



KANISA  
LIKO  
HAPA

# Reykjavík Iceland





Ukiwa na Mlima uliofunikwa na-theluji kati-ka upande wa nyuma, Reykjavík, mji mkuu wa kupendeza wa Iceland, unatoa ukaribisho kwa taifa la kisiwa zaidi ya maili 1,000 (1,609 km) kutoka bara la Ulaya. Awali ukikaliwa na Maharamia wa Scandinavia mnamo 874 BK, Reykjavík ni kitovu cha utamaduni, uchumi, na shughuli za kiserikali za Iceland, vilevile moja ya majiji masafi, ya kijani, na yenye usalama ulimwenguni.

Wakazi wawili wa kwanza wa Iceland walibalizwa huko Denmark mnamo 1851. Baada ya muda mfupi walirudi Iceland, na mnamo 1853 tawi la kwanza lilianzishwa. Leo kuna takribani waumini 300 katika Iceland katika matawi matatu, katika Reykjavik, Akureyri, na Sellfoss. Hekalu la karibu liko London, England, maili 1,177 (1,894 km) kutoka Reykjavík.

Ingawa idadi ya waumini ni ndogo, Kanisa linaendelea kukua. Licha ya changamoto za kutengwa, tafsiri ya nyenzo za Kanisa, hali ya hewa isiyo rafiki, na vikwazo vya kiutamaduni, viongozi wa Kanisa wameahidi kwamba siku moja Iceland itakuwa mfano kwa nchi zingine. Rais Gordon B. Hinckley (1910–2008) alizuru Iceland na kuwakumbusha waumini kwamba wao ni “watu ‘imara na wenye nguvu na uwezo’ wa kufanya mambo makubwa” (“Inapendeza kuwa na Nchi ya kuvutia, nchi Nzuri,” *Habari za Kanisa*, Sept. 21, 2002, 10).

- Misheni ya Iceland ilianzishwa mnamo 1894, lakini ufundishaji wa injili ulisitishwa mnamo 1914. Iceland ikawa sehemu ya misheni ya Denmark Copenhagen mnamo 1975.
- Mnamo 1977, Mzee Joseph B. Wirthlin (1917–2008), wakati huo akiwa mshiriki wa Akidi ya Kwanza ya Sabini, aliiweka wakfu rasmi Iceland kwa ajili ya kuhubiri injili.
- Mnamo 1981 Kitabu cha Mormoni kilichapishwa katika lugha ya Iceland—lugha ambayo haiongelewi kokote ulimwenguni.



Katika nyakati za Kuvunjika Moyo,  
Mkumbuke Mjane wa Naini  
*Keith J. Wilson*

12



Amini katika Ukombozi  
wa Mwokozi  
*Rais Henry B. Eyring*

18



Kufanya  
Kuhudumu  
kuwe kwa  
Shangwe  
8



Masomo matatu  
Kuhusu Upendo,  
Shangwe, na Amani  
*Brian K. Ashton*

26

# Unapokuwa Umevunjika Moyo

**M**aisha yana kupanda na kushuka. Wakati mwingine tunapokuwa chini, tunajiuliza kile Mungu anachofanya—kwa nini Baba mwenye upendo anaruhusu hili litokee? Mashaka haya yanaweza kupanda juu hata sisi kuuliza, “Hivi Mungu anajali kweli kuhusu mimi binafsi?”







Katika hali kama hii, nimepata maandiko haya kuwa yenye msaada:


- **Zaburi 8:4-5:** “Mtu ni kitu gani hata umkumbuke? . . . Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, na umemvika taji ya utukufu na heshima.”
- **Yohana 10:14:** wakati wa maisha Yake hapa juu ya dunia, Yesu alijielezea Yeye kama “mchungaji mwema” na kuongeza, “[Mimi] nawajua kondoo wangu.”
- **Musa 1:39:** huu ni mmojawapo wa mistari ninayoipenda sana, ambapo Bwana anafunua lengo Lake kwa Nabii Joseph Smith: “Kwa maana tazama, hii ndiyo kazi yangu na utukufu—kuleta kutokufa na uzima wa milele wa mwanadamu”—hivyo kusesitiza shauku Yake kwetu kama watu binafsi.
- **Luka 7:11-16:** Siyo tu maelezo haya yanatufundisha juu ya nguvu ya Mwokozi dhidi ya kifo—ukumbusho muafaka kwenye msimu huu wa Pasaka—lakini kwangu yanawakilisha mfano bora wa uelewa wake makini kwa ajili yetu binafsi. Kati ya miujiza yote ya Yesu, michache ni ororo na yenye huruma kama kuhudumu Kwake kwa mjane wa Naini. Ninaposhiriki katika makala yangu (ona ukurasa wa 12), maelezo haya yanaonyesha kwa mfano shauku ya Mwokozi katika na upendo kwa kila mmoja wetu.

Keith Wilson

Profesa mshiriki, Chuo Kikuu cha Brigham Young



- 5 Amefufuka!**   
"Kifo kimeshindwa; mwanadamu yuko huru. Kristo ameleta ushindi!"
- 6 Taswira za Imani:** Bob na Lori Thurston—  
Misheni ya Cambodia Phnom Penh   
Misheni yao haikuwa kile walichotarajia, lakini pia iliwarariki katika njia zisizotarajiwa.
- 8 Kanuni za Kuhudumu:** Kufanya Kuhudumu kuwe kwa Shangwe  
Moja ya vyanzo vikuu vya furaha ya kweli hupatikana katika kuhudumu.
- 12 Katika nyakati za Kuvunjika Moyo, Mkumbuke Mjane wa Naini**  
*Na Keith J. Wilson*  
Kama vile alivyofanya kwa mjane wa Naini, Mwokozi atakuja kwetu katika nyakati zetu za uhitaji mkubwa.
- 18 Amini katika Ukombozi wa Mwokozi**  
*Na Rais Henry B. Eyring*  
Mwokozi atatuongoza kwenye ukombozi kutoka kwenye majaribu yetu pale tunapokuwa wenye haki zaidi.
- 24 Muziki:** Bustanini Tukufu   
*Na Tammy Simister Robinson*  
Mwokozi aliishi na kufa kwa ajili yetu.
- 26 Masomo matatu Kuhusu Upendo, Shangwe, na Amani**  
*Na Brian K. Ashton*  
Unaweza kupata furaha bila kujali hali zako.
- 32 Sauti za Watakatifu wa Siku za Mwisho**   
**Tufani ikiharibu mipango ya harusi; vile maisha ya hapa duniani yalivyo hasa; wimbo uliotoa tumaini; mwaliko uliokubalika.**
- 36 Baraka za Kujitegemea:** Biashara Inashamiri   
*Na Joshua J. Perkey*  
Mwanasheria anapoteza kazi yake lakini anapata msukumo wa kiungu katika madarasa ya Kanisa ya Kujitegemea.
- 38 Nyumba Zetu, Familia Zetu:** Mwana Wetu ni Mwana wa Baba wa Mbinguni   
*Na Jerlyn Murphy*  
Bila kujali ni kwa kiasi gani tunawapenda watoto wetu, Mungu anawapenda zaidi.
- 40 Kufundisha Vijana na Watoto Wadogo:** Kuvumilia janga   
Vidokezo ya kuwasaidia watoto wako kuhisi amani.

 Kupitia kwa Haraka




**Juu ya Jalada**  
**Barabara ya kwenda Emau,**  
na Wendy Keller.

## Sehemu

### Vijana Wakubwa

42

Pamoja na chaguzi zote tuna-zokumbana nazo na **maamuzi yenye kubadilisha maisha** tunayofanya, ni kwa jinsi gani tunaweza kujua kwamba **tunafuata mpango wa Mungu** kwa ajili yetu? Soma makala za mwezi huu juu ya kupokea ufunuo.



### Vijana

50

Jifunze jinsi ya kutumia baraka zako za kipatriaki, pata msukumo wa kuanza **tamaduni mpya za Pasaka**, na **tafuta amani** kwa ajili yako na wengine unaposoma makala za mwezi huu.



### Watoto

Jifunze zaidi kuhusu **kwa nini tunasherehekea Pasaka** kwa kusoma kuhusu Yesu Kristo, Upatanisho Wake na Ufufuko, na kile vinachomaanisha kwetu.



## MAKALA ZENYE HABARI MAALUMU ZA-KIDIJITALI PEKEE

**Kufanyia mazoezi Misuli Yako ya Kiroho***Na Aspen Stander*

Ili kuzuia kufifia kwa ushuhuda wetu, tunapaswa daima kujenga misuli yetu ya kiroho.

**Je, Unaishi Injili kwa shingo upande?***Na Chakell Wardleigh*

Ni nini hasa tofauti kati ya kuwa mwenye shughuli nyingi Kanisani na kuwa mtendaji katika injili?

## TAFUTA ZAIDI

Kwenye app ya Maktaba ya Injili na kwenye [liahona.Lds.org](http://liahona.Lds.org), unaweza:

- Kupata toleo la sasa.
- Kugundua yaliyomo-ya kidijitali pekee.
- Kutafuta matoleo yaliyopita.
- Kuwasilisha hadithi na majibu yako.
- Kuagiza au kutoa agizo la zawadi.
- Kuzidisha usomaji kwa vifaa vya kidijitali.
- Kushiriki makala na video unazozipenda sana.
- Kupakua au kuchapisha makala.
- Kusikiliza makala yako uipendayo.

## WASILIANA NASI

Tuma barua pepe na majibu yako kwenda [liahona@ldschurch.org](mailto:liahona@ldschurch.org).

wasilisha hadithi yako-inayokuza imani kwenye [liahona.Lds.org](http://liahona.Lds.org) au barua pepe kwenda:

*Liahona*, flr. 23

50 East North Temple Street

Salt Lake City UT 84150-0023, USA

**APRILI 2019 VOL. 6 NO. 1  
LIAHONA 18604 743**

Gazeti la Kimataifa la Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

**Urais wa Kwanza:** Russell M. Nelson, Dallin H. Oaks, Henry B. Eyring

**Akidi ya Mitume Kumi na Wawili:** M. Russell Ballard, Jeffrey R. Holland, Dieter F. Uchtdorf, David A. Bednar, Quentin L. Cook, D. Todd Christofferson, Neil L. Andersen, Ronald A. Rasband, Gary E. Stevenson, Dale G. Renlund, Gerrit W. Gong, Ulisses Soares

**Mhariri:** Randy D. Funk

**Washauri:** Brian K. Ashton, Randall K. Bennett, Becky Craven, Sharon Eubank, Cristina B. Franco, Donald L. Hallstrom, Larry S. Kacher, Erich W. Kopischke, Lynn G. Robbins

**Mkurugenzi Mtendaji:** Richard I. Heaton

**Mkurugenzi wa Magazeti ya Kanisa:** Allan R. Loyborg

**Meneja wa Biashara:** Garff Cannon

**Mhariri Mtendaji:** Adam C. Olson

**Mhariri Mtendaji Msaidizi:** Ryan Carr

**Mchapishaji Msaidizi:** Camila Castrillón  
**Kuandika na kuhariri:** Maryssa Dennis, David Dickson, David A. Edwards, Matthew D. Flitton, Garrett H. Garff, Jon Ryan Jensen, Charlotte Larcabal, Michael R. Morris, Eric B. Murdock, Sally Johnson Odekirk, Joshua J. Perkey, Jan Pinborough, Richard M. Romney, Mindy Selu, Lori Fuller Sosa, Marissa Widdison

**Mkurugenzi Mtendaji Sanaa:** J. Scott Knudsen

**Mkurugenzi wa Sanaa:** Tadd R. Peterson

**Usanifu:** Jeanette Andrews, Fay P. Andrus, Mandie Bentley, C. Kimball Bott, Thomas Child, Joshua Dennis, David Green, Colleen Hinckley, Eric P. Johnsen, Susan Lofgren, Scott M. Mooy, Emily Chieko Remington, Mark W. Robison, Brad Teare, K. Nicole Walkenhorst

**Mratibu wa Haki Miliki:** Collette Nebeker Aune

**Meneja wa Uzalishaji:** Jane Ann Peters  
**Uzalishaji:** Ira Glen Adair, Julie Burdett, Thomas G. Cronin, Bryan W. Gygi, Ginny J. Nilson, Mairissa M. Smith

**Kabla ya Chapa:** Joshua Dennis, Ammon Harris

**Mkurugenzi wa Uchapishaji:** Steven T. Lewis

**Mkurugenzi wa Usambazaji:** Troy R. Barker

Kwa usajili na bei nje ya Marekani na Kanada, nenda kwenye [store.Lds.org](http://store.Lds.org) au wasiliana na kituo cha usambazaji cha Kanisa katika eneo lako ama kiongozi wa kata au tawi.

**Wasilisha miswada na maswali** katika [liahona.Lds.org](http://liahona.Lds.org); na barua pepe [liahona@ldschurch.org](mailto:liahona@ldschurch.org); ama kwa barua *Liahona*, Rm. 2420, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150-0024, USA.

*Liahona* (neno katika Kitabu cha Mormoni linaloanishwa "dira" ama "kielekezi") imechapishwa katika Kialbeni, Kiarmeni, Bislama, Kibulgaria, Kikambodia, Kisebuano, Kichina, Kichina (kilichorahisishwa), Kikroeshia, Kicheki, Kidenishi, Kiholanzi, Kiingereza, Kiestoni, Kifiji, Kifinishi, Kifaransa, Kijerumani, Kigiriki, Kiangaria, Kiaislandi, Kikindonesia, Kiitaliano, Kijapani, Kikiribati, Kikorea, Kilatvia, Kilithuania,

Kimalagasi, Kimarshalizi, Kimongolia, Kinorwei, Kipolishi, Kireno, Kiromania, Kirusi, Kisamoa, Kislovenia, Kihispania, Kiswahili, Kiswidi, Kitagalogi, Kitahiti, Kithai, Kitonga, Kiukreni, Kiurdu, na Kivietinamu. (Masafa hutofautiana kwa lugha.)

© 2019 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa Limepigwa chapa Marekani.

**Taarifa ya Hakimiliki:** Isipokuwa imeelezwa vinginevyo, watu binafsi wanaweza kunakili yaliyomo katika *Liahona* hii kwa matumizi yao binafsi, yasiyo ya kibiashara (ikijumuisha kwa miito ya Kanisa). Haki hiyo yaweza kuondolewa wakati wo wote. Kazi za picha zisinakiliwe kama kuna zuio linaloeleza hivyo kwenye mstari pembeni ya mchoro. Maswali juu ya hakimiliki yaelekezwe kwa Intellectual Property Office, 50 E. North Temple St., FL 13, Salt Lake City, UT 84150, USA; email: [cor-intellectualproperty@ldschurch.org](mailto:cor-intellectualproperty@ldschurch.org).

**For Readers in the United States and Canada:** April 2019 Vol. 6 No. 1. LIAHONA

(USPS 311-480) Swahili (ISSN 2326-3695) is published twice a year (April and October) by The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150. USA Subscription price is \$1.00 per year; Canada, \$1.20 plus applicable taxes.

Periodicals Postage Paid at Salt Lake City, Utah. Sixty days' notice required for change of address. Include address label from a recent issue; old and new address *must* be included. Send USA and Canadian subscriptions to Salt Lake Distribution Center at address below. Subscription help line: 1-800-537-5971. Credit card orders (American Express, Discover, MasterCard, Visa) may be taken by phone or at [store.Lds.org](http://store.Lds.org). (Canada Post Information: Publication Agreement #40017431)

POSTMASTER: Send all UAA to CFS (see DMM 507.1.5.2). NONPOSTAL AND MILITARY FACILITIES: Send address changes to Distribution Services, Church Magazines, P.O. Box 26368, Salt Lake City, UT 84126-0368, USA.

---

**A**meƒufuka!  
Ameƒufuka!  
Sema kwa sauti  
ya shangwe.

*Ameƒungua kifungo chake cha siku tatu;*

*Acha dunia yote na ishangilie.*

*Kifo kimeshindwa; mwanadamu  
yuko huru.*

*Kristo ameleta ushindi.*

*(“Ameƒufuka” Wimbo, no. 199.)*



Unapomkumbuka Mwokozi Pasaka hii,  
unaweza kutembelea [lds.org/go/4195](https://lds.org/go/4195)  
kuona sanaa ya kupendeza na shuhuda  
kutoka kwa Mitume kuhusu sifa za Mwokozi  
ambazo zilifanya Upatanisho Wake na  
Ufufuko viwezekane.



## Bob na Lori Thurston

Walitumikia Misheni ya Cambodia Phnom Penh



*Katika misheni yao ya kwanza pamoja, Bob na Lori Thurston walijifunza kwamba kuhudumu kwenye maana kunaweza kufanyika licha ya vikwazo vya lugha na tofauti za utamaduni kwa sababu sote tu watoto wa Mungu.*

LESLIE NILSSON, MPIGA PICHA

### Bob:

Siku moja tuliweza kusikia sauti ya muziki, na tuligundua hema lilikuwa likipi-gwa. Huko Cambodia, hiyo aidha humaani-sha mtu anafunga ndoa au mtu amefariki.

### Lori:

Tuligundua kwamba mama wa watoto watano au sita alikuwa amefariki punde. Hakukuwa na mume wa kumzungumzia. Watoto waliamka tu na kugundua mama yao alikuwa amefariki.

Binti mmoja alikuwa tu akilia kwa sauti ya makelele. Kupitia mtafsiri, binti alisema, "mimi ndiye mtoto wa kwanza. Nina wadogo zangu hawa wote. Sijui nitafanya nini."

Nilimnyanyua juu kwenye mikono yangu. Ningewezaje kutofanya hivyo? Msichana huyu punde tu alikuwa amepoteza mama yake. Nilizungumza naye kwa kiingereza na kusema, "najua hunielewi, lakini ninaahidi utamwona mama yako tena. Utakuwa SAWA. Hutaachwa peke yako."

Uzoefu wa aina nyingi kama huu ume-tupatia muunganiko maalumu na watu wa Cambodia.

### GUNDUA ZAIDI

Pata Taswira zaidi za Imani kwenye [lds.org/go/18](https://lds.org/go/18).





## Kanuni za Kuhudumu

# KUFANYA

# KUHUDUMU

# kuwe Shangwe

Kuhudumu kwa upendo huleta shangwe kwa wote mtoaji na mpokeaji.

**W**akati mwingine utafutaji wetu wa furaha katika maisha haya unaweza kuonekana kama kukimbia juu ya kifaa cha mazoezi ya kukimbia. Tunakimbia na kukimbia na bado tunahisi kama hatukufika kokote. Kwa baadhi, wazo la kuwahudumia wengine kiurahisi huonekana nyongeza zaidi ya mambo ya kufanya.

Lakini Baba yetu wa Mbinguni anataka tupate uzoefu wa shangwe na ametuambia “wanadamu wapo, ili wapate shangwe” (2 Nefi 2:25). Na Mwo-kozi alifundisha kwamba kuwahudumia wengine ni sehemu muhimu ya jinsi tunavyoleta shangwe katika maisha yetu na katika maisha ya wengine.

### Shangwe Ni Nini?

Shangwe imetolewa maana kama “hisia ya kuridhika kwa hali ya juu na furaha.”<sup>1</sup> Manabii wa siku za mwisho wametoa ufafanuzi juu ya wapi shangwe inatoka na jinsi inavyopatikana. “Shangwe tunayohisi inahusiana kidogo sana na hali za maisha yetu na inahusiana kwa kila kitu na fokasi ya maisha yetu,” alisema Rais Russell M. Nelson. “. . . Shangwe huja kutoka kwa na kwa sababu ya [Yesu Kristo]. Yeye Ndiye kiini cha shangwe yote.”<sup>2</sup>



## Kuhudumu kunaleta shangwe

Wakati Lehi alipokula tunda la mti wa uzima, nafsi yake ilijawa na “shangwe tele” (1 Nefi 8:12). Tamanio lake la kwanza lilikuwa ni kushiriki tunda hili pamoja na wale aliowapenda.

Utayari wetu wa kuwahudumia wengine unaweza kuleta aina hii ya shangwe kwetu na kwao. Mwokozi aliwafundisha wafuasi Wake kwamba matunda tunayoleta wakati tumeunganishwa Naye husaidia kutuletea utimilifu wa shangwe (ona Yohana 15:1–11). Kufanya kazi Yake kwa kuhudumia na kutafuta kuwaleta wengine Kwake kunaweza kuwa uzoe-fu wenye shangwe (ona Luka 15:7; Alma 29:9;

Mafundisho na Maagano 18:16; 50:22). Tunaweza kupata uzoefu wa shangwe hii hata mbele ya upinzani na maumivu (ona 2 Wakorintho 7:4; Wakolosai 1:11).

Mwokozi alituonyesha mfano mkamilifu kwamba moja ya kiini kikuu cha shangwe ya kweli katika maisha ya duni-ani hupatikana kupitia huduma. Tunapowahudumia kaka na dada zetu kama Mwokozi, kwa hisani na upendo katika mioyo yetu, tunaweza kupata uzoefu wa shangwe ambayo inaenda zaidi ya furaha tu.

“Tunapokumbatia [kuhudumu] kwa moyo wa utayari, tuta . . . karibia kuwa watu wa Sayuni na kuhisi shangwe isiyo kifani na wale ambao tumewasaidia katika njia ya ufuasi,” alifundisha Dada Jean B. Bingham, Rais Mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama.<sup>3</sup>

## KIINI CHA SHANGWE YA KWELI

Mwokozi alituonyesha mfano mkamilifu kwamba shangwe ya kweli katika maisha ya duniani inaweza kupatikana kupitia huduma.



## Tunawezaje Kufanya Kuhudumu Kuwe Shangwe Zaidi?

Kuna njia nyingi za kuleta shangwe tele katika kuhudumu kwetu. Hapa kuna mawazo machache:

- 1. Elewa lengo lako katika kuhudumu.** Kuna sababu nyingi za kuhudumu. Hatimaye, juhudi zetu zinapaswa kuwa sambamba na malengo ya Mungu “kuleta kutokufa na uzima wa milele wa mwanadamu” (Musa 1:39). Tunapokubali mwaliko wa Rais Russell M. Nelson wa kuwasaidia wengine katika njia ya agano, tunaweza kupata shangwe katika kushiriki kwenye kazi ya Mungu.<sup>4</sup> (Kwa mengi juu ya lengo la kuhudumu, ona “Kanuni za Kuhudumu: Lengo Litakalobadilisha Kuhudumu Kwetu,” katika *Liahona* ya Januari 2019.)
- 2. Fanya kuhudumu kuwahuu watu siyo majukumu.** Rais Thomas S. Monson mara nyingi alitukumbusha “Kamwe usiruhusu shida ya kutatuliwa kuwa muhimu zaidi ya mtu anayepaswa kupendwa.”<sup>5</sup> Kuhudumu kunahusu kuwependa watu, siyo kuhusu mambo ya kufanya. Tunapooongezeka kwenye kupenda kama Mwokozi alivyopenda, tutakuwa wenye kuchanua zaidi kwenye shangwe ambayo huja kutokana na kuwatumikia wengine.

- 3. Fanya kuhudumu kuwe rahisi** Rais M. Russell Ballard, Kaimu Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, anatumia: “mambo makuu huletwa kupitia vitu vidogo na rahisi. . . . Matendo yetu madogo na rahisi ya ukarimu na huduma yataongeza kwenye maisha yaliyojawa na upendo kwa Baba wa Mbinguni, kujitoa kwenye kazi ya Bwana Yesu Kristo, na hisia za amani na shangwe kila mara tunapomfikia kila mmoja.”<sup>6</sup>
- 4. Ondoa msongo kwenye kuhudumu.** Siyo jukumu lako kutafuta wokovu wa mtu fulani. Hiyo ni kati ya mtu yule na Bwana. Jukumu letu ni kuwapenda na kuwasaidia kumgeukia Yesu Kristo, ambaye ni Mwokozi wao.

## Usicheleweshe Shangwe ya Kuhudumu

Wakati mwingine watu wanasita kuomba msaada unaohitajika, hivyo kutoa huduma yetu kunaweza kuwa hasa kile walichohitaji. Lakini kujilazimisha kwa watu siyo jibu, vilevile. Kuomba ruhusa kabla ya kuhudumu ni wazo zuri.

Mzee Dieter F. Uchtdorf wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alisimulia kuhusu mama mseja aliyepata tetekuwanga—na kisha watoto wake kuu-gua pia. Nyumba ambayo kwa kawaida ilikuwa safi ikawa na mparaganyiko na chafu. Vyombo na nguo chafu zikawa nyingi.

Katika wakati ambapo alihisi kuzidiwa kabisa, akina dada wa Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama walibisha kwenye mlango wake. Hawakusema, “Tujulishe kama tunaweza kusaidia.” Walipoio-na hali, waliharakisha kwenye kutenda.

“Walisafisha nyumba, wakaleta mwangaza na uwazi nyumbani, na wakamwita rafiki alete chakula kilichohitajika sana. Wakati hatimaye walipomaliza kazi yao na kusema kwaheri, walimwacha mama yule kijana akiwa analia—machozi ya shukrani na upendo.”<sup>7</sup>

Wote watoaji na wapokeaji walihisi mwako wa shangwe.

## Kuza Shangwe katika Maisha Yako

Kadiri zaidi tunavyokuza shangwe, amani, na kuridhika katika maisha yetu, ndivyo zaidi tutaweza kushiriki na wengine pale tunapohudumu. Shangwe huja kupitia Roho Mtakatifu (ona Wagalatia 5:22 na Mafundisho na Maagano 11:13). Ni kitu ambacho tunaweza kukiomba (ona Mafundisho na Maagano 136:29) na kukialika katika maisha yetu. Hapa kuna mawazo machache kwa ajili ya kukuza shangwe katika maisha yetu wenyewe:

- 1. Hesabu baraka zako.** Unapotathmini maisha yako, andika katika shajara yako mambo ambayo Mungu amekubariki nayo.<sup>8</sup> Gundua mazuri yanayokuzunguka kote.<sup>9</sup> Kuwa makini kwenye kile kinachoweza kuwa kinakuzuia kuhisi shangwe na andika njia za kukitatua au kuvielewa vizuri zaidi. Wakati wa msimu huu wa Pasaka, tenga muda wa kutafuta muunganiko mkubwa zaidi na Mwokozi (ona Mafundisho na Maagano 101:36).
- 2. Fanyia mazoezi kujali.** Shangwe inaweza kukupata kiurahisi zaidi katika nyakati tulivu za tafakuri.<sup>10</sup> Sikiliza kwa makini kile kinachokuletea shangwe (ona 1 Mambo ya Nyakati 16:15). Kukaa mbali na vyombo vya habari wakati mwingine kunaweza kuwa muhimu ili kufanyia mazoezi kujali.<sup>11</sup>
- 3. Epuka kujilinganisha.** Imesemwa kwamba ulinganishaji ni mwizi wa shangwe. Paulo alionya kwamba wale “wanaojipi ma nafsi zao na nafsi zao, na wakijilinganisha nafsi zao na nafsi zao, hawana akili” (2 Wakorintho 10:12).
- 4. Tafuta ufunuo binafsi.** Mwokozi alifundisha: “Ikiwa utamomba, nawe utapokea ufunuo juu ya ufunuo, maarifa juu ya maarifa, ili uweze kujua siri na mambo ya amani—yale ambayo huleta shangwe, yale ambayo huleta uzima wa milele” (Mafundisho na Maagano 42:61).

## Mwaliko wa Kutenda

Ni kwa jinsi gani unaweza kuongeza shangwe unayopata katika maisha yako kupitia kuhudumu? ■

Kanuni katika makala hii zinaweza kutumiwa katika mwingiliano wetu wa kila siku lakini zimekusudiwa kuwasaidia akina kaka na akina dada wahudumiaji katika juhudi zao za kubariki watu binafsi na familia walizopangiwa.

## MUHTASARI

1. “Shangwe,” en.oxforddictionaries.com
2. Russell M. Nelson, “Shangwe na Kunusurika Kiroho,” *Liahona*, Nov. 2016, 82.
3. Jean B. Bingham, “Kuhudumu Kama Mwokozi Anavyofanya,” *Liahona*, Mei 2018, 106.
4. Ona Russell M. Nelson, “Tunaposonga Mbele Pamoja,” *Liahona*, Aprili 2018, 4–7.
5. Thomas S. Monson, “Kupata Shangwe katika Safari,” *Liahona*, Nov. 2008, 86.
6. M. Russell Ballard, “Kupata Shangwe kupitia Huduma ya Upendo,” *Liahona*, Mei 2011, 49.
7. Dieter F. Uchtdorf, “Kuishi Injili kwa Shangwe,” *Liahona*, Nov. 2014, 120–123.
8. Ona Henry B. Eyring, “Ee Kumbuka, Kumbuka,” *Liahona*, Nov. 2007, 67.
9. Jean B. Bingham, “Kwamba Shangwe Yenu Iwe Timilifu,” *Liahona*, Nov. 2017, 87.
10. Ona Dieter F. Uchtdorf, “Kwa Vitu Vyenyeye Umuhimu Zaidi,” *Liahona*, Nov. 2010, 21.
11. Ona Gary E. Stevenson, “Kupatwa Kiroho,” *Liahona*, Nov. 2017, 46.





Katika nyakati za Kuvunjika Moyo, Mkumbuke

# *Mjane wa Naini*

Hasa tunapohisi kusahaulika au kutoonekana, lazima tukumbuke: Yesu alikuja kumsaidia mjane wakati uleule alipokuwa na hitaji, na Yeye atakuja kwetu vilevile.

**Na Keith J. Wilson**

Profesa mshiriki wa Maandiko ya Kale, Chuo Kikuu cha Brigham Young

**W**akati mwingine katika kupanda na kushuka kwa maisha, tunaweza kuhisi kwamba Mungu hajishughulishi katika maisha yetu ya kila siku. Mipangilio yetu inaonekana kiasi ya kuchosha na ya kukinaisha. Hakuna mabadiliko mengi, na wakati mwingine ni vigumu kuonyesha eneo moja ambapo Mungu moja kwa moja ameingilia katika hali zetu. Wakati wowote ninaposhtushwa na hisia hizi za kutokuwa muhimu katika maisha yangu mwenyewe, mara nyingi namfikiria mwanamke katika Agano Jipya ambaye yawezekana alihisi hivi. Hakutajwa katika maandiko lakini anajulikana kirahisi kwa jina la kijiji chake na kwa wasifu wake wa ndoa.


Mwanamke ni mjane wa Naini, na ndiye mwinjilisti Luka tu anayeandika hadithi yake ya kupendeza. Kwangu mimi anawakilisha kiini cha huduma binafsi ya Mwokozi na jinsi Yeye alivyowafikia waliovunjika moyo, watu wa kawaida wa jamii Yake. Tukio hili kwa sauti linakamilisha suala kuhusu ikiwa Mungu anatufahamu na kutujali.

Muhtasari mfupi wa muujiza kutoka Luka sura ya 7 unafafanua Yesu akizuia maandamano ya mazishi na kimiujiza akimrejsha kijana aliyekufa kwenye uzima. Lakini kuna mengi zaidi ya kuelewa kuhusu mazingira. Kama ilivyo kwa miujiza yote, lakini hasa kwa huu, muktadha ni muhimu kuelewa tukio hili. Nikiwa nimefundisha Chuo Kikuu cha Brigham Young Kituo cha Yerusalemu, nitashiriki nanyi baadhi ya utambuzi binafsi kuhusu muujiza huu.

Naini ilikuwa ni kijiji kidogo cha wakulima wakati wa Yesu, kikijikumbatiza kati ya Mlima More, ambao unaclezea upande wa mashariki wa Bonde la Yezreli. Mji wenyewe ulikuwa nje ya njia iliyotumika mara kwa mara. Ufikiaji wake ulikuwa kwa kupitia njia moja tu. Wakati wa kipindi cha Yesu, makazi haya yangukuwa madogo na masikini kiasi, na yamebaki hivyo tangu awali. Nyakati zingine katika historia yake, mji huu umezungukwa na nyumba chache kama 34 na watu 189 tu.<sup>1</sup> Leo ni makazi ya takribani wakazi 1,500.

Luka anaanza maelezo yake kwa kukumbusha kwamba Yesu alikuwa Kapernaumu siku moja kabla na alimponya mtumwa wa Akida (ona Luka 7:1–10). Kisha tunajifunza kwamba “*siku moja baadaye*” (mstari wa 11; msisitizo umeongezwa), Mwokozi alienda kwenye mji ulioitwa Naini, akisindikizwa na kundi kubwa la wafuasi. Mpangilio ni wa muhimu sana. Kapernaumu iko katika ufuko wa kaskazini wa Bahari ya Galilaya, futi 600 (m. 183) chini ya usawa wa bahari. Naini ni kama maili 30 (km 48) kusini magharibi mwa Kapernaumu kwenye futi 700 (m.213) juu ya usawa wa bahari, hivyo kuhitaji nguvu, kupanda juu ya kilima kwenda Naini. Ili kutembea kutoka Kapernaumu kwenda Naini, ingechukua angalau siku moja au mbili. Hivi karibuni iliwachukua kundi la wanafunzi vijana wa Chuo Kikuu cha Brigham Young Kituo cha Yerusalemu masaa 10 kutembea safari hii kwenye njia za lami. Hii inamaanisha kwamba pengine Yesu aliamka mapema sana au yawezekana alitembea wakati wa usiku ili aweze kuzuia maandamano ya maziishi “*siku moja baadaye*.”<sup>2</sup>

Yesu alipoukaribia mji baada ya safari ya kuchosha, kijana yawezekana alikuwa kwenye miaka 20<sup>3</sup> alikuwa amebewa kwenye kitanda cha mazishi. Luka anatumbea kwamba kijana huyu alikuwa mwana pekee wa mjane, na baadhi ya wanazuoni wanatafsiri maneno ya Kigiriki kumaanisha kwamba hakuwa na mtoto







mwingine.<sup>4</sup> Kundi kubwa la wanakijiji walimsindikiza katika janga hili baya la kifamilia.

Kwa kawaida, kufiwa mwana kungekuwa ni janga kwa yeyote, lakini fikiria kidokezi cha mjane huyu. Ingeweza kumaanisha nini kijamii, kiroho, na kifedha kuwa mjane bila ya mrithi katika Israeli ya kale? Katika utamaduni wa Agano la Kale, iliaminika kuwa wakati mume alipokufa kabla ya uzee, ilikuwa ishara ya hukumu ya Mungu kwa ajili ya dhambi. Hivyo, baadhi waliamini kwamba Mungu alikuwa akitoa adhabu juu ya huyu mjane aliyenusurika. Katika kitabu cha Ruthu, wakati Naomi alipoachwa mjane katika umri mdogo, aliomboleza, “Bwana amenirudisha sina kitu, na Mwenyezi Mungu amenitesa (Ruthu 1:21, Tafsiri ya Kiwango cha Kimataifa).<sup>5</sup>

Siyo tu kulikuwa na maumivu ya kiroho na kihisia, lakini mjane huyu wa Naini alikuwa pia akikabiliwa na ukata wa fedha—hata kuonyesha njaa usoni.<sup>6</sup> Baada ya ndoa, mwanamke alikabidhiwa kwa familia ya mumewe kwa ajili ya ulinzi wa kifedha. Kama mume angekufa, basi utunzaji wake ungekabidhiwa kwa mwanawe wa kuzaa. Sasa wakati mwana wa kuzaa na wa pekee wa mjane huyu alikuwa amekufa, alikuwa mwishoni mwa kamba yake kifedha. Kama mwanawe alikuwa kwenye miaka 20, yawezekana mjane huyu





alikuwa mwanamke wa umri wa kati, akiishi katika mji mdogo, wa mashamba yaliyojitenga, na sasa alijikuta fukara kiroho, kijamii na kifedha.

Kwa usahihi kwenye dirisha jembamba la wakati ambapo wanakijiji walikuwa wamembeba mwana wa mjane huyu ili kumzika, Yesu alikutana na maandamano na alikuwa na “huruma juu yake” (Luka 7:13). Kwa kweli, haya yaweza kuwa maelezo pungufu sana ya Luka. Yesu kwa kiasi fulani alihisi hali ya ufukara wote wa mjane huyu. Pengine alitumia usiku akijibwaga kwenye sakafu yake ya udongo, akimsihi Baba wa Mbinguni kujua sababu. Pengine aliuliza wazi wazi kwa nini Baba wa Mbinguni alimtaka awe na maisha marefu katika dunia hii. Au pengine alikuwa na hofu ya upweke uliobaki ambao angeupata. Sisi hatujui. Lakini tunajua ya kwamba Mwokozi alichagua kuondoka Kapernaumu haraka, ambapo ilimhitaji Yeye kutembea usiku ili kuzuia maandamano ya mazishi muda muafaka kabla hawajauweka mwili ardhini.

Ndiyo, alipoona uso wake uliojaa machozi wakati akitembea nyuma ya maandamano, Yesu alihisi huruma tele kwa

mwanamke huyu—lakini inaonekana kwamba huruma Yake ilikuja kutokana na hisia Yeye alizopata muda mrefu kabla ya Yeye “kutokea” kuzuia msafara ule wa mazishi. Aliwasili pale wakati muafaka wa mahitaji yake.

Yesu kisha alimwambia mjane “usilie” (mstari wa 13). Bila kuwa na woga wa kutoheshimu tambiko, “Aligusa jeneza,” na maandamano “yakasimama.” Kisha Akaamuru, “Kijana, Nakuamuru, Amka.

“Yule maiti akaketi, na akaanza kusema. Na [Yesu] akampa mama yake” (mistari 14–15). Kiuhalisia, umati wa wanakijiji na wafuasi wa Yesu waliingiwa na hofu pale huzuni yao ya pamoja ilipobadilika kuwa shangwe halisi. Wote “wakamtu-kuzua Mungu, wakisema, nabii mkuu ametokea kwetu” (mstari wa 16). Lakini muujiza huu ulikuwa pia kuhusu kuiokoa nafsi moja iliyokata tamaa. Yesu alijua kwamba kuna kitu hakiku-wa sawa kabisa kwa mwanamke huyu—mtu ambaye alidharauliwa katika utamaduni wao. Hali yake ilihitaji umakini Wake wa haraka, hata kama ingembidi kusafiri mbali kuwepo pale kwa uangalifu kwa wakati muafaka. Alijua hali yake ya

kukata tamaa, na Alikuwa haraka. Rais Thomas S. Monson (1927–2018) alizungumzia ukweli usiopingika aliposema, “Siku moja, tutakapoangalia nyuma kwenye vile vilivyokuwa vinaonekana kama bahati katika maisha yetu, tutatambua kuwa labda havikuwa bahati kabisa.”<sup>7</sup>

Sasa, kama tukio hili lilivyo la kuinua, ni lazima liwe zaidi ya hadithi nzuri ya Biblia kwetu. Linathibitisha pasipo makosa kwamba Yesu alijua kuhusu mjane huyu masikini, aliyesahaulika, na fukara. Hasa tunapohisi kusahaulika au kutoonekana au tusio na thamani, lazima tukumbuke: Yesu alikuja kwa mjane katika wakati wake wa uhitaji mkubwa, na Yeye atakuja kwetu vilevile. Kwa kuongezea, somo la pili tunalo-weza kupata kutokana na mfano wa Mwokozi ni umuhimu wa kunyoosha mkono kuwabariki wengine wanaotuzunguka. Wengi ndani ya mduara wako watakuwa wamevunjika moyo kwa nyakati tofauti. Ikiwa unaweza kuwaambia kuhusu “Dada Naini” na jinsi Bwana alivyojua kwa hakika kuvunjika kwake moyo na janga lake

kuu la binafsi, ingeweza kubadilisha usiku kuwa mchana. Kumbuka ugunduzi wenye hisia kali wa Rais Spencer W. Kimball (1895–1985): “Mungu anatuona, na anatuchunga. Lakini mara nyingi ni kwa kupitia mtu mwingine kwamba anakidhi mahitaji yetu.”<sup>8</sup>

Kati ya miujiza yote ya Yesu wakati wa muda Wake duniani, kwangu mimi, michache ni ororo na yenye huruma kama kuhudumu Kwake kwa mjane wa Naini. Unatukumbusha kwamba tuna thamani Kwake na kwamba kamwe Yeye hatatusahau. Hatuwezi kusahau hilo. ■


#### MUHTASARI

1. Ona E. Mills, *Census of Palestine 1931: Population of Villages, Towns, and Administrative Areas* (1932), 75.
2. Ona S. Kent Brown, *The Testimony of Luke* (2015), 364.
3. Ona Brown, *The Testimony of Luke*, 365.
4. Ona Brown, *The Testimony of Luke*, 365.
5. Katika Isaya 54:4 Bwana anamwambia mjane Israeli kuwa “mashutumumu ya ujane wako hutayakumbuka tena” (Tafsiri Mpya ya Kiingereza).
6. Ona Brown, *The Testimony of Luke*, 365.
7. Thomas S. Monson, katika Joseph B. Wirthlin, “Masomo Niliyojifunza katika Safari ya Maisha,” *Liahona*, Mei 2001, 38.
8. *Teachings of Presidents of the Church: Spencer W. Kimball* (2006), 82.



Kuangalia video ya Biblia “Mjane wa Naini,” tembelea [lds.org/go/041917](https://www.lds.org/go/041917).





**Na Rais  
Henry B. Eyring**  
Mshauri wa Pili  
katika Urais wa  
Kwanza

# AMINI KATIKA Ukombozi WA MWOKOZI

Upatanisho na Ufufuko wa Mwokozi unampa Yeye nguvu ya kutuimarisha katika majaribu yetu au kutukomboa kutokana nayo.

**K**wa wale kati yetu ambao tumepoteza wapendwa wetu, njia mbele inaweza kuwa yenye huzuni na upweke—hata zaidi kwa wale wasio na ufahamu na ushuhuda wa Upatanisho na Ufufuko wa Mwokozi Yesu Kristo. Kumbuka wanafunzi Wake wawili wenye shaka wakiwa njiani kwenda Emau. Bwana aliyefufuka alisogea karibu nao na kuwauliza kwa nini walikuwa na huzuni. Luka anatupatia jibu:

“Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote:

“Tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulibisha.

“Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli” (Luka 24:19–21).

Tunapata faraja kutoka kwenye ufahamu na ushuhuda wetu kwamba *Alikuwa* Yeye aliyeikomboa Israeli. *Alikuwa* Yeye ambaye “[alikata] kamba za kifo” (Mosia 15:23). *Alikuwa* Yeye aliyekuwa “limbuko lao waliolala” (1 Wakorintho 15:20). *Alikuwa* Yeye aliyefanya maagano ya hekaluni yawezekane ambayo yanatuunganisha milele na wale “tuliwapenda tangu mwanzo, na tuliwapoteza muda mfupi!”<sup>1</sup>

Katika msimu huu wa Pasaka, ningependa kushiriki sehemu ya ujumbe wa mkutano wa ibada nilioutoa miaka kadhaa iliyopita kuhusu nguvu ya Mwokozi ya ukombozi. Umeniimarisha nilipouandaa na kuutoa. Ninaomba kwamba utawaimarisha ninyi pale mnapousoma.

### **Mwokozi anafahamu Huzuni Wetu**

Maisha hufika kikomo mapema kwa baadhi na hatimaye kwetu sote. Kila mmoja wetu atajaribiwa kwa kukabiliwa na kifo cha mtu tunayempenda.

Siku moja nilikutana na mwanaume ambaye nilikuwa sijamwona toka mke wake alipofariki. Ilikuwa ni nafasi kukutana katika hali ya

mapumziko ya kupendeza. Alikuwa akitabasamu aliponikaribia. Nikikumbuka kifo cha mke wake, nilitoa salamu yangu ya kawaida kwa umakini: “Unaendeleaje?”

Tabasamu lilipotea, macho yake yakawa na majimaji, na akasema kwa utulivu, kwa ari kubwa, “naendelea vizuri. Lakini ni vigumu sana.”

*Ni* vigumu sana, kama wengi wenu mlivyojifunza na sisi sote tutakavyojua wakati mwingine. Sehemu ngumu ya jaribu hilo ni kujua nini cha kufanya kwenye huzuni, upweke, na kupoteza ambako tunaweza kuhisi kana kwamba sehemu yetu imeondolewa. Huzuni unaweza kuendelea kama maumivu ya muda mrefu. Na kwa baadhi, kunaweza kuweko hisia za hasira na kukosekana kwa haki.



Upatanisho na Ufufuko wa Mwokozi unampa Yeye nguvu za kutukombo katika jaribu kama hilo. Kupitia uzoefu Wake, Yeye anaweza kujua huzuni wetu wote. Angeweza kuujua kwa msukumo wa Roho, lakini badala yake Yeye alichagua kuujua kwa kuupitia Yeye mwenyewe. Haya ndiyo maneno:

“Na tazama, atazaliwa na Mariamu, huko Yerusalemu ambayo ni nchi ya babu zetu, yeye akiwa bikira, chombo cha thamani na kilichochaguliwa, ambaye atawezeshwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kupata mimba, na kumzaa mwana, ndio, hata Mwana wa Mungu.

“Na atakwenda, na kuteseka maumivu na masumbuko na majaribio ya kila aina; na hii kwamba neno litimizwe ambalo linasema atabeba maumivu na magonjwa ya watu wake.

“Na atajichukulia kifo, ili afungue kamba za kifo ambazo zinafunga watu wake; na atajichukulia unyonge wao, ili moyo wake ujae rehema, kulingana na mwili, ili ajue kulingana na mwili jinsi ya kuwasaidia watu wake kulingana na unyonge wao” (Alma 7:10–12).

Watu wema wanaokuzunguka watajaribu kuelewa huzuni wako wakati wa kifo cha mpendwa wako. Wanaweza kuhisi huzuni wao wenyewe. Mwokozi haelewi tu huzuni bali pia anahisi huzuni *wako* binafsi ambao wewe pekee unahisi. Na anakujua kikamilifu. Anajua moyo wako.

### **Mwalike Roho Mtakatifu**

Mwokozi anaweza kujua yapi kati ya mambo mengi unayoweza kufanya ambayo yatakuwa bora kwako unapomwalika Roho Mtakatifu kukufariji na kukubariki. Yeye atajua wapi ni pazuri kwako kuanzia. Wakati mwingine itakuwa ni kuomba. Wakati mwingine itakuwa kwenda kumfariji mtu mwingine. Ninafahamu kuhusu mjane aliyekuwa na ugonjwa wa kudhoofisha aliyepata msukumo wa kiungu wa kumtembelea mjane mwingine. Sikuwepo pale, lakini nina hakika kwamba Bwana alimpa

---

*Mwokozi angejua huzuni wetu kwa  
msukumo wa Roho lakini badala yake  
alichagua kuujua kwa kuupitia  
Yeye Mwenyewe.*

msukumo mfuasi mwaminifu kumfikia mwingine na hivyo aliweza kuwasaidia wote.

Kuna njia nyingi Mwokozi anaweza kuwasaidia wale wanaohuzunika, kila moja ikiwa yenye kufaa kwao. Lakini unaweza kuwa na uhakika kwamba Yeye anaweza na atafanya katika njia ambayo ni bora sana kwa wale wanaohuzunika na wale wanaowazunguka. Kitu kimoja kisichobadilika pale Mungu anapowakomboa watu kutokana na huzuni ni kwamba wana-hisi unyenyekevu kama wa watoto mbele Zake. Mfano mkuu wa nguvu ya unyenyekevu wa uaminifu huja kutoka kwenye maisha ya Ayubu (ona Ayubu 1:20–21). Kisichobadilika kingine, ambacho Ayubu pia alikuwa nacho, ni imani ya kudumu katika nguvu ya Ufufuo ya Mwokozi (ona Ayubu 19:26).

Sote tutafufuka, ikijumuisha wapendwa wako waliokufa. Kuunganika huku tena pamoja nao hakutakuwa kwa muda mfupi bali kwa miili ambayo haitakufa kamwe wala kuwa dhaifu.

Wakati Mwokozi alipowatokea Mitume Wake baada ya Ufufuko, Yeye hakuwaondolea tu hofu katika huzuni yao bali pia sisi sote ambao tunge-weza kuhuzunika. Aliwaondolea hofu wao na sisi kwa njia hii:

“Amani iwe kwenu. . . .

“Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe: nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa, kama mnavyoniona mimi kuwa nayo” (Luka 24:36, 39).

Bwana anaweza kutupatia msukumo wa kiungu kuifikia nguvu ya ukombozi kutoka kwenye huzuni katika njia ambayo inatufaa zaidi. Tunaweza kuchagua kuwahudumia wengine kwa ajili ya Bwana. Tunaweza kushuhudia juu ya Mwokozi, juu ya injili Yake, juu ya urejesho wa Kanisa Lake, na juu ya Ufufuo Wake. Tunaweza kutii amri Zake.

Yote kati ya chaguzi hizo humwalika Roho Mtakatifu. Ni Roho Mtakatifu anayeweza kutufariji katika njia inayokidhi hitaji letu. Na kwa msukumo wa Roho, tunaweza kuwa na ushuhuda wa Ufufuo na uoni wa

wazi wa muunganiko mtakatifu mbeleni. Nilihisi faraja hiyo pale nilipoangalia chini kwenye jiwe la kaburi la mtu niliyemfahamu—mtu ninayefahamu kwamba ninaweza hapo baadaye kumkumbatia katika mikono yangu. Kujua hilo, siyo tu nilikombolewa kutoka kwenye huzuni bali pia kujazwa na tumaini la furaha.

Kama mtu yule mdogo angeishi kuwa mkubwa, angehitaji ukombozi katika aina nyingine ya majaribu. Angejaribiwa kubaki mwaminifu kwa Mungu kupitia changamoto za kimwili na kiroho ambazo huja kwa kila mtu. Japokuwa mwili ni uumbaji unaovutia, kuufanya uweze kutenda ni changamoto ambayo hutujaribu sote. Kila mtu lazima ahangaike kupitia ugonjwa na matokeo ya kuzeeka.

#### **“Kuwa Mnyenyekevu”**

Nguvu ya ukombozi kutokana na majaribu yetu ipo. Inafanya kazi kwa njia sawa kama ukombozi kutoka kwenye jaribu katika kukabiliana na kifo cha mpendwa wetu. Kama ukombozi ulivyo si mara zote kuwa uhai wa wpendwa wetu

---

*Mwokozi anaweza na ata-  
saidia katika njia ambayo  
ni bora kwa wale  
wanaohuzunika na wale  
wanaowazunguka.*

utalindwa, ukombozi wa kutoka majaribu mengine si kuwa utayaondoa. Bwana anaweza asitoe unafuu mpaka tuonyeshe imani kwenye kufanya chaguzi ambazo zitaleta nguvu ya Upatanisho kufanya kazi katika maisha yetu. Yeye haitaji hilo kwa sababu hajali bali kwa sababu ya upendo kwetu.

Mwongozo wa kupokea nguvu ya Bwana ya ukombozi kutokana na upinzani katika maisha ulitolewa kwa Thomas B. Marsh, wakati huo akiwa Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili.





Alikuwa katika majaribu magumu, na Bwana alijua angepata mengi zaidi. Hapa ni ushauri kwake ambao ninauchukua kwa ajili yangu na ninautoa kwenu: “Jinyenyekeze; na Bwana Mungu wako atakuongoza kwa mkono, na kukupa jibu la sala zako” (Mafundisho na Maagano 112:10).

Mwokozi daima anataka kutuongoza kwenye ukombozi kupitia sisi kuwa wenye haki zaidi. Hilo linahitaji toba. Na hilo linachukua unyenyekevu. Hivyo njia ya ukombozi daima inahitaji unyenyekevu ili kwamba Bwana aweze kutuongoza kwa mkono pale ambapo Yeye anataka kutupeleka kupitia matatizo yetu na kwenye utakaso.

Majaribu yanaweza kuzaa uchungu au kuvunjika moyo. Unyenyekevu mimi na wewe tunaohitaji kwa ajili ya Bwana kutuongoza kwa mkono huja kutokana na imani. Huja kutokana na imani kwamba Mungu kweli anaishi, kwamba Yeye anatupenda, na kwamba kile Yeye anachohitaji—kigumu kadri kitakavyokuwa—kitakuwa daima bora kwetu.

Mwokozi alitunyeshia unyenyekevu huo. Mmesoma jinsi Alivyoomba katika Bustani ya Gethsemane wakati alipoteseka kwa jaribu kwa niaba yetu kupita uwezo wetu wa kufikiri au kuvumilia, au hata kwangu kuelezea. Mnakumbuka ombi Lake: “Baba, ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki: walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke” (Luka 22:42).

Alimfahamu na kumwamini Baba Yake wa Mbinguni, Elohimu mkuu. Alifahamu kwamba Baba Yake alikuwa na nguvu zote na ukarimu usio na mwisho. Mwana Mpendwa aliomba kwa maneno ya unyenyekevu—kama yale ya mtoto mdogo—kwa nguvu ya ukombozi kumsaidia.

### **Chukua Ujasiri na Faraja**

Baba hakumkomboa Mwana kwa kuondoa jaribu. Kwa ajili yetu Hakufanya hivyo, bali alimruhusu Mwokozi kumaliza kazi aliyokuja kutimiza. Bado daima tunaweza kuchukua ujasiri na faraja kutokana na kufahamu usaidizi ambao Baba alitoa:

“Malaika kutoka mbinguni akamtokea akamtia nguvu.

“Naye kwa vile alivyokuwa katika dhiki akazidi sana kuomba: hari yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka nchini.

“Alipoondoka katika kuomba kwake, akawajia wanafunzi wake, akawakuta wamelala usingizi kwa huzuni,

“Akawaambia, Mbona mmelala usingizi? Ondokeni, mkaombe, msije mkaingia majaribuni” (Luka 22:43–46).

Mwokozi aliomba kwa ajili ya ukombozi. Kile Alichopewa hakikuwa kumbia kutoka kwenye jaribu bali faraja ya kutosha kulishinda kwa shangwe.

Amri Yake kwa wanafunzi Wake, ambao wao wenyewe walikuwa wakaribiwa, ni mwongozo kwetu. Tunaweza kuamua kuufuata. Tunaweza

*Yesu Kristo alilipa deni kwa ajili  
ya dhambi zetu zote na za Watoto wote wa  
Baba wa Mbinguni ili kwamba tungeweza  
kukombolewa kutokana na kifo na dhambi*

kuamua kunyanyuka na kuomba kwa imani na unyenyekevu mkubwa. Na tunaweza kufuata amri iliyoongezwa katika kitabu cha Marko: “Ondokeni, Twendeni zetu” (Marko 14:42).

Kutoka kwenye hili, una ushauri wa kushinda majaribu ya kimwili na kiroho ya maisha. Utahitaji msaada wa Mungu baada ya kufanya yote unayoweza wewe mwenyewe. Hivyo ondoka na uende, lakini pata msaada Wake mapema kadiri uwezavyo, siyo kusubiri hali ya hatari ili kuomba ukombozi.

Ninawapa ushahidi wangu wa dhati kwamba Mungu Baba anaishi na anatupenda. Ninajua hilo. Mpango Wake wa furaha ni mkamilifu, na *ni* mpango wa furaha. Yesu Kristo alifufuka, kama sisi tutakavyofufuka. Aliteseka ili kwamba Yeye aweze kutusaidia katika majaribu yetu yote. Alilipa deni kwa ajili ya dhambi zetu zote na za Watoto wote wa Baba wa Mbinguni ili kwamba tungeweza kukombolewa kutokana na kifo na dhambi.

Ninajua kwamba katika Kanisa la Yesu Kristo, Roho Mtakatifu anaweza kuja kutufaraji na kutusafisha pale tunapomfuata Bwana. Hebu na mpokee faraja Yake na usaidizi katika wakati wenu wa uhitaji, kupitia majaribu yote na taabu za maisha yenu. ■

*Kutoka kwenye hotuba ya mkutano wa ibada, “Nguvu ya Ukombozi,” iliyotolewa katika Chuo Kikuu cha Brigham Young mnamo Januari 15, 2008.*

### **MUHTASARI**

1. “Lead, Kindly Light,” *Nyimbo za Kanisa*, no. 97.



MAELEZO KUTOKA GETSEMAE, NA J. KIRK RICHARDS. MATAWI YA MZEITUNI KUTOKA GETTY IMAGES

# Bustanini Tukufu

*Kwa makini* ♩ = 60-68

Maneno na Muziki na Tammy Simister Robinson

1. Bu - sta - ni - ni tu - ku - fu, Ni - li - pa - ta wo - ko - vu.  
 2. Mwi - li wa - li - je - ru - hi, U - ka - ji - to - a za - wa - di.  
 3. Na ni - ya - nywa - po ma - ji, Na - nye - nye - ke - a mi - mi.

Geth - se - ma - ne Bw - a - na, Ye - su ku - ni - o - mbe - a.  
 Kwa wo - te u - li - te - swa, Ye - su u - li - ni - fi - a.  
 Mwi - li u - li - u - to - a Ni - ta - ku - shu - hu - di - a.

Ye - su ku - ni - o - mbe - a. Chu - ku - a wa - ngu mo - yo.  
 Ye - su u - li - ni - fi - a. Chu - ku - a wa - ngu mo - yo;  
 Ni - ta - ku - shu - hu - di - a. Chu - ku - a wa - ngu mo - yo;

Ni - te - nde ma - pe - nzi yako; Geth - se - ma - ne Bw - a - na,  
 Ni - te - nde ma - pe - nzi yako, Kwa wo - te u - li - te - swa  
 Ni - te - nde ma - pe - nzi yako; Ha - u - ta - te - swa te - na,

Ye - su ku - ni - o - mbe - a Ye - su ku - ni - o - mbe - a.  
 Ye - su u - li - ni - fi - a. Ye - su u - li - ni - fi - a.  
 Ni - ta - ku - fu - a - ta Bwa-na. Ni - ta - ku - fu - a - ta Bwa-na.

© 2003 Tammy Simister Robinson. Haki zote zimehifadhiwa

Wimbo huu unaweza kunakiliwa kwa ajili ya mahitaji, yasiyo ya kibiashara ya matumizi kanisani ama nyumbani.

Notisi hii lazima ijumuishwe katika nakala inayotengenezwa.



**Na Brian K. Ashton**

Mshauri wa Pili katika Urais  
Mkuu wa Shule ya Jumapili

# Masomo matatu juu ya Upendo, Shangwe, na Amani

---

Kufuata hatua hizi tatu kunaweza kuleta tofauti kubwa katika maisha yako na kukusaidia kuhisi matunda ya Roho.

**N**ilipokuwa mwanafunzi wa chuo, niliwaza sana kuhusu siku zangu za mbeleni. Nili-pofika kwenye siku hizo—nikimaanisha maisha baada ya chuo—nilijifunza masomo muhimu matatu ambayo yalileta tofauti kubwa katika maisha yangu. Ninataka kushiriki nanyi masomo haya kwa tumaini kwamba hamtachukua muda mrefu kama niliochukua kujifunza masomo hayo. Yana-weza kuwasaidia kupata shangwe tele katika maisha—na hatimaye kupata kuinuliwa na Baba yenu wa Mbinguni.

## **1. Tafuta Furaha, Amani, na Roho Mtakatifu**

Nilikutana na mke wangu, Melinda, wakati nikiwa mwanafunzi wa mwaka wa pili chuoni, takribani miezi sita baada ya kurudi kutoka kwenye misheni yangu. Nilijua mara moja kwamba nilitaka kumuoa Melinda. Melinda, hata hivyo, hakuwa na uzoefu sawa na wangu. Haikuwa hivyo mpaka miaka mitano baadaye kwamba



---

*Unapofanya  
mambo madogo  
na kuamini  
katika dhabihu  
ya Yesu Kristo,  
unaweza  
kupata upendo,  
shangwe,  
na amani  
licha ya  
hali zako.*

hatimaye alipokea jibu kwamba ilikuwa “SAWA” kama angeolewa nami.

Katika kipindi hicho cha miaka mitano, nilipata moja ya jaribu zito zaidi la maisha yangu. Nilijua nani nilipaswa kumuoa, na Roho alinisihi sana, lakini sikuonekana kufikia lengo hilo.

Muda mfupi baada ya kuhitimu, Melinda aliamua kwenda misheni—kwa sehemu, nashawishika, alitaka kuwa mbali na mimi. Kulikuwa na nyakati wakati akiwa katika misheni yake nilipokuwa na huzuni kwa sababu nilifokasi kwenye kile nilichokosa. Hata hivyo, nilikuwa nikisoma maandiko na kusali kila siku, kutumikia Kanisani, na kujitahidi kufanya mambo yaliyomkaribisha Roho Mtakatifu katika maisha yangu.

Mapema, asubuhi ya Jumapili moja yenye baridi sana huko Minneapolis, Minnesota, Marekani, nilipokuwa nikiendesha gari kwenda kwenye mkutano wa Kanisa, niliwaza, “ninapaswa kuwa mwenye huzuni sana muda huu. Hakuna kilichoonekana kwenda jinsi nilivyotaka. Lakini sina huzuni. Ninahisi furaha isiyoelezeka!”

Sasa, ni kwa jinsi gani ningeweza kuwa na furaha kama nilikuwa napitia kile, ambacho kwangu, kilikuwa jaribu zito?

Jibu linapatikana katika Wagalatia 5:22–23: “Tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi.”

Kwa sababu nilikuwa nikifanya mambo yanayomwalika Roho katika maisha yangu, nilihisi upendo wa Mungu. Nilihisi furaha na amani. Ningeweza kuteseka kwa muda mrefu na bado kuwa na furaha.

Kuwa na upendo, furaha, na amani katika maisha yetu, familia zetu, na ndoa zetu hakuji kutokana na kuwa na nyumba kubwa, gari nzuri, nguo

zilizo kwenye fasheni, mafanikio ya kazi, au lolote kati ya mambo mengine ulimwengu unayosema yanaleta furaha. Kwa kweli, kwa sababu hisia za upendo, furaha, na amani huja kutoka kwa Roho, kuzihisi hakuhitaji kuhusisha hali zetu za kimwili kabisa.

Tafadhali eleweni kuwa sisemi kwamba daima tutakuwa na furaha au kwamba hali zetu za kimwili kamwe haziathiri furaha yetu. Kwa kweli, kama hatuonji uchungu, hatuwezi kujua utamu (ona Mafundisho na Maagano 29:39; ona pia Musa 6:55).

Tunahitaji kuteseka wakati mwingine.

Zaidi ya hayo, baadhi ya hali za kimwili na kihisia zinaweza kutusababishia mateso mazito na kufanya iwe vigumu kwetu kuhisi Roho. Lakini ikiwa tunajitahidi kuwa na Roho katika maisha yetu na tunamwamini Mungu, tunaweza, kwa ujumla, kuwa na furaha.

Ninashuhudia kutokana na uzoefu binafsi kwamba hii ni kweli. Tangu uzoefu wangu wakati Melinda akiwa kwenye misheni yake, nimegundua kwamba kama ninafanya mambo yanayomwalika Roho katika maisha yangu, ikijumuisha kuchagua kuamini na kukubali kwamba mambo yataenda sawa kama Mungu anavyokusudia, daima ninakuwa na furaha (ona Yakobo 3:2).<sup>1</sup>

### **Usiangukie kwenye Kisicho Halisi.**

Shetani anatoa kisicho halisi kama mbadala wa yote Mungu anayofanya ili kujaribu kutukanganya na kutudanganya. Licha ya juhudi za shetani kutushawishi vinginevyo, Mwokozi anatumia kwamba “mti mbaya [hauwezi] kuzaa matunda mema” (3 Nefi 14:18). Kwa sababu shetani ni mti mbaya, hawezi kutusababisha kuhisi “upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, [na] kiasi” (Wagalatia 5:22–23). Badala yake, Shetani anataka kutufanya wenye huzuni (ona 2 Nefi 2:27).

Basi ni nini Shetani anafanya? Anajaribu kutudanganya.

Rafiki yangu, mmoja wa wateule, alidanganywa. Rafiki yangu alitumikia misheni na alikuwa mmisionari wa kufana. Aliporudi nyumbani kutoka kwenye misheni yake, alikusudia kufanya mambo madogo yote ambayo yalimwalika Roho katika maisha yake na yaliyomuimarisha katika misheni yake. Na kwa muda, alifanya.

---

*Shetani anatoa  
kisicho halisi  
kama mbadala  
wa yote Mungu  
anayofanya ili  
kujaribu  
kutukanganya  
na kutudanganya.  
Mwokozi  
anatumfundisha  
kwamba “mti  
mbaya [hauwezi]  
kuzaa matunda  
mema”*

(3 Nefi 14:18).

Hata hivyo, aliwaona marafiki, wengi wao wakiwa wamisionari waliorudi, wakija kanisani kila jumapili lakini nje ya kanisa wakiishi kama ulimwengu ulivyoishi. Walionekana wenye furaha. Walikuwa wakifanya vitu vyenye kuleta “kuchangamsha”. Na mtindo wao wa maisha haukuonekana kuhitaji juhudi kubwa kama yake ilivyohitaji.

Taratibu aliacha kufanya mambo madogo madogo ambayo yalikuwa yamemletea nguvu ya kiroho kwenye misheni yake. Bado alikuwa na ushuhuda, lakini aliniambia kwamba alikuwa amehitimisha, “Kama nilikuwa nahudhuria tu mikutano yangu ya Kanisa, nilikuwa SAWA—nilikuwa kwenye njia.” Hata hivyo, alisema, “Kiroho, nilikuwa mlegevu.”<sup>2</sup> Pale alipoishi kama ulimwengu ulivyoishi, uchaguzi mmoja mbaya ulipelekea mwingine, na punde akapata ujauzito.

Chaguzi zake zisizo za haki hatimaye zilimnasa. Hakuwa na furaha, na alijua hilo. Kwa bahati nzuri, rafiki yangu aligundua kwamba alikuwa amedanganywa, na alitubu.

Hadithi yake inasisitiza kwamba hata walio bora kati yetu wanaweza kudanganywa. Zaidi ya hayo, hadithi yake inaonyesha kwamba lazima siku zote tuweke ulinzi dhidi ya udanganyifu. Tunafanikisha hili kwa kufanya mambo madogo ambayo humwalika Roho katika maisha yetu.

Nina furaha kusema kwamba leo rafiki yangu ni mwenye furaha, anajitahidi kutii amri, na yuko hai kimwili na kiroho katika injili.

Udanganyifu wa Shetani huja kwa njia nyingi. Nitataja chache tu.

Shetani hujaribu kutushawishi kuyapa kipau-mbele mambo ya muda kuliko mambo ya kiroho. Tunaweza kuona kama vipaumbele vyetu si vya kiroho kwa kugundua mara nyingi kiasi gani tunasema, “nina shughuli nyingi au nimechoka

sasa hivi ku \_\_\_\_\_.” Jaza nafasi iliyo wazi: kuhudhuria hekaluni, kuhudumu, kujifunza na kutafakari maandiko, kutimiza wito wangu, au hata kuomba.

Sababu moja ya sisi kuhisi tuna shughuli nyingi ni kwamba Shetani anafanya kazi kwa bidii kutuvuruga. Anatomia simu viganjani mwetu, redio ndani ya gari zetu, televisheni nyumbani mwetu, na vitu vingine vingi kutufanya tuvurugwe karibu kila wakati. Kama matokeo, tunahisi tuna shughuli nyingi kuliko ilivyo hasa.

Matokeo mengine ya uvurugaji huu ni kwamba tunatafakari kidogo sana. Shetani anafanya kazi kutuvuruga kwa sababu anajua kwamba kutafakari, hasa maandiko, hupelekea uongofu mkubwa na ufunuo.

Lingine la udanganyifu wa Shetani huja kupitia wazo kwamba matendo

yetu ya nje yana maana sana kuliko msukumo wa ndani. Wakati tunapokosa msukumo sahihi wa kufanya mambo ya kiroho, tunashindwa kupata uzoefu wa shangwe ya injili. Kama matokeo, kutii amri kunaanza kuonekana kama kazi ngumu, na shetani anajua kwamba kama akifanikiwa kutufanya tuhisi hivi, kuna uwezekano wa kuacha kufanya kile tunachojua tunapaswa kufanya.

Shetani pia anatudanganya kwenye kuamini kwamba shangwe na furaha vinakuja kutokana na kuwa na maisha rahisi au kwa kuburudika tu wakati wote. Haviji kwa namna hiyo. Ukweli ni kwamba hakuna shangwe au furaha bila kitu cha kushinda (ona 2 Nefi 2:11, 23).

La mwisho kati ya udanganyifu wa Shetani nitakalolitaja ni kwamba anajaribu kutushawishi kwamba uovu, na burudani yake ya muda mfupi, kweli ni furaha. Shetani anajua kwamba, angalau kwa muda, hisia fulani zinaweza (1) kutufanya tudhani kwamba tunahisi matunda ya Roho, (2) kutuvalisha kinyago cha matamano yetu kwa matunda hayo, au (3) kuhisi kama mbadala unaokubalika.



Kwa mfano, Shetani anaweza kutujaribu sisi tutafute matamano kwenye nafasi ya upendo. Anaweza kutuvutia kwa furaha badala ya shangwe ya kudumu. Anajaribu kutuvuruga kuliko kutupatia amani. Angetufanya tuwe wenye kujisikia wenye haki katika macho yetu wenyewe, wenye ari, na sahihi kisiasa badala ya kutokuwa wabinafsi, watiifu daima, na wenye fokasi ya kiroho inayofaa. Majaribu yake yanaweza kutusababisha kuchanganyikiwa, ambayo huweza kutupelekea kufikiri kwamba kutokutii amri kutaleta furaha.

### 3. Fanya Mambo Madogo

Kwa kawaida ni mambo madogo ambayo humleta Roho katika maisha yetu, hutulinda dhidi ya kudanganywa, na hatimaye hutusaidia kupata nguvu ya kutii amri na kupata uzima wa milele. Mwokozi alifundisha kanuni hii kwa wazee wa Kanisa huko Kirtland, Ohio: “Kwa hiyo, msichoke kutenda mema, kwa kuwa mnaijenga misingi ya kazi kubwa. Na kutokana na mambo madogo huja yale yaliyo makuu” (Mafundisho na Maagano 64:33).

Kwa nini mambo madogo ni muhimu sana? Katika mstari unaofuata, Mwokozi alielezea kwamba “Bwana anahitaji moyo na akili yenye kukubali” (Mafundisho na Maagano 64:34). Kwa nini Mwokozi aliunganisha kufanya mambo madogo na moyo na akili yenye kukubali? Kwa sababu kwa kuendelea kufanya mambo madogo, tunaiweka mioyo na akili zetu kwa Mungu, ambako kunatusafisha na kututakasa (ona Helamani 3:35.)

Kusafishwa na kutakaswa huku hubadilisha asili yetu hasa, kidogo kidogo, ili kwamba tuwe zaidi na zaidi kama Mwokozi. Hii pia hutusababisha kuwa wasikivu zaidi kwa msukumo

wa Roho Mtakatifu, ambao hutufanya tuwe na uwezekano mdogo wa kudanganywa.

Katika mwaka wangu wa shule ya upili, baba yangu alinifundisha seminari nyumbani kwetu. Kwa sababu mada ya mwaka ule ilikuwa Kitabu cha Mormoni, baba yangu aliamua kwamba tungekisoma pamoja, mstari kwa mstari, na kujadili kile tulichojifunza. Tuliposoma, baba yangu angeuliza maswali ambayo yalinifanya nifikirie kuhusu kile tulichokuwa tunasoma, na angefafanua mambo ambayo sikuyaelewa. Bado naku mbuka kujifunza kuhusu Mwokozi na kuhisi kwamba kweli aliwatembelea Wanefi na kwamba kweli ningeweza kusamehewa dhambi zangu kwa sababu ya Upatanisho Wake.

Ninafuatisha msingi wangu katika maandiko kwenye vikao vile mimi na baba yangu tulivyo kuwa navyo pamoja. Nilihisi kitu tuliposoma. Na pengine muhimu zaidi, matamaniao yangu, sababu ya kufanya jambo, na matendo vili badilika. Nilitaka kuwa mzuri zaidi. Nilianza kuona wapi nilikuwa nikidanganywa. Nilitubu kile mara. Mwishoni mwa mwaka wangu wa mwisho chuoni, nilikuwa nikisoma maandiko kila siku.

Katika wakati huu, Rais Ezra Taft Benson (1899–1994) aliwaomba waumini wa Kanisa kuso ma Kitabu cha Mormoni kila siku na kufanyia kazi kile walichojifunza.<sup>3</sup> Hivyo, kwa kuongezea kwenye kingine nilichokuwa nikisoma, nilisoma angalau kitu kutoka kwenye Kitabu cha Mormoni.

Kwenye misheni yangu nilijifunza jinsi ya kusoma hasa na kusherehekea maandiko. Siyo tu nilihisi Roho Mtakatifu niliposoma, bali pia nilianza kuhisi shangwe nilipoyapekua maandiko kutafuta majibu kwa matatizo yangu na yale ya watu niliokuwa nikiwafundisha.





---

*Ninaahidi  
kwamba ikiwa  
utasherehekea  
maandiko kila  
siku, hasa  
Kitabu cha  
Mormoni,  
utamwalika  
Roho  
kwenye  
maisha yako.*

Baada ya misheni yangu, niliendelea kusherehekea maandiko kila siku. Kwa sababu utamaduni huu ulialika Roho Mtakatifu kwenye maisha yangu, nilipokea mwongozo Wake kunisaidia kutumia muda wangu kwa ufanisi zaidi. Kama matokeo, nilifanya vizuri shuleni na, baadaye, kazini. Ilikuwa rahisi kufanya chaguzi nzuri. Niliomba zaidi na nilikuwa mwenye bidii zaidi katika kutimiza miito yangu. Kusherehekea maandiko kila siku haku-kutatua matatizo yangu yote, lakini maisha yalikuwa rahisi.

Mnamo Agosti 2005, Rais Gordon B. Hinckley (1910–2008) alitoa changamoto ya kusoma au kusoma kwa mara nyingine Kitabu cha Mormoni kabla ya mwisho wa mwaka.<sup>4</sup> Kwa sababu nilikuwa nikisoma kutoka kwenye Kitabu cha Mormoni kila siku, nilikuwa tayari kwenye Etheri au Moroni. Kwa hiyo, baada ya kumaliza wiki moja au mbili baadaye, nilihitimisha kwamba nilikuwa nimemaliza changamoto ya Rais Hinckley.

Lakini kisha mwalimu wa nyumbani mwamini-fu alikuja kutembelea familia yetu. Aliniuliza mae-ndeleo yangu kwenye mwaliko wa Rais Hinckley.

Nilimwambia kwamba nilikuwa na bahati nzuri ya kuanza Kitabu cha Mormoni kabla ya changamoto ya Rais Hinckley. Kisha, kwa kujipa haki, nilitangaza kwamba nilikuwa nimemaliza jukumu.

Kwa bahati nzuri, mwalimu wangu wa nyumbani aliona mambo kitofauti. Pale taratibu aliponisahihisha, Roho alininong'oneza kwamba mwalimu wangu wa nyumbani alikuwa sahihi.

Sasa nilitakiwa kusoma sura mbili kila siku ili kumaliza tena ifikapo mwisho wa mwaka.

Nilipoongeza kasi ya kusoma katika Kitabu cha Mormoni, niligundua kwamba hata nguvu zaidi ilikuja katika maisha yangu. Nilikuwa na shangwe zaidi. Niliona mambo kwa uwazi zaidi. Nilitubu mara nyingi zaidi. Nilitaka kuwatumikia na kuwa-okoia wengine. Sikuweza kuathirika kirahisi na udanganyifu na majaribu ya Shetani. Nilimpenda Mwokozi zaidi.

Novemba ile niliitwa kuwa askofu wa kata yetu. Kukamilisha changamoto ya Rais Hinckley kuliniandaa kwa wito huo. Tangu hapo, nimegundua kwamba kadiri ninavyokuwa na shughuli nyingi iwe kazini au kanisani, ndivyo zaidi

ninahitaji kusoma maandiko, hasa Kitabu cha Mormoni.

Unaweza kuwa na baraka na nguvu sawa na hiyo katika maisha yako ikiwa nawe pia utasherehekea maandiko kila siku. Ninaahidi kwamba ikiwa utasherehekea maandiko kila siku, hasa Kitabu cha Mormoni, utamwalika Roho kwenye maisha yako na kiuhalisia utaomba kila siku, utatubu mara nyingi zaidi, na kuona ni rahisi kuhudhuria kanisani na kupokea sakramenti kila wiki.

Ninashuhudia kwamba unapofanya mambo madogo na kumwamini Bwana, unaweza kupata upendo, shangwe, amani, na furaha bila kujali hali zako. Ninashuhudia pia kwamba hii imewezekana kwa sababu ya dhabihu ya Yesu Kristo. Kila kitu kizuri huja kwa sababu Yake (ona Moroni 7:22, 24). ■

*Kutoka kwenye hotuba ya mkutano wa ibada, "Furaha, Uwongo, na Mambo Madogo," iliyotolewa katika Chuo Kikuu cha Brigham Young mnamo Novemba 5, 2017.*

#### MUHTASARI

1. Tunapokuwa imara katika imani ya Kristo, tunaweza kusherehekea upendo wa Mungu bila kujali hali zetu.
2. Muhtasari na nakala ya usahili katika umiliki wa mwandishi.
3. Ona Ezra Taft Benson, "Jukumu Takatifu," *Ensign*, Mei 1986, 77–78; ona pia "Kitabu cha Mormoni—Jiwe Kuu la Tao la Dini Yetu," *Ensign*, Nov. 1986, 4–7.
4. Ona Gordon B. Hinckley, "Ujumbe waUrais wa Kwanza: Ushuhuda wa Kusisimua na wa Kweli," *Ensign*, Agosti. 2005, 2–6.

# Siyo Hata Tufani Ingeweza Kutuzuia

**M**uda mfupi baada ya kurudi kutoka kwenye misheni yangu, nilipokea mwaliko wa kwenda kwenye dansi. Kwenye dansi, nilisahau nilipoweke simu yangu na mvulana alijitolea kunisaidia kuitafuta. Tulipokuwa tukizungumza, tuligundua wote tulikuwa wamisionari waliorudi na tulishiriki mawazo mengi na malengo.

Uhusiano wetu uliendelea kukua, na tukachumbiana. Ilikuwa ndoto yetu kuunganishwa katika Hekalu la Washington D.C. Kabla halijafungwa kwa ajili ya ukarabati mnamo Machi 2018. Lakini baada ya kufanya uamuzi huo, tulijaribiwa. Kwanza, nilipoteza kazi yangu na sikuwa na njia ya kuweka akiba pesa kwa ajili ya safari yetu ya hekaluni. Pili, tufani ilikuwa njiani kupiga Puerto Rico kabla ya siku yetu ya harusi.

Wakati Tufani Maria ilipopiga, iliharibu kisiwa chetu cha kupendeza.

Maduka yalifungwa. Hatukuwa na umeme; maji, chakula, na vitu vingine vya muhimu vilikuwa vigumu kupatikana. Tulipoteza kila kitu tulichokuwa tumeandaa kwa ajili ya tafrija yetu. Ilibidi tuahirishe tafrija, na ilionekana kama ingetubidi kuahirisha harusi yetu pia. Kusafiri nje na ndani ya Puerto Rico kulizuiliwa, na hakuna aliyejua ingekua kwa muda gani. Nilianza kuhisi kuvunjika moyo, na nilijawa na mashaka na kuchanganyikiwa.

Usiku mmoja, mimi na mchumba wangu tulizungumzia hali yetu. Kusafiri hakukuwa kwa uhakika, na tusingekuwa na tafrija au mavazi ya harusi, lakini Roho alithibitisha kuwa tulihitaji kumwamini Bwana. Jambo la muhimu zaidi lilikuwa ni kuunganishwa hekaluni. Tuliomba kwa Baba wa Mbinguni kwa ajili ya usaidizi.

Pale usafiri wa kutoka nje ya Puerto Rico uliporejwa, tulitakiwa kufanya

upya mipango ya safari na kupanga upya tarehe ya kuunganishwa kwetu. Hatukuwa na mawasiliano kwa wiki kadhaa baada ya tufani, lakini simu ya rafiki ilifanya kazi. Alitupatia tuitumie kuwasiliana na watu wa hekaluni. Tulitweza kupanga upya kila kitu hii tuweze kuunganishwa! Wiki chache kabla ya safari yetu, wanafamilia walijitolea viatu na nguo na kutusaidia kupata vitu vingi kwa ajili ya harusi yetu.

Pale hatimaye tulipoingia hekaluni, tuliacha mashaka yetu yote nyuma. Tulishikana mikono kuingia kwenye wakati wetu ujao pamoja. Ninaweza kwa kweli kusema nilihisi mkono wa Bwana ukituongoza na kutuhakikishia kwamba kadiri tulivyomuamini Yeye, kila kitu kingekuwa SAWA. Leo, tumebarikiwa kuwa na mtoto mzuri wa kiume na sisi ni familia iliyounganishwa milele. ■

**Koraima Santiago de Jesus, San Juan, Puerto Rico**

**B**aada ya Tufani Maria, ilionekana kama ingebidi tuahirishe harusi yetu.





## “Hivyo Ndivyo Ilivyo!”

**N**ilifika nyumbani nikiwa nimechelewa usiku mmoja wa majira ya baridi baada ya kufanya usahili mwingi kama askofu. Nilikuwa nimechoka. Kazi ilikuwa na uzito mkubwa kwa wiki kadhaa, na familia na majukumu ya Kanisa vilinifanya nihisi kujinyoosha kupita kikomo changu.

Jioni ile, ilinibidi kurekebisha gari yangu ili niweze kufika kazini asubuhi iliyofuata. Nilipovaa nguo zangu za kazi, nilibadilisha majukumu kutoka kuwa askofu na kuwa makanika. Nili-lala juu ya sakafu ya baridi ya gereji chini ya gari na kuanza kazi. Kwa nini ilikuwanipate baridi, uchovu, na kuvunja konzi zangu baada ya kuwa tayari nimefanya kazi kwa bidii siku hiyo? Nilikuwa nikipoteza subira yangu na kuanza sala ya kulia, kumsihi Baba wa Mbinguni.

“Je, inawezekana Ungeweza kunisaidia kidogo?” nilisema. “Ninajaribu kila niwezalo kuwa baba, mume, na askofu mwema na kuishi kulingana na amri. Je, nisingeweza kuhudumu vizuri zaidi ikiwa ningepata mapumziko kidogo?”

Tafadhali nisaidie nifanikishe hili ili niende kulala.”

Ghaffa, maneno matatu dhahiri, ya kipekee yalikuja kwa ushujaa kwenye akili yangu: “Hivyo ndivyo ilivyo!”

“Nini?” Nilijibu.

Maneno yalikuja tena: “Hivyo Ndivyo Ilivyo!”

Uelewa ulianza kuijaza akili na moyo wangu wakati maneno yalipokuja kwa mara ya tatu: “Hivyo ndivyo ilivyo!” Maneno yalipeleka ujumbe kwenye moyo wangu. “Yalikuwa” ni maisha ya dunia, na nilikuwa nikipitia muda wa ukuaji uliokusudiwa kunisaidia mimi kuwa kile Baba wa Mbinguni anataka niwe. Ilikuwa ni kama Roho aliniambia, “Je, ulitegemea safari hii ya dunia kuto-kuwa na mahangaiko?” Niliponyanyuka kutoka kwenye ile sakafu ngumu ya baridi, sikuwa vilevile.

Kutegemeana na jinsi tunavyoitikia, majaribu yanaweza kuonekana kama zawadi kutoka kwa Baba wa Mbinguni mwenye upendo. Anatupatia fursa ya kupata majaribu ili tuweze kujifunza kumgeukia. Tunapofanya hivyo,

**N**ilikuwa nikitengeneza gari yangu wakati ujumbe wa wazi ulipokuja kwa ushujaa kwenye akili yangu.

tunabarikiwa kwa ukuaji wa kujifunza na kiroho.

Maneno matatu yalivyokuja akilini mwangu usiku ule wenye baridi juu ya sakafu ngumu ya gereji yangu yamenibariki kwa zaidi ya miaka 35. Najaribu kwa bidii kuona kwamba hakuna jaribu lisilofaa. Ninaona majaribu kama fursa za kujifunza mambo ambayo nisingeweza kujifunza kwa njia nyingine yoyote. ■

**Richard J. Anderson, Utah, Marekani**

# Kumuona Baba Akiimba

**N**imekuwa katika misheni yangu huko Honolulu, Hawaii, Marekani, kwa miezi minne na nusu tu wakati nilipopata mshtuko mkubwa wa moyo na baadaye kubainika kuwa na kifafa. Miezi iliyofuata ilileta matembezi ya hospitali, vipimo visivyo na idadi, na dawa mpya yenye matokeo ya kukatisha tamaa.

Kabla ya hapo, nilikuwa nimefokasi sana kwenye kazi ya umisionari kiasi kwamba sikufikiria nyumbani, lakini tangu wakati wa mshtuko wangu wa moyo, moyo ulipata maumivu. Niliwakosa wazazi wangu na kuhisi mpweke hata wakati nilipozungukwa na watu wema, wenye kujali. Sikutaka kwenda nyumbani, bali nilitaka kuhisi amani.

Kwa ruhusa ya rais wangu wa misheni, nilizungumza na wazazi wangu kwenye simu kuhusu matibabu yangu. Baba yangu, ambaye alikuwa

ametimiza ndoto yake ya maisha yote ya kujiunga na Kwaya ta Tabernacle ya Temple Square, alinihakikishia kwamba angeimba kwa moyo wake wote kwa ajili yangu katika mkutano mkuu, ambao ulianza siku iliyofuata.


Asubuhi iliyofuata, niliomba kwa dhati kwa ajili ya amani ambayo niliihitaji sana. Nilikuwa nimepokea majibu kwa maswali mahususi wakati wa mkutano mkuu kabla, na niliamini kwamba ningeweza kupokea mwongozo tena. Mkutano ulipoanza, kwaya iliimba “Dearest Children, God Is Near You,” (*Nyimbo za Kaniisa*, na. 96). Ndani ya dakika ya kwanza, nilimwona baba yangu kwenye sikirini ya TV. Kamera ilimulika na kuvuta uso wake kwa muda kadhaa.

Machozi yalikuja machoni mwangu wakati hisia nzuri mno za amani zilionifunika. Nilijua ya kwamba Mungu

alinipenda. Yeye alijua kile hasa nilichohitaji siku ile—hakikisho rahisi kwamba Yeye alikuwa karibu na alikuwa akini-fahamu. Nilihisi upendo wa Mungu, na kwa nyongeza, upendo wa familia yangu, wenza wangu, na rais wangu wa misheni. Badala ya kuhisi kulemewa, sasa niliona fursa ya kusogea karibu na Bwana.

Changamoto zangu za kiafya hazikuondoka. Ilinibidi nikatishe misheni yangu mapema baada ya yote, lakini nilijua kwamba Mungu alikuwepo pale na kwamba Yeye alinipenda. Hakikisho hilo limenifuata kupitia maumivu mengine mengi ya moyo na limenipa tumaini katika saa zangu za giza. Wengine wanaweza kuiita bahati, lakini ninajua kwamba kumwona baba akiimba kuhusu upendo wa Mungu ulikuwa ni muujiza mdogo katika wakati wangu wa uhitaji. ■

**Maria Oka, California, Marekani**



**M**achozi yalikuja machoni mwangu pale nilipomwona baba yangu kwenye sikirini ya TV.

# Mwaliko kwa ajili ya Ricardo

**N**inaposikia kuhusu shughuli ya Kanisa, daima huwa ninawaalika watu 10 ambao siyo waumini wa Kanisa kuhudhuria. Nimefanya hili kwa miaka mingi. Ninatengeneza mialiko na kuuweka kila mmoja ndani ya bahasha nyeupe na kumwomba Roho aniongoze. Kisha ninatoa mialiko. Mara chache wote 10 wanahudhuria, lakini hata kama mmoja tu anahudhuria, ninahisi nimefanikiwa.

Miaka kadhaa iliyopita, niliandaa mialiko kumi kwa ajili ya shughuli ya wanandoa. Nilitoa tisa kwa watu kazini na kubaki na moja. Sikujua nani wa kumpa. Dakika chache baadae, Ricardo, mwakilishi wa mauzo, alipita karibu na meza yangu. Nilihisi msukumo wa kumualika, japokuwa alikuwa amekataa mwaliko kutoka kwa mfanyakazi mwenza wa kuhudhuria tukio kanisani kwake. Sikudhani Ricardo angevutiwa.

Lakini Ricardo alipopita karibu na meza yangu tena akielekea nje, nilihisi msukumo tena. Hata hivyo, alitoka haraka kiasi kwamba sikupata nafsi ya kuzungumza naye. Nilisali kwamba Ricardo angerejea ikiwa nilipaswa kumpa mwaliko.

Baada ya kumaliza kusali, Ricardo alirudi kuniuliza swali. Baada ya hapo, nilisema, “Ricardo, kanisa langu lina shughuli kwa ajili ya wanandoa. Tunakwenda kushiriki uzoefu kuhusu jinsi ya kuishi kwa furaha kila siku. Baada ya hapo, kutakuwa na dansi. Nikikualika, utakuja?”

“Bila shaka!” Ricardo alisema, lakini jibu lake halikunishawishi.



**N**ilitoa mialiko tisa kwa watu kazini na nilibakiwa na mmoja. Sikujua nani wa kumpa.

“Angalau nilifanya sehemu yangu,” niliwaza.

Mke wangu pamoja nami tuliwasili kwenye shughuli mapema ili kuwakaribisha watu wakati wakiingia. Ghafila, nilimwona Ricardo na mke wake, Regina. Niliwatambulisha kwa mke wangu na kwa wengine waliokuwa wakihudhuria. Jioni ile yote, Ricardo na Regina walionekana walikuwa wakifurahia. Nilishangazwa waliposema wangekuja kanisani jumapili kujifunza zaidi.

Ricardo, Regina, na watoto wao wawili walijifunza zaidi. Hatimaye,

walijiunga na Kanisa. Baadae, waliunganishwa hekaluni. Ricardo wakati fulani aliniambia kwamba yeye na mke wake walikuwa wakizungumza kuhusu talaka, lakini ndipo Bwana alimuongoza Ricardo ofisini kwangu.

Tangu wakati huo nilimwomba Mungu msamaha kwa kudhani kwamba Ricardo asingekubali mwaliko wangu. Nimejifunza kwamba ni muhimu kumualika kila mtu. Huwezi kujua nani atakubali. ■

**Martin Apolo Cordova, Paraná, Brazil**

# Biashara Inashamiri

Na Joshua J. Perkey  
Magazeti ya Kanisa

Shukrani kwa kile alichojifunza katika madarasa ya kujitegemea, wakati mlango mmoja ulipofunga kwa Teddy Reyes, mwingine punde ulifunguka.

**N**i saa 10:00 alfajiri huko Santo Domingo, Jamhuri ya Dominika, na Teddy Reyes tayari amekwisha amka na anafanya kazi. Ana mengi ya kufanya leo kuendeleza biashara yake inayoshamiri. Anaanza kukatakata nyanya na mikate. Kisha anatengeneza mchuzi wake maalumu.

Ifikapo saa 12:00 asubuhi, wafanyakazi wawili wanafika kumsaidia, na matayarisho yanashika kasi. Ifikapo saa 2:00 asubuhi, tayari wamekwisha tengeneza mikate 300, ikifungwa kila mmoja kwenye kifungashio cha plastiki na kupangwa kwenye mabegi. Wafanyakazi wengine sita hutokea, na kundi lote linatoka kwenda kuuza.

Ifikapo saa 3:00 asubuhi, mikate yote isipokuwa michache—mitatu au minne ambayo Teddy alitunza kuwalisha timu yake—imekwisha uzwa.

Biashara ni nzuri kwa Teddy. Lakini mambo daima yamekuwa si rahisi. Kwa kweli, kwa miaka mitano iliyopita, hakuweza kupata kazi imara katika taaluma yake aliyochagua—kama mwanasheria.



Hivyo ni kwa jinsi gani Teddy alifanya badiliko kutoka kwenye kushauri wateja kwenda kwenye kuuza mikate? Ilichukua juhudi kubwa, ndiyo, lakini pia ilichukua matumizi makini ya kanuni alizojifunza darasani zilizo-tolewa kupitia mafunzo ya Kanisa ya Huduma ya Kujitegemea.

### **Kupoteza Kazi Yake**

Miaka mitano iliyopita, maisha kwa Teddy yalionekana ya kupendeza. Alikuwa na kazi nzuri kama mwanasheria, alikuwa ameo karibuni, na alikuwa amembatiza mke wake. “Lakini tulipata baadhi ya changamoto,” alisema, “na nikapoteza kazi yangu.”

Kwa miaka minne iliyofuata Teddy alihangaika kutafuta kazi. “Kulikuwa na kazi nyingi ambazo ningeweza kufanya, lakini hakuna aliyetaka kunilipa. Niljiribu kuanzisha ajira tofauti tofauti mimi mwenyewe, lakini hilo halikufanikiwa.”

Mke wake, [Stephany], alikuwa na kazi nzuri, lakini mshahara wake pekee usingeweza kulipa gharama zote. Punde wanandoa walipata mtoto. Walifurahia, lakini kipato chao kilizidi kubana. Walipoteza nyumba yao, ilibidi wauze gari yao, na walitumia akiba yao yote. Hatimaye ilibidi wahamie kwenye nyumba ndogo iliyomilikiwa na mama ya [Stephany].

Lakini Teddy hakukata tamaa. Punde fursa isiyotarajiwa ilijitokeza.

### **Nguvu ya Kujitegemea**

Baada ya miaka ya mahangaiko, Teddy alijua ulikuwa ni muda wa mabadiliko.

“Niliamua kuchukua kozi ya Kanisa ya kujitegemea,” anasema. “Nilisikia kuhusu kozi hizo lakini mara zote

nilidhani hazikuwa kwa ajili yangu. Nilidhani zilikuwa tu kuhusu kufanya mambo peke yako. Madarasa yalikuwa ya kuvutia.”

Kwanza, Teddy alijiunga na kundi la Kusimamia Fedha Binafsi. Kisha akajiunga na kundi la Kuanzisha na Kukuza Biashara Yangu. Makundi ya madarasa yalimsaidia Teddy kwenye uelewa wa biashara yake lakini pia yalimsaidia kujijenga kiroho.

“Kuchukua madarasa haya kulibadili kila kitu,” anasema. “Niliamua kufanya kila kitu walichofundisha. Na kipato changu kilibadilika mara moja. Nilianza kulipa zaka kamili, kusali kila siku, kusoma maandiko, na kuonyesha imani. Na mambo yalibadilika—nilianza kuweka akiba ya pesa na kuitakasa sabato. Kila kanuni ilinibariki.”

Katika kundi hili la Kuanzisha na Kukuza Biashara Yangu, Teddy alijifunza jinsi ya kuainisha bidhaa zenye kuwezekana ambazo zingeweza kuwanufaisha wateja pale wanapoishi. Alipotathmini kile ambacho watu walikuwa wakihitaji, mwongozo ulianza kutiririka. Katika eneo lake, watu walipenda mikate iliyotengenezwa siku hiyo hiyo, lakini pia walipenda kuipata kwa kuagiza—na kupelekewa.

“Hoteli nyingi zina mchuzi maalumu ambao hufanya chakula chao kupendwa,” Teddy anasema. “Hivyo nilitengeneza mchuzi wangu mwenyewe maalumu kwa ajili ya mikate!”

### **Kukuza Biashara Yake**

Siku alipofungua biashara yake, Teddy alitengeneza mikate 30.

“Dakika thelathini baadaye, nilikuwa nimekwisha rudi nyumbani,” anasema.

“Mke wangu alisikitika aliponikuta kwenye kochi. Aliniuliza nilikuwa nafanya nini nyumbani muda ule—sikupaswa kuwa nauza mikate? Nilikuwa tayari nimeuza yote!”

Wiki chache baadaye, Teddy aliwasiliana na shule na wafanya biashara wa eneo lake. Wengi walitamani kununua mikate yake, na biashara yake ikaanza kukua. Alijifunza haraka jinsi ya kutunza mboga mbichi ili zikae kwa muda mrefu. Anajua pia muda kamili wa mchuzi wake maalumu kutumika. Anaagiza na kuchukua mikate kila asubuhi. Ananunua mboga zenye punguzo la bei Jumamosi, ambazo zina gharama ndogo lakini bado zitakuwa nzuri Jumatatu.

Punde alikuwa akipokea mahitaji kwa ajili ya aina maalumu za mikate, na hata idadi kubwa kwa ajili ya matukio maalumu. Alihitaji msaada na alianza kuajiri watu.

Kwa kutengeneza mahusiano chanya na shule na wafanya biashara wa eneo lake, Teddy alianzisha uteja hai, na wenye muendelezo. Ndani ya miezi minne, alikuwa na wafanyakazi nane na alikuwa akiuza mikate 300 kwa siku, siku tano kwa wiki. Timu yake ya mauzo ilikuwa na ufanisi kiasi kwamba waliuza kila mkate hata wakati wa majira ya jua ambapo shule zilikuwa zimefungwa. Sasa Teddy yuko tayari kupanuka tena.

Kwa sababu alihudhuria madarasa ya kujitegemea, alipata mwongozo wa kuja na wazo la biashara ya mikate. “Kwa sababu ya mwongozo huu kutoka Kanisani na baraka nilizopokea,” anasema, “nina ushuhuda imara wa Kanisa la Yesu Kristo.” ■



## Mwana Wetu ni Mwana wa Baba wa Mbinguni

Jerlyn Murphy

**M**wana wetu mpendwa mdogo, Hayden, alikuja kwenye ulimwengu huu akiwa wa bluu, hapumui, na akihangaika kwa ajili ya maisha. Hali. Hajonge.

Wakati madaktari na wauguzi walipoharakisha kuingia chumbani hospitalini, nilijua kuna kitu hakikuwa sawa kabisa. Mume wangu na baba yangu haraka walimpa Hayden baraka ya ukuhani, na Hayden alikimbizwa kwenye chumba cha wagonjwa mahututi. Punde aligundulika kuwa na tati-zo lisilo la kawaida la moyo kutofanya kazi ipasavyo. Ndani ya siku chache alipitia upasuaji kadhaa wa moyo.

Kupitia nguvu ya muujiza ya baraka ya ukuhani, kufunga, na sala, Hayden alishinda yote na alinusurika. Tulikuwa na shangwe isiyo kifani kumleta mwana wetu nyumbani na kuanza maisha yetu mapya pamoja.

Hayden alileta shangwe isiyopimika kwenye maisha yetu. Tulimthamini na kumpenda mno. Lakini kadiri muda ulivyopita, nilianza kuwa na wasi-wasi kwamba alikuwa haonyeshi maendeleo kama ilivyotarajiwa. Japokuwa wataalamu walituhakikishia kwamba hatimaye angekuwa sawa, wasiwasi wa kusumbua uliendelea pale nilipohangaika kumsaidia mwanangu.

Mimi na mume wangu tulijifunza yote tuliyoeweza kuhusu ugonjwa wa Hayden. Tulifanya kila kitu tulichoagizwa na madaktari kufanya. Bado maendeleo hayakuja.



Nilichoka na kukata tamaa. Nilimsihi Baba wa Mbinguni kunisaidia kumpata mtu ambaye angeweza kumsaidia Hayden, lakini usaidizi haukuja. Hali ya Hayden ilizidi kuwa mbaya. Alianza kupata kifafa. Tulipata hofu. Tulidhani tulikuwa tunampoteza.

Usiku mmoja, nilichelewa kulala nikitafuta majibu. Nilimwandikia Hayden barua. Nilimwambia jinsi gani ninampenda na kwa kiasi gani nilikuwa nikijaribu kufanya maisha yake yawe rahisi. Niliahidi ningetumia siku zote zilizobaki za maisha yangu nikijaribu kumpatia msaada aliohitaji.

Kukata tamaa na kutokuwa na uhakika kwa muda vilinizidia. Nilipiga magoti na kumuuliza Baba yangu wa Mbinguni, “Kwa Nini?” Nilidhani alimtuma Hayden kwangu kwa sababu alijua sitakata tamaa kujaribu kumsaidia mwanangu. Hivyo kwa nini sikupata jibu lolote? Kwa nini kila daktari mpya na kila tiba mpya ilipelekea kikwazo kingine? Je, Baba wa Mbinguni alimpenda Hayden?

Sitasahau kamwe wakati ule. Hisia nyingi za upendo ghafla zilinifunika. Maneno ambayo hayakuwa ya kwangu yaliingia akilini mwangu: “Jerlyn, unadhani unampenda kuliko Ninavyompenda?”

Niliganda. Wakati uliganda. Machozi yalititirika usoni mwangu—siyo kwa kukata tamaa kama mwanzo, bali kwa tumaini, uelewa, na upendo.

Katika dakika ile moja, kila kitu kilibadilika. Moyo wangu ulilainika. Maswali yangu

yalibadilika. Ninajua sasa kwamba Baba yangu wa Mbinguni anampenda Hayden kwa upendo mkamilifu. Hayden aliletwa hapa katika mwili ambao ulikidhi mahitaji yake na fursa zake kwa ajili ya ukuaji na kujifunza. Ana seti yake ya kipekee ya uwezo na changamoto kama vile kila mmoja wetu. Nimekuja kujua kwamba watoto wenye ulemavu ni wa thamani na watoto wape ndwa wa Baba wa Mbinguni ambao wana kazi maalumu hapa katika dunia hii.

Mume wangu na mimi kwa uaminifu tuna-pokea majibu na baraka, lakini yanakuja katika wakati wa Bwana, siyo wakati wetu. Tumeongozwa kwenye

vitabu sahihi, tiba sahihi, shule sahihi, na waalimu sahihi kumsaidia Hayden kufanikiwa katika maisha

yake ya duniani. Tunajitahidi kutafuta njia ambayo Baba yetu wa Mbinguni ameitoa kwa Hayden badala ya njia tuliyotaka yeye apite. Tunafanya kila tunachoweza kumsaidia Hayden kufikia uwezekano wake mtakatifu na kuishi maisha ambayo Baba yake wa Mbinguni amemtengenezea. Uelewa wa mpango wa Baba wa Mbinguni umekuwa wazi zaidi sasa kiasi kwamba tunaielewa kuwa Hayden alikuwa Wake kabla Hayden hajawa wetu. ■

*Mwandishi anaishi Arizona, Marekani.*

---

Maneno ambayo hayakuwa ya kwangu yaliingia akilini mwangu: “Unadhani unampenda kuliko ninavyompenda?”



#### KIINI: ZAWADI YA BURE

“Kwa sababu ambazo kwa kawaida hazijulikani, baadhi ya watu huzaliwa na mapungufu ya kimwili. Sehemu maalumu za mwili zinaweza kuwa haziko

kawaida. Mfumo wa urekeshaji unaweza kuwa hauko sawasawa. Na miili yetu yote inapatwa na ugonjwa na kifo. Hata hivyo, zawadi ya mwili ni bure. Bila mwili, hatuwezi kupata utimilifu wa shangwe.

“Mwili mkamilifu hauhitajiki ili kupata takdiri takatifu. Kwa kweli, baadhi ya roho nzuri zimepewa hifadhi ndani ya miili dhaifu. Nguvu kubwa ya kiroho mara nyingi hujengwa na wale wenye changamoto za kimwili kwa usahihi kwa sababu wanapata changamoto. Watu kama hao wanapewa haki kwenye baraka zote Mungu alizonazo kwa ajili ya watoto Wake waaminifu na watiifu.”

Rais Russell M. Nelson, “Sisi Ni Watoto wa Mungu,” *Ensign*, Nov. 1998, 86–87.

# Kuvumilia Janga

**H**ivi karibuni au baadae, watoto watakabiliwa na janga, iwe ni karibu na nyumbani au mbali. Lakini “hata wakati dunia inapokuwa kwenye ghasia kote kutuzunguka, tunaweza kupokea baraka ya amani ya ndani.”<sup>1</sup> Hapa ni baadhi ya mambo unayoweza kufanya kuwasaidia watoto kuhisi amani hiyo.



## Uthabiti

Wakati janga linapotokea, watoto wanaweza kuhisi kama ulimwengu wao hauko sawa. Kuwa mfano wa uthabiti kwao. Zungumza kwa utulivu na kwa ujasiri kuhusu tukio. Endeleza utaratibu kadiri uwezavyo. Fanya kila uwezalo kuendeleza jioni ya familia nyumbani, kusoma maandiko, sala, na tabia zingine za familia. Kadiri ya muda unavyokwenda watoto wanaweza kujifunza kwamba hata wakati ulimwengu wao unatikisika, injili huleta mtazamo na maisha yanaendelea.

## Heshima

Onyesha heshima katika hisia za watoto. Wasikilize watoto na tambua jinsi wanavyohisi. Waonyeshe kwamba unachukulia mambo yao kwa umakini. Wape faragha ikiwa wanaihitaji lakini waache wajue unapatikana wakiwa tayari kuzungumza. Kwa uaminifu jibu maswali pale yana-poibuka kwa kuzingatia umri walionao. Acha watoto wako wajue kwamba wanaweza siku zote kuzungumza nawe kuhusu woga na wasiwasi wao.



## Mwongozo

Watoto wako wanaweza kuuliza, “Kwa nini Mungu huacha mambo mabaya yatokee?” Elezea kwamba nyakati nzuri na mbaya ni sehemu ya maisha na sehemu ya mpango wa milele wa Mungu. Anamruhusu kila mtu kufanya chaguzi zake mwenyewe, na wakati mwingine watu hufanya chaguzi mbaya ambazo husababisha maumivu. Nyakati zingine, majanga si kosa la mtu bali ni sehemu ya uhalisia. Bila kujali chochote, Baba wa Mbinguni yuko pale kwa ajili yetu. Kwa msaada wake, tunaweza kujifunza na kukua, hata kutokana na uzoe-fu wenye maumivu. Tunaweza kumgeukia Yeye ili kupata amani.

## Uwezeshaji

Waonyeshe watoto kwamba wana nguvu ya kuleta utofauti kwa kuwapa njia ya kusaidia. Kwa mfano, wangeweza kusa- idia kukusanya michango kwa ajili ya waathiriwa wa majanga, kumtembelea rafiki mgonjwa au aliyeumia hospitalini, kumpa furaha mtu anayekabiliwa na kupoteza familia, au kuwaombea wale wanaohangaika. Hatuwezi kurekebisha kila kitu, lakini tuna uwezo wa kufanya mengi mazuri, na “tunafanyia kazi amani pale tunaposaidia kutuliza mate- so ya mwingine.”<sup>2</sup>



## Faraja

Wakumbushe watoto wako kwamba Mungu anawapenda na kwamba wewe unawape- nda. Usitoe ahadi za uwongo kwamba hakuna kitu kibaya kitakachotokea kwao, bali waha- kikishie kwamba wako salama sasa na kwamba utafanya yote uwezayo kuwalinda. Wahakiki- shie kwamba Baba wa Mbinguni atawasaidia kupitia jaribu lolote linalokuja kwenye njia yao.

Unapojikuta umevunjwa moyo kwa jaribu, kumbuka kwamba mwishoni, mema yata- shinda maovu. “Tunapigana vita dhidi ya dhambi, . . . lakini hatupaswi kukata tamaa,” alifu- ndisha Rais Thomas S. Monson (1927–2018). “Ni vita ambayo tunaweza kushinda na tutashi- nda. Baba yetu wa Mbinguni ametupa vifaa tunavyohitaji ili kufanya hivyo. Yeye ndiye aliye katika usukani. Hatuna chochote cha kuogopa.”<sup>3</sup> ■

## MUHTASARI

1. “Amani,” Mada za Injili, topics.lds.org.
2. “Amani,” Mada za Injili.
3. Thomas S. Monson, “Kuangalia nyuma na Kusonga Mbele,” *Liahona*, May 2008, 90.

## KWA WATOTO

Ndani ya *Rafiki* ya mwezi huu:

- “Nitamwona Yeye tena” (ukurasa R20)
- “Kadi za Faraja” (ukurasa R21)

Kwa nyenzo zingine, tembelea [lessonhelps.lds.org](http://lessonhelps.lds.org) na bofya “Msaada wa Masomo kwa Mada.”



## KWA AJILI YA VIJANA WALIOBALEHE

Katika toleo hili

- “Kutafuta Amani kwa Ajili Yako na Wengine katika Nya- kati za Matatizo” (ukurasa wa 52–53).

Kwa nyenzo zingine, tembelea [youth.lds.org](http://youth.lds.org).



## Je, Mungu Ananiongoza?

**M**aisha yetu yamejawa na chaguzi kubwa: kazi ipi ya kufanya, nani wa kufunga naye ndoa, wapi pa kwenda kusoma, n.k. Maisha yetu pia yamejawa na wasiwasi: kuchagua matumizi bora ya muda, kujari-bu kuelewa injili, na kutafuta amani katikati ya majaribu. Yote kwa yote, **tunahitaji ufunuo binafsi**. Lakini wakati mwingine yaweza kuwa vigumu kujua jinsi ya kuupokea na jinsi ya kuutambua pale tunapoupokea. Wakati hatupati au kutambua majibu, tunaweza kujiuliza, “Je, yule alikuwa Roho au mawazo yangu tu?” “Kwa nini nilihisi mwongozo wa kufanya kile na kisha nikashindwa?” “Kwa nini ninahisi kama vile Mungu hajibu sala zangu?”

Kwa bahati nzuri, katika “kufanya Maamuzi: Haki ya Kujiamulia dhidi ya Ufunuo” (ukurasa wa 44), Erin anashiriki hadithi yake kuhusu ufunuo binafsi wakati alipotakiwa kufanya uamuzi wenye kubadilisha maisha. Wakati **Mungu anataka kutuongoza**, Yeye anataka pia kutusaidia kujifunza kutegemea haki yetu ya kujiamulia kufanya chaguzi nzuri.

Kujifunza jinsi Roho Mtakatifu anavyozungumza na wewe binafsi ni sehemu nyingine ya muhimu ya kupokea na kutambua ufunuo. Inaweza kuwa vigumu kwa kila mmoja wetu. Katika ukurasa wa 48, vijana waku-bwa **wengi wanashiriki jinsi wanavyopokea ufunuo**.

Katika makala ya kidijitali pekee, Aspen anaelezea kwamba ufunuo binafsi huitaji “Kufanyia Mazoezi Misuli Yako ya Kiroho.”

Kufikiria kuhusu wakati ujao kunaweza kuwa kwa kuchosha, hata kuogopesha. Hasa kama kijana mku-bwa. Lakini ninapokumbuka jinsi **Mungu alivyoyangoza maisha yangu** katika siku za nyuma, inanipa ujasiri wa kusonga mbele na kutenda, nikiamini kwamba **Yeye ataendelea kunipa mwongozo ninaohitaji** nikiwa njiani.

Kwa moyo wa dhati,

Katie Sue Embley

*Katie Sue*



## USHAURI BORA . . .

*Vijana wakubwa wanashiriki ushauri bora waliowahi kupata kuhusu kupokea ufunuo binafsi:*

"Mshauri wangu wa Mahususi Kwa Vijana aliwahi kuniambia, 'Jenga uhusiano wako na Mungu kama Baba yako halisi wa kiroho. Kadiri ulivyo imara uhusiano wako na Yeye, ndivyo zaidi utaelewa na kuongozwa.' Hilo limeleta tofauti kubwa katika sala zangu."

—**Grant Goolsby, California, Marekani**

"Patriaki wa kigingi chetu amefanya kila mtu akariri kishazi kimoja: 'Ili kupokea ufunuo, soma ufunuo.' Imenisaidia sana niliposoma maandiko."

—**Shellby Tippets, Missouri, Marekani**

"Chukua muda kutafakari. Joseph Smith alitafakari Yakobo 1:5 kabla hajaamua kutenda. Wakati mwingine Baba wa Mbinguni anatutaka sisi kuwekeza katika sala na kusoma kabla Yeye haja-tupatia majibu. Tunajifunza zaidi kwa njia hiyo."

—**Natasha Herbst, Utah, Marekani**

"Sikiliza kwa moyo wako, siyo masikio yako."

—**Sai Tua, American Samoa**

*Ni ushauri upi bora umewahi kupokea kuhusu toba? Tutumie jibu lako kwenye [liahona.lds.org](http://liahona.lds.org) kabla ya Aprili 30, 2019.*

## KUHUSU MWANDISHI KIJANA MKUBWA

**Erin Rider** ni wakili na mtengenezaji msaidizi wa podcast. Amekimbia nusu yake ya kwanza ya mbio za masafa marefu. Akiwa hana kazi hufurahia kusoma, matembezi marefu, na kutumia muda pamoja na familia na marafiki.



**Aspen Stander** ni mwandishi na mhariri kutoka Utah, Marekani. Anapenda matembezi marefu, kusafiri, kusoma, na kupiga piano.



**Katie Sue Embley** anadhani ulimwengu umejaa watu wazuri ambao hadithi zao zinapaswa kusikika. Anasoma uandishi wa habari na Kihispania, kwa lengo la #shiriki wema.



## KATIKA SEHEMU HII

**44** Kufanya Maamuzi: Haki ya Kujiamulia dhidi ya Ufunuo Na Erin Rider

**48** Ufunuo Binafsi



Tafuta makala hizi na nyingine zaidi:

- Kwenye [liahona.lds.org](http://liahona.lds.org)
- Katika **Vijana Wakubwa kila wiki** (kwenye "Vijana Wakubwa" katika Maktaba ya Injili)
- Kwenye [facebook.com/liahona](https://www.facebook.com/liahona)

## SHIRIKI HADITHI YAKO

Je, una hadithi ya kupendeza ya kushiriki? Au je, unataka kuona makala kuhusu mada fulani? Kama ndivyo, tunataka kusikia kutoka kwako! Unaweza kuwasilisha makala yako au jibu lako kwenye [liahona.lds.org](http://liahona.lds.org).

## KIDIJITALI PEKEE

Kufanya Mazoezi Misuli Yako ya Kiroho Na Aspen Stander



# Kufanya Maamuzi: Haki ya Kujiamulia dhidi ya Ufunuo

Linapokuja  
suala la maamuzi  
makubwa, ni  
kwa kiasi gani  
tunahitaji  
kumtegemea  
Mungu kutuambia  
nini cha kufanya?

Na Erin rider

**K**ila siku kila mmoja wetu hukutana na maamuzi mengi. Baadhi ni ya kidunia, kama, “Ni nini napaswa kuvaa?” “Nini napaswa kula kwa ajili ya chakula cha mchana?” “Je, ni muda wa kununua gari mpya, au naweza kubaki na ya zamani kwa muda mrefu kidogo?” Lakini mara nyingi kila mara tunakutana na uamuzi mkubwa—“Je, ninapaswa kurudi shule?” “Je ninapaswa kuikubali kazi hii?” “Je, ninapaswa kuhamia katika jiji jipya?” “Je ninapaswa kununua nyumba?” “Je ninapaswa kwenda miadi na mtu huyu?” “Je ninapaswa kufunga ndoa na mtu huyu?” na kadhalika.

Tunapokabiliwa na maamuzi makubwa, tunajaribu—kwa usahihi—kuchukua muda mrefu kufanya uchaguzi. Tunafuata ushauri uliotolewa kwa Oliver Cowdery katika Mafundisho na Maagano 9:8–9, ambapo Bwana anasema:

“Lakini, tazama, ninakuambia, kwamba unalazimika kulichunguza katika akili yako; ndipo uniulize kama ni sahihi, na kama ni sahihi nitaufanya moyo wako

uwake ndani yako; kwa njia hiyo, utahisi kuwa hiyo ni sahihi.

“Lakini kama siyo sahihi hutapata hisia za namna hiyo, bali mzubao wa mawazo ambayo yatakufanya usahau kitu kile kisicho sahihi.”

Japokuwa huu hakika ni ushauri mzuri, linapokuja suala la maamuzi makubwa, wakati mwingine tunategemea kwa kiasi kidogo sana sehemu ambayo Mungu hutuambia kile kilicho sahihi na si vya kutosha kwenye sehemu ambapo Yeye hutuambia kulichunguza katika akili zetu. Tunakwama tukisubiri Mungu kuthibitisha maamuzi yetu kiasi kwamba tunaacha fursa nzuri zitupite. Tunaweza hata kutambua kazi ya haki ya kujiamulia, lakini tunaogopa kufanya uamuzi ambao unaweza kututoa kwenye njia kutoka kwenye “mpango” wetu uliobainishwa kabla na kuishia kukisia kwamba chochote zaidi ya mwako wa moyo au sauti kutoka mbinguni humaanisha kwamba uchaguzi wetu ni mbaya. Kwa wengi wetu, mvuto huu usioelezeka



kati ya haki ya kujiamulia na ufunuo binafsi huongoza kwenye swali moja la muhimu: Ni nini wajibu wa Mungu katika kutusaidia kufanya maamuzi?

### **Wajibu wa Mungu katika Kufanya Uamuzi**

Pengine swali hili linaweza kujibiwa vizuri kupitia hadithi ya kaka wa Yaredi. Kuna mpangilio wa kuvutia wa ukuaji katika hadithi hii ambao unatufundisha kuhusu jinsi Mungu anavyotarajia tufanye maamuzi. Baada ya lugha kuchanganywa kwenye Mnara wa Babeli, Yaredi anamuomba kaka yake kumuuliza Bwana ikiwa walipaswa kuondoka, na kama ndivyo, wapi walipaswa kwenda (ona Ether 1:36–43). Kaka ya Yaredi anauliza, na Bwana anawaongoza kwenye ufuko wa bahari. Wanaposafiri, Bwana anazungumza nao katika wingu na kuongoza kila hatua ya safari yao. Hatimaye wanafika ufukoni mwa bahari, ambapo wanakaa kwa miaka minne.

Mwishoni mwa miaka minne, Mungu anamwambia kaka wa Yaredi kujenga mashua na kuwa tayari kuvuka bahari. Wakati kaka wa Yaredi anagundua merikebu hazikuwa na hewa, anafuata mpangilio uleule wa kwenda kwa Mungu kumuuliza kile anachopaswa kufanya. Kama ilivyotarajiwa, Bwana alijibu kwa kumpa maelekezo ya kina kutengeza matundu upande wa juu na chini wa merikebu. Gundua mpangilio wa ufunuo mpaka sasa: Mungu anawapa mpango, wanauliza maswali kuhusu jinsi ya kutimiza mpango, na Mungu anajibu kwa majibu ya kina na ya uhakika.

Baada ya kutengeneza matundu kwenye merikebu, kaka wa Yaredi anagundua kwamba merikebu hazitakuwa

na mwanga. Kwa mara nyingine tena anamuuliza Mungu ni nini angepaswa kufanya. Badala ya kujibu, hata hivyo, Mungu anauliza—“Ungetaka nifanye nini ili muwe na mwangaza kwenye mashua yenu?” (Etheri 2:23). Badala ya kutoa maelekezo ya kina kama Ali-vyofanya kabla, wakati huu Bwana anamsubiri kaka wa Yaredi kuamua nini cha kufanya.

Aina hii ya jibu kutoka kwa Bwana pengine ni gumu kulielewa wakati wa kujaribu kufanya uamuzi. Tunafundishwa kuomba na kusubiri jibu, hivyo kiuhalisia tuna wasiwasi tunapokosa jibu. Mara nyingi tunajiuliza ikiwa ukosefu wa jibu la wazi unakidhi kuwa “mzu-bao wa mawazo” ukionyesha kwamba uchaguzi wetu ni mbaya. Wakati mwingine tunajiuliza ikiwa inamaanisha hatuko waadilifu vya kutosha kusikia jibu au ikiwa hatuombi kwa “kusudi halisi” (ona Moroni 10:4). Lakini kuna njia ya tatu ambayo wakati mwingine

hatuifikirii—pengine, kama vile kwa kaka wa Yaredi, Mungu anasubiri *sisi* tufanye uamuzi *wetu wenyewe*

### **Kufanya Uamuzi**

Hivi karibuni nilikutana na hali ambayo ilitoa changamoto kwa jinsi nilivyofikiria kuhusu haki ya kujiamulia na ufunuo binafsi. Nilipokuwa nakaribia mwisho wa kuhitimu, nilipata nafasi tofauti za kazi katika majiji tofauti na nisingeweza kuamua ipi ya kuchukua. Kama kaka wa Yaredi, nilikuwa nimepitia uzoefu wa nyakati nyingi ambapo nilikuwa nimesali kuhusu uamuzi mkubwa na Mungu alijibu kwa jibu lenye uhakika. Kwa kutegemea uzoefu huo wa mwanzo, nilianza kumuomba Mungu anisaidie kuamua ni kazi gani ningechagua. Nilikuwa pia nikifanya sehemu yangu kwa kujifunza kuhusu kila nafasi ya kazi na kushauriana na watu wengi. Lakini bila kujali ni kwa kiasi gani niliomba, mbingu zilika kimya, na sikupokea jibu.

Tarehe ya mwisho ya kufanya maamuzi ilikaribia, na nilianza kupata wasiwasi. Hakika huu ulikuwa ni uamuzi Bwana alipaswa kuujali, hivyo kwa nini Hakuajibu? Pengine hakujali kuhusu kazi ipi nilichagua, lakini lazima ajali kuhusu ni jiji lipi nilihamia kwani ingekuwa na matokeo kwenye maisha yangu. Bwana daima alikuwa akijali kuhusu maamuzi yangu huko nyuma, hivyo kwa nini Asingejali kuhusu huu pia?

Hata hivyo bila kujali nilijaribu kwa kiasi gani, hakuna jibu lililokuja. Niliianza kujiuliza ikiwa nilikuwa nimesonga mbali kutoka kwa Mungu kiasi kwamba sikuweza kusikia jibu Lake. Nilijiuliza pia ikiwa nisingeweza kusikia kwa sababu bila kufahamu *sikutaka* kusikia jibu. Hatimaye, siku moja kabla ya tarehe ya mwisho, nilijua nilipaswa kufanya uamuzi, hivyo nilitumia busara yangu na kufanya uamuzi. Usiku ule niliomba, nikiuliza ikiwa Yeye angeniambia kama jibu langu halikuwa sahihi. Bado jibu halikuja, hivyo niliamua kuikubali kazi.





Miezi kadhaa baadaye, nilikuwa bado na mashaka na uamuzi wangu, hivyo niliomba baraka ya ukuhani ili kuwa na uha-kika. Katika baraka niliambiwa kwamba sikupata jibu la ombi langu kwa sababu Bwana alikuwa na furaha kwa uamuzi wowote ambao ningefanya. Baraka hii iliimarisha ushauri niliopewa kabla na rais wangu wa misheni, ambaye aliniambia kwamba mara nyingi haijalishi ni uamuzi gani tunafanya. Mungu anatutaka tujifunze jinsi ya kusimama kwa miguu yetu miwili na kuamua jinsi ya kuishi maisha yetu. Rais wangu wa misheni pia alinikumbusha kwamba Mungu, kama Baba yetu wa Mbinguni, hatatuadhibu na kutuondolea fursa zilizoahidiwa ikiwa kwa dhati tunajaribu kuamua nini cha kufanya.

Kaka wa Yaredi vilevile angeweza kupe-ndekeza karibia suluhisho lolote kupata mwanga kwenye mashua, na Bwana ange-likubali. Kiwango cha uzoefu kilikuwa siyo tu kwa kaka wa Yaredi kuimarisha imani yake bali pia kujifunza kufanya uamuzi.

## Kutumia Haki ya Kujiamulia

Kutoka kwenye mtazamo wa milele, kutumia haki ya kujiamulia ni sehemu muhimu ya ukuaji binafsi. Bila kuwa nayo, hatuwezi kufanya aina ya maamuzi ambayo yatatusaidia kufikia uwezekano wetu mkamilifu. Ukuaji, sawa na kila kitu katika injili, huja mstari juu ya mstari, kanuni juu ya kanuni” (2 Nefi 28:30). Mungu anatutaka tuwe watu waliojiandaa, siyo watu waliopooza, na Yeye anatarajia sisi kutumia haki yetu ya kujiamulia kuishi maisha yetu vizuri kadiri tuwezavyo.

Tukiweza kujifunza kutafuta usawa kati ya haki ya kujiamulia na ufunuo, tunaweza kupata ukuaji kweli kiroho. Hiki ndicho kilichotokea kwa kaka wa Yaredi. Baada ya kutafakari, alifanya kazi kuyeyusha mawe 16 kutoka kwenye mwamba na kumuomba Mungu kuyagusa na kuyafanya yatoe mwanga (ona Etheri 3:1–5). Wakati huu, wakati Mungu alipojibu, kila kitu kilibadilika. Badala ya kusikia sauti ya Bwana mawinguni, kaka wa Yaredi hasa *alimwona* Bwana, ambaye

siyo tu alitokea Yeye mwenyewe lakini pia alimwonyesha kaka wa Yaredi maono ya kustaajibisha ya ulimwengu na kila kitu ambacho kingekuja (ona Etheri 3:6–26). Inawezekana kwamba kaka wa Yaredi asingekuwa ameandaliwa kiroho kupokea ono lile kama kwanza asingepata uzoefu wa ukuaji binafsi ambao ulikuja kutokana na kufanya uamuzi wake mwenyewe.

Tunapofanya maamuzi, tunapaswa kwa hakika kufuata ushauri wa Alma wa “kushauriana na Bwana kwenye mate-ndo [yetu] yote” (Alma 37:37). Wakati Bwana anatumia tufanye uamuzi fulani, Yeye atatumia kusaidia kutuzuia kutokwenda mrama. Lakini pia lazima tujandae kusimama na kusonga mbele kwa imani, bila kujali jibu linakuja au la. Ili mradi tunatunza maagano yetu na kubaki waaminifu kwenye injili ya Yesu Kristo, tunaweza kuhisi ujasiri katika maamuzi yetu ya haki na amani kwamba Bwana ameridhishwa na juhudi zetu. ■  
**Mwandishi anaishi Utah, Marekani.**



Ni kwa jinsi gani unaweza kuo-nyesha tofauti kati ya ufunuo na mawazo yako mwenyewe?



# UFUNUO BINAFSI

## Mahususi

**T**unaishi katika ulimwengu wenye fursa nyingi. Tuna uhuru wa kuchagua kazi zetu wenyewe, shule, mwenza, wapi tunataka kuishi, na mengine mengi zaidi. Kweli ni baraka kubwa katika kizazi chetu. Lakini kwa upande mwingine, inafanya chaguzi hizi zote kuwa ngumu zaidi kwa sababu ni vigumu kufanya maamuzi wakati kukiwa na njia na fursa nyingi ambazo zitaongoza kwenye mambo mazuri. Tunawezaje kuchagua mema wakati kuna fursa nyingi ambazo ni njema? Unapohisi kupotea na kuchanganyikiwa katika dhoruba hii ya maamuzi, jua kwamba Baba wa Mbinguni anataka kukuongoza. Unaweza kuchagua njia sahihi na kupata majibu unayotafuta ikiwa utafuata sauti Yake. Tambua jinsi anavyozungumza na wewe, muamini Yeye, mfuata nabii, kuwa mvumilivu, kuwa mwenye msimamo wa kutegemea mazuri, na kuwa na imani, na hatimaye utao-ngozwa katika uelekeo sahihi.

—Vira Vashchenko, *Kyiv, Ukraine*

**K**ote katika maisha yangu nimeona jinsi Bwana alivyoniongoza, na kutambua kwamba mafanikio yangu yote ni shukrani Kwake na kwa mwongozo Wake. Hata katika nyakati ninapofikiri ninatembea peke yangu, mwishoni, huniacha nijue na kuhisi kwamba Yeye daima amekuwepo pale pamoja nami. Hiyo ndiyo maana nimefanya maamuzi ya kusonga mbele daima kwa imani, hata wakati ninapohisi kwamba niko peke yangu. Kwangu mimi, njia yangu haiko wazi wakati mwingine, na siwezi daima kuona kile kinachonisubiri huko baadaye, lakini daima ninachukua hatua za imani, na kisha ninaanza kuona nuru na kutambua mkono wa Mungu katika maisha yangu. Najua kwamba Baba yetu wa Mbinguni na Mwanawe, Yesu Kristo, wanatupenda na Wapo tayari kutuongoza, lakini Wao pia wanategemea sisi tuweke imani Kwao na kutenda pale tunapopokea msukumo wa kiungu kutoka kwa Roho.

—Indhira Mejia, *Jamhuri ya Dominika*



**N**adhani kwamba moja kati ya mbinu za kuvutia tunazopaswa kuwa na ujuzi nazo ni uwezo wa kutambua minong'ono laini ya Roho Mtakatifu. Kusoma maandiko kwa bidii kumeni-sukuma kuongeza ujuzi huo. Mara zote nimekuwa nikiamini kwamba yeye atafutaye kwa bidii atapata; na atafunuliwa siri za Mungu, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu (ona 1 Nefi 10:19). Kwa maneno mengine, ikiwa ninataka kumtambua Roho, siwezi kujiacha niongozwe kwenye mawazo yasiyofaa au shughuli za kila siku za maisha, lakini badala yake ninapaswa kuzama kwenye kazi ya kujisahau. Hapo ndipo nitakuwa mzuri zaidi kuweza kumtambua Roho kwa sababu niko tayari kwa ajili ya hilo! Kama vile ambayo meli haiwezi kwa urahisi kusafiri katikati ya tufani, hatuwezi kumsikia Roho kama tumechukuliwa mbali na shughuli za maisha ambazo ziko nje ya uwezo wetu.

—*Emmanuel Borngreat Dogbey, Accra, Ghana*

**P**ale ninapozidi kukua, imenibidi nijifunze lugha ya Roho. Roho huzungumza nami kupitia mawazo rahisi. Imechukua mazoezi kadhaa kuzoea hilo, lakini mara nyingi Roho huja kwangu katika mahali patulivu, kama vile nikiwa ndani ya gari yangu kuelekea kazini. Najua si mawazo yangu kwa sababu Roho mara nyingi atajipenyeza wakati ambapo sifikirii hata mada ile.

—*Clarissa Mae Taylor, Utah, Marekani*

**K**atika familia yetu ndogo, tunamtambua Roho kwa sababu ya amani tunayohisi, hasa mimi na mume wangu pamoja kama wanandoa. Kama ni mawazo yetu wenyewe, hatuhisi kamwe kwamba ni kitu sahihi hasa—daima kunakuwepo na shaka au hofu. Lakini kama ni ufunuo, daima tunahisi amani, hata kama tunajaribu kujipa moyo na mambo hayaonekani kuleta maana mwanzoni. Tunapoufuata na kuufanyia kazi, daima tunaona mambo yakiwa sawa na kila kitu kinatendeka ilivyopaswa. Hapo ndipo tunapotazamana na kusema, “Ee sasa inaleta maana!”

—*Maryana Wright, Utah, Marekani*



Japokuwa sote tunaweza kupokea ufunuo binafsi kwa njia tofauti, kitu kimoja hakika ni cha kweli: Mungu huzungumza nasi mara kwa mara. Tunapaswa tu kuwa tayari kuweka juhudi ili kuongeza uwezo wetu wa kutambua na kusikia sauti Yake. Kama Rais Russell M. Nelson alivyoshauri: “Omba katika jina la Yesu Kristo kuhusu matatizo yako, hofu zako, udhaifu wako—ndio, mahitaji ya moyo wako. Na kisha sikiliza! Andika mawazo ambayo yana-kuja kwenye akili yako. Andika hisia zako na zifuatilie kwa vitendo ambavyo unashawishiwa kufanya. Unaporudia mchakato huu siku baada ya siku, mwezi baada ya mwezi, mwaka baada ya mwaka, “utakua katika kanuni ya ufunuo.” (Ufunuo kwa ajili ya Kanisa, Ufunuo kwa ajili ya Maisha Yetu,” *Liahona*, Mei 2018, 95). ■



## KATIKA SEHEMU HII



- 52 **Kutafuta Amani kwa Ajili Yako na Wengine katika Nyakati za Matatizo**  
Na Alex Hugie pamoja na Aspen Stander
- 54 **Maisha ni Mbio ya masafa marefu**  
Na Sally Johnson Odekirk
- 60 **Maswali na Majibu: Ni kwa jinsi gani baraka zangu za kipatriaki zinaweza kunisaidia kufanya maamuzi?**
- 62 **Jaribu Baadhi ya Tamaduni Mpya za Pasaka**  
Na David Dickson
- 64 **Neno la Mwisho: Onyesho Kuu la upendo wa Mungu**  
Na Rais M. Russell Ballard

## Mara ya kwanza

nilipoenda kwenye shule ya upili, kuna jambo moja nilihangaika nalo: pale somo jipya lilipotambulishwa, nilipata ugumu kuelewa. Jioni moja niliomba kwa Baba wa Mbinguni anisaidie nielewe na kushinda changamoto ile. Nilikuwa na imani, na niliweza kuelewa vizuri zaidi. Tangu hapo, sala na imani vimekuwa kwenye orodha yangu ya mambo ya kufanya shuleni na kila mahali ninapokwenda.

Kuwa katika shule ya wavulana kuna changamoto kwa sababu ya baadhi ya mambo yaliyo kinyume na maadili ambayo wanafunzi hufanya. Hilo linapotokea, maneno ya wazazi wangu huja akilini mwangu: "Usifanye jambo ambalo litamfukuza Roho Mtakatifu." Nina shukrani kwa ajili ya mama yangu, ambaye daima hunikumbusha kumsikiliza Roho Mtakatifu. Tunapofanya kile kilicho chema, Mungu hutubariki.

**Nyame S.,** miaka 16, Ghana



**W**akati mwingine maisha hugeuka juu chini na nje ndani. Unaweza kuwa unahofia kuhusu mambo ya familia, afya, matatizo shuleni, au idadi nyingine ya matukio yanayo-  
sumbua katika ulimwengu wa leo. Tunawezaje kupata amani binafsi katika ulimwengu wenye matatizo? Haijalishi ukosefu wako wa amani huja kutokana na matukio yaliyo nje ya uwezo wako au kutokana na mambo unayoweza kushawishi na kubadilisha, hapa kuna baadhi ya mawazo kukusaidia kupata amani ya ndani kupitia Yesu Kristo.

## **NJIA 4 ZA KUPATA AMANI KWA AJILI YAKO**

### **1. Fokasi kwenye yale ya milele**

Ni vigumu kuhisi amani wakati umefokasi tu katika wasiwasi wa muda mfupi. Lakini kama ukifokasi kwenye picha kubwa, mpango wa Mungu wa furaha, unaweza kupata amani katika kujua kwamba kile kinachoumiza kwa sasa hakitadumu milele. Kwa mfano, hekalu hutusaidia kufokasi kwenye umilele. Rais Gordon B. Hinckley (1910–2008) alisema kwamba hekaluni “mtajua amani ambayo haiwezi kupatikana sehemu nyingine yeyote.”<sup>1</sup>

### **2. Achana na kile kilicho nje ya uwezo wako**

Pale kitu kilicho nje ya uwezo wako kinapochukua amani yako, kinaweza kushawishi kwenye kuhisi kukosa tumaini ua hasira. Lakini haisaidii kudumu katika vitu usivyoweza kubadilisha. Bada-  
la yake, sogea karibu na Mwokozi ili kupata amani ya ndani hata kama maisha hayakuendei vizuri. Yeye ameahidi kukutumia Mfariji, Roho Mtakatifu (ona Yohana 14:26–27).

### **3. Samehe Wengine**

Mara nyingi jambo gumu la kuacha lipite ni ubaya unaohisi wakati mtu anapokukosea. Lakini Mzee Dieter F. Uchtdorf wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alifundisha: “Tutapokea shangwe ya msamaha katika maisha yetu wenyewe wakati tunapokuwa tayari kutoa shangwe hiyo bila kikwazo kwa wengine. . . . Kama matokeo, Roho wa Bwana atajaza nafsi zetu kwa shangwe inayoambatana na amani takatifu ya ufahamu (ona Mosia 4:2–3).”<sup>2</sup> Kumgeukia Mwokozi kunaweza kukusaidia kuwa huru kutokana na mizigo ya kihisia na kujazwa na amani.

### **4. Tubu na mtegemee Kristo**

Bila kujali nini kingine kinakwenda vizuri katika maisha yako, kubeba mzigo wa dhambi daima kutakunyang’anya amani. Wakati mwingine tunamhitaji askofu wetu atusaidie kutubu kikamilifu. Lakini sote tunahitaji kutubu mara kwa mara na, kupitia Upatanisho wa Yesu Kristo, kuwa huru kutokana na kila kitu kinachotuzuia kuwa zaidi kama Yeye.

# **KUTAFUTA AMANI**





# kwa Ajili Yako na Wengine katika Nyakati za Matatizo

Na Alex Hugie pamoja na Aspen Stander  
Magazeti ya Kanisa

*Hapa kuna njia nane za kujisaidia wewe  
mwenyewe na wengine kuhisi amani  
wakati maisha yanapokuwa magumu.*



## NJIA 4 ZA KUWASAIIDIA WENGINE KUPATA AMANI

### 1. Shiriki Injili ya Yesu Kristo.

Kama vile tunavyoweza kupata amani kwa ajili yetu kwa kufokasi juu ya Mwokozi, tunaweza kuwaongoza wengine Kwake kama “mwanzilishi wa amani” (Mosia 15:18) Kwa mfano, kujaribu kushiriki andiko au nukuu kutoka kwenye mkutano mkuu ambayo imekusaidia wewe kujifunza zaidi kuhusu Yesu Kristo.

### 2. Kuwa mpatanishi

Wasaidie rafiki zako au ndugu zako kutatua matatizo. Kama vile watu wa Anti-Nephi-Lehi katika kitabu cha Alma, tunaweza kuzika silaha zetu za vita—silaha kama umbea, kutafuta kisasi, au kuwa wabinafsi—na kuzibadilisha kwa vyombo vya amani: kuzungumza kwa ukarimu, kutii amri za Mungu, na kusamehe wengine (ona Alma 24:19).

### 3. Kuwa msikilizaji mzuri

Wakati mwingine watu wanaohangaika wanahitaji kuzungumza kwa uwazi kuhusu mawazo na hisia zao badala ya kunyamaza. Hatupaswi kutatua matatizo yao kwa ajili yao, bali tunaweza tu kusikiliza matatizo yao na kutoa msaada, kuonyesha upendo na uelewa kama wa Kristo.

### 4. Wahudumie wale walioko kwenye kata na jumua yako.

Ungeweza kujitolea kwenye kituo cha wasio na makazi, kuhudumu kama mwalimu mwenzi, au kuleta zawadi kwa familia mpya katika ujirani wako. Wasaidie watu kupata amani katika vitu vidogo. Kuwa na sehemu ya kudumu ya kula na kulala, mshauri wa kutegemewa, au uhakika mdogo kwamba mtu fulani anajali kunaweza kuwa na matokeo ya muda mrefu.

Yesu alizungumza maneno haya ya faraja kwa wale wote wanaohangaika kutafuta amani: “Amani nawaachieni, amani yangu nawapa: niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msiwe na wasiwasi moyoni mwenu, wala msifadhike.” (Yohana 14:27). Ikiwa tutajileta sisi na kuwaleta wengine karibu na Yesu Kristo, tunaweza kupata amani hata wakati maisha yanapokuwa magumu. ■

#### MUHTASARI

1. Gordon B. Hinckley, katika “Furahia katika Baraka za Hekalu,” *Liahona*, Des. 2002, 33.
2. Dieter F. Uchtdorf, “Hatua ya Kurudi Salama,” *Liahona*, Mei 2007, 101.



# MAISHA NI **MASAF**A





# MAREFU

*Vijana hawa Watakatifu wa Siku za Mwisho wanaishi leo ambapo Mtume Paulo aliishi wakati wa kipindi cha Agano Jipya. Na wanaishi kwa maneno yake.*

## **Na Sally Johnson Odekirk**

Magazeti ya Kanisa

**M**iezi michache iliyopita, darasa la seminari lilikutana katika Kilima cha Maazi, karibu na Atheni, Ugiriki, ambapo Mtume Paulo aliwahi kutoa mahubiri yenye nguvu (ona Matendo ya Mitume 17:22–34). Wanafunzi walizungumza kuhusu ushawishi wa seminari katika maisha yao, ikijumuisha mafundisho ya Paulo.

“Kuishi Ugiriki kunafanya Agano jipya kuwa halisi,” anasema Alexis H., miaka 18. “Baba yangu hupenda kwenda kwenye magofu tofauti ambapo Paulo alifundisha na angeshiriki andiko au kutusimulia hadithi kuhusu wapi tukio lilitendeka.

Kama vile Paulo alivyopata changamoto katika siku zake, vijana wa Ugiriki pia wanakabiliwa na masuala ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi. Mikutano ya vijana na kambi ya Wasichana havitokei kwa wingi huko Ugiriki, na hata kuhudhuria seminari kunaweza kuwa vigumu sana. Licha ya hizi na changamoto zingine, vijana wa Ugiriki hufanyia mazoezi maneno ya kutia moyo ya Paulo ya “kusimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili” (Wafilipi 1:27).

Kuishi Ugiriki humanisha waumini hawa vijana wanapata kufurahia hali ya hewa ya joto, fukwe, chakula, na dansi. Pia wao hufurahia sana kukutana pamoja wao kwa wao. Pale wanapokutana katika seminari na shughuli za tawi, wamekuwa imara katika imani na urafiki.




*"Nimejifunza kwamba injili inafanana kila mahali. Kushi ughaibuni, nimejifunza kufokasi kwenye kweli za injili na kuhisi Roho badala ya kuvutwa na utamaduni."*  
—Bryana W., 15



*"Niliandika neno kumbuka kwenye kioo changu ili kukumbuka yale yote yaliyotokea mwaka huu: KNV, kambi ya Wasichana, seminari. Inanisaidia kukumbuka wapi nimetoka."* —Marie H., 17



*"Ninajua kwamba ninapenda seminari ninaweza kuhisi kuridhika kujua kwamba ninafanya kile ninachohitaji kufanya, na ninajua kwamba kila kitu kitakuwa SAWA."* —Lizzie T., 17



*Loukia C., 15, alitoa ushuhuda wake kwa mara ya kwanza kwenye kambi ya Wasichana na baadaye alibatizwa.*



*Kundi la seminari mbele ya jumba Ila mkutano a Atheni.*

### Seminari katika Kilima cha Maazi

Wakati seminari ilipoanza Ugiriki miaka michache iliyopita, kulikuwa na wanafunzi watano tu. Walikutana asubuhi tatu kwa wiki, pamoja na wengine wakijiunga kupitia mkutano wa video wa mtandaoni. Wanakutana pia Jumatano mchana kwa ajili ya seminari, ikifuatiwa na shughuli. Wamekuwa karibu na kila mmoja na kuwa nuru kwa rafiki zao, ambao wanauona mfano wao. Pale rafiki zao wanapouliza maswali, vijana wawaleta seminari na kwenye Shughuli za pamoja.

Mvulana mmoja, Pavlos K., 15, anasema, "Kwenda seminari ni njia nzuri ya kuianza siku na hunisaidia kuwa imara. Kunaniweka katika hali ya mawazo ya kuwa mfano kwa wengine. Kunanisaidia kuanza siku nikitafakari kuhusu Yesu Kristo."

Pale vijana wanapokua katika nguvu na umoja, baraka na fursa huja. Kwa mfano, mnamo 2017 walibarikiwa kuhudhuria Kwa Ajili ya Nguvu Kwa Vijana (KNV), mkutano mkubwa wa vijana wa kanda. Wasichana pia walishiriki kwenye Kambi yao ya kwanza kabisa ya Wasichana huko Ugiriki. Kama matokeo, wamekuwa karibu zaidi kama kundi, na wasichana wawili walijiunga na Kanisa.

### Mkutano wa Kimataifa wa KNV

Mkutano, uliofanyika huko Ujerumani, uliwaleta pamoja vijana Watakatifu wa Siku za Mwisho kutoka Ulaya yote. Vijana kutoka Ugiriki na Cyprus walikuja kutoka mamia ya maili, na uzoefu wa mkutano ulikuwa na matokeo makubwa kwao. Kwa Maximos A., 14, "kitu cha kukumbukwa sana kwenye KNV ilikuwa ni pale tuliposhiriki shuhuda zetu. Kila mmoja alihisi Roho, na ilinipa msukumo wa kupata ushuhuda wangu mwenyewe."

"Mwanzoni vijana wanne tu walikuwa wainde," anaongeza Loukia C., 15, "lakini mwishoni, tulikuwa na 15 waliohudhuria—rekodi ya Ugiriki—ikijumuisha 3 marafiki wasio waumini."

"Ilikuwa ya kupendeza kuwa pamoja mahali fulani ambapo mnashiriki injili inayofanana na wewe si tofauti. Tulikuwa wote pamoja, na tulikuwa tukihisi Roho mmoja. Mambo haya yananisaidia."

"Baba yangu si muumini na asingeniruhusu niende kwenye KNV au kubatizwa," anasema Jesiana, 16. "Lakini waumini wa tawi walifunga kwa ajili yangu, na bibi yangu alizungumza na

baba yangu. Baada ya hilo alisema ningeweza kwenda!”

Kwenye KNV, nilipitia uzoefu wa mara ya kwanza kwa wingi, kama vile, “kushiriki katika masomo na shughuli na kushiriki ushuhuda wangu kulinisaidia kuelewa vile ilivyo hasa kuhisi Roho Mtakatifu. Sikuwahi kumhisi Roho kama vile hapo mbeleni, na nilikuwa na furaha na kuvutiwa. Nilitoa ushuhuda wangu kwa mara ya kwanza.”

Kwa kuongezea kwenye kushibishwa kiroho, vijana waliweza kupumzika na kuburudika pamoja kwenye mkutano. Haig T., 14, alikuja kwenye mkutano kutoka Cyprus. “Nilijifunza kuchangamana, kuwa na urafiki wa kweli, na kuburudika, hata katika nyakati ngumu.”

### Kambi kwa Wasichana

Kambi ya Wasichana ilikuwa na matokeo ya kufanana. Wasichana kumi na wawili walikutana na viongozi wao karibu na eneo la kale la vita la Masafa Marefu. Walitumia siku tatu pamoja, wakijifunza kutegemeana kwa ajili ya nguvu na kujipa moyo.

“Nilipokuwa na miaka 12,” anasema Loukia, “nilikwenda kanisani kwa mara ya kwanza na nilikuwa mwenye furaha, lakini kisha niligundua kwamba nilikuwa peke yangu wa miaka 12. Sasa, miaka miwili baadaye, tuna wasichana wengi ambao kwa mara ya kwanza tuliweza kuwa na kambi ya Wasichana. Walipokutana pamoja, anasema, “niligundua kile inachomaanisha kuwa Mtakatifu wa Siku za Mwisho. Tunapoishi injili, nuru inatuzingira.”



“Sehemu niliyoipenda zaidi ya KNV ilikuwa michezo, dansi, na mikutano ya makundi, ambayo ilikuwa mikutano na tafakari ya ibada za asubuhi. Ilinisaidia kuwa mwenye msaada zaidi na mvumilivu na kushukuru zaidi kwa ajili ya maandiko.”  
—Haig T., 14




Njiani kuelekea kwenye KNV huko Stuttgart, Ujerumani.



Kwenye mkutano wa KNV, matamshi ya tahajia ya neno “Omba,” kutoka Yakobo 1:5

# “Simameni imara katika roho moja, kwa moyo mmoja.”

Wafilipi 1:27



Irini S. Akifanya onyesho kwenye KNV



“Kwenye KNV, tulianza kuwa kundi na ilituimarisha. Ilinisaidia kubadilisha na kushawishi programu ya vijana wa Ugiriki kwa sababu sasa tunajua vizuri zaidi.” —Alexis H., 18



“Kuimba jukwaani kwenye KNV ilikuwa ni mojawapo ya jambo la kijasiri nililowahi kufanya na moja ya nyakati za muujiza nilizowahi kuwa nazo. Kwa sasa, nimejifunza jinsi tulivyo wa muhimu katika ulimwengu huu wa kupendeza.” —Irini S., 17



*"Kwenye kambi ya Wasichana nilijifunza kwamba maisha ni kama mbio za masafa marefu. Ilisaidia kukuza imani yangu, kujua kwamba tunapaswa kuendelea katika njia iliyo sahihi, kama vile tunakimbia mbio za masafa marefu. Uzoefu huo unanisaidia kukuza ushuhuda wangu na kuendelea kuwa na imani na kubaki kwenye njia sahihi."*  
—Winifred K., 14

# Maisha ni mbio za masafa marefu, siyo mbio fupi."

Dhamira ya kambi ya Wasichana



Wasichana kwenye Mbio za Masafa Marefu, Ugiriki.



"Sisi sote ni wa kipekee, kama vile changarawe ufukoni zilivyo." —Bryana W.



"Kutazama mawio ya jua kulileta roho wa utulivu, wa kupendeza." —Lizzie T.

Kwa Bryana W., 15, KNV na kambi ya Wasichana vilimsaidia kuvunja ukimya na kuzungumza na wengine. "Familia yangu inahama mara kwa mara, na nilipata wakati mgumu kuwa karibu na wengine kwa sababu nilikuwa na aibu," anasema. "Lakini kwa kuwa nilikuwa karibu na kundi letu kwenye KNV, nilipata marafiki wazuri. Wakati wa mkutano wa ushuhuda, tulishiriki hisia zetu, na nilitambua kwamba wengine walihisi sawa na vile nilivyohisi."

Marie H., 17, anakumbuka dhamira ya kambi, "Maisha ni mbio za masafa marefu, siyo mbio fupi." Wasichana na viongozi wao walijadili umuhimu wa kuvumilia na kumaliza mbio, anasema. "Ilinikumbusha kwamba ninaweza kuvumilia, kupiga hatua mwenyewe, na kubaki nimefokasi mwisho wa mstari. Kisha ninaweza kifikia mambo ambayo Baba wa Mbinguni ananitaka nifanye."

Mojawapo ya mambo ya kuvutia kambini ilikuwa ni mkutano wa ibada asubuhi wakati wa jua kuchomoza kwenye ufuko asubuhi yao ya mwisho. Lizzie T., 17, anasema, "Tulichukua maandiko yetu, tulikuwa na mkutano wa ibada, na kutazama machweo ya jua. Sote tulihisi upendo wa Mungu. Lilikuwa ni hitimisho la kupendeza kwa muda tuliotumia na kila mmoja wetu."

## Kuukabili Wakati Ujao Bila Woga

"Kutoka kwenye KNV na kambi ya Wasichana, nilijifunza mengi kuhusu injili na jinsi inavyoweza kunisaidia katika maisha yangu," anasema Irini S., 17. "Nilipata marafiki wengi na kujifunza jinsi ilivyo muhimu kuelezea mawazo na hisia zangu. Nilihisi




Kambi ya Wasichana, 2017—ya kwanza kabisa huko Ugiriki.

Roho Mtakatifu kwa kiasi kikubwa na upendo wa Mwokozi wetu, Yesu Kristo.”

Kuwa pamoja na vijana wengine Watakatifu wa Siku za Mwisho, anasema, kuliimarisha ujasiri wake. “Kabla ya KNV sikuweza kuona wema na mambo mazuri ambayo Mungu amefanya kwa ajili yetu na mipango ambayo Yeye bado anafanya kwa ajili yetu.”

“Hatupaswi kuathiriwa na yeyote au chochote kile kinachotuzunguka ambacho kitajaribu kutuvuta mbali kutoka kwenye kuishi injili,” Manasseh A., 17 anasema. “Injili inafanana kila mahali na tunapaswa daima kubaki kwenye njia sahihi.”


Na iwe ni Ugiriki au popote pale ulimwenguni, kushiriki njia hiyo pamoja kunaturuhusu kuwa wamoja katika roho. ■



“Nilipenda sana kuona jinsi ilivyo kuwa pamoja na vijana walio na imani inayofanana. Nilihisi kama sote tulikuwa tumeunganishwa katika njia maalumu, zaidi tu ya kujua jina la kila mmoja.”  
—Pavlos K., 15



“Ninafurahi kwamba nilipata fursa ya kukutana na vijana wengine ambao wanapitia mambo sawa na yale ninayofanya kila siku.” —Joshua K., 17



“KNV na kambi ya Wasichana vina hisia zinazofanana bila kujali popote unapoenda ulimwenguni. Nilifurahia kambi ndogo ya Wasichana kwa sababu ilikuwa rahisi kuwa karibu na kila mmoja.” —Olivia H., 15



“Mimi si muumini wa Kanisa, lakini ninakuja kila wiki ninayoweza kuja. Ninapendezwa na kile wasichana wanachokisimamia.” —Irene C., 14

## Kanisa huko Ugiriki



Mapema miaka ya 1900, Rigas Pofantis, mpiga chapa kutoka Atheni, alituma ombi kwa viongozi wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho kwa ajili ya taarifa. Rais wa misheni ya Kanisa huko Uturuki alimfundisha Pofantis, ambaye alibatizwa mnamo Oktoba 1905.



Kanisa lilipata ukuaji mdogo huko Ugiriki mpaka miaka ya 1905, wakati waumini wa Kanisa wenye asili ya Ugiriki-na Amerika huko jijini Salt Lake, Utah, Marekani, walipoanzisha jamii ya Watakatifu wa Siku za Mwisho yenye utamaduni wao ili kulinda urithi wao na kuendeleza umoja na nchi zao za asili.



Viongozi wa Kanisa waliunda mkusanyiko mdogo huko Atheni mnamo 1965 na kuunda tena upya mnamo 1967. Walianzisha misheni ya Ugiriki Atheni 1990 na kukamilisha ujenzi wa jumba la kwanza la ibada huko Ugiriki mnamo Mei 1999.



Atheni, Ugiriki, jumba la ibada huko Halandri



Uumini wa Kanisa: 802  
Mikusanyiko: 3

# “Je, ni kwa jinsi gani baraka yangu ya kipatriaki inaweza kunisaidia kufanya maamuzi?”

*“Baraka ya kipatriaki ni ufunuo kwa mpokeaji, hata mwonekano wa wazi katikati ya barabara, kulinda, kushawishi, na kuleta motisha ya kutenda na uadilifu. Baraka ya kipatriaki kiuhalisia ina sura kutoka kwenye kitabu chako cha uwezekano wa milele. . . .*

*“. . . ni Liahona ya nuru kukuongoza bila makosa kwenye nyumba yako ya mbinguni.”*

Rais Thomas S. Monson (1927–2018), “Baraka Yako ya Baba Mkuu: Liahona ya Nuru,” *Ensign*, Nov. 1986, 65, 67.



## Liahona Yetu Binafsi

Baraka za kipatriaki ni njia ambayo Baba wa Mbinguni hutusaidia kujua utambulisho wetu kabla ya

maisha ya duniani, utambulisho wetu wa maisha ya duniani, na utambulisho wa milele. Kwa kujua kweli hizi tatu kutuhusu sisi, kunatusaidia kufuata mpango Mungu alionao kwa ajili yetu. Tunajua sisi ni akina nani, kwa nini tuko hapa, na wapi tunaweza kuwa. Kama Liahona ilivyofanya kazi kulingana na imani na bidii ya Nefi na familia yake katika kufuata ushauri wake (ona 1 Nefi 16:28), sisi pia tunaweza kuwa waaminifu na wenye bidii katika kufuata Liahona zetu weneye na ushauri wake, ambao utatuongoza kwenye uwezekano wetu mtakatifu.

*Mzee Utai, miaka 20, Misheni ya Ajentina Salta*



## Mtazamo wa Milele

Ninapojihisi kuwa sijui chochote katika kufanya maamuzi, ninageukia baraka yangu ya kipatriaki

na kutafakari ufunuo wake mtakatifu. Na kisha kufanya maamuzi kunakuwa rahisi. Siyo tu inanisaidia kuvumilia maisha yangu ya duniani na kuvuna baraka zilizoahidiwa, lakini pia inanikumbusha kujiandaa kuingia kwa kustahili katika ufalme wa Mungu. Inanisaidia mara kwa mara kukua katika imani, kuamini mapeenzi ya Bwana, na kuishi kwa mtazamo wa milele.

*Abegail F., miaka 18, Cagayan Valley, Ufilipino*



## Ushauri wa Mbinguni

Baraka yangu ya kipatriaki inanipa ushauri kutoka kwa Baba yangu wa Mbinguni. Ikiwa nitafuata

ushauri huo, ninajua nitapata ufunuo katika maamuzi ninayohitaji kufanya. Anajibu baadhi ya maswali yangu hata kabla sijayauliza.

*Cami H., miaka 16, Utah, Marekani*

## Msikilize Roho

Ikiwa unatafuta faraja na mwongozo au jibu la swali muhimu, unaweza kuomba kwa dhati na kusoma baraka yako ya baba mkuu kwa kusudi halisi la moyo, wakati ukimsikiliza Roho. Kupekua maandiko kunasaidia pia. Ninaamini kwamba ukifanya hivi kwa kusudi halisi, Bwana atakujibu, katika muda Wake, katika njia nzuri zaidi.

*Kezia B., miaka 15, Hawaii, Marekani*

## Baraka Zilizoahidiwa

Baraka za kipatriaki hutuambia kile Mungu anachotaka kutubariki nacho. Yeye hutupatia maonyo na kufafanua jinsi tunavyoweza kuwa zaidi kama Yeye. Tunapojua kile Baba wa Mbinguni alichonacho kwa ajili yetu na jinsi ya kukipata, tutachagua na kutenda ipasavyo kukipata.

*Hunter H., miaka 18, Utah, Marekani*

*Majibu yanakusudiwa kwa ajili ya msaada na mtazamo, si kama matamko rasmi ya mafundisho ya Kanisa.*



## Kama msichana, je, ninapaswa kufokasi zaidi kwenye elimu na kazi au kwenye kuwa mke na mama?

Tunajua kwamba “familia ni kiini cha mpango wa Muumbaji” na kwamba “Akina mama kimsingi wana wajibu wa malezi ya watoto wao.”<sup>1</sup> Na pia tunajua kwamba, kwa sababu nyingi nzuri, wote wanaume na wanawake wameshauriwa na manabii kupata elimu.<sup>2</sup> Kwa kuongezea, tunajua kwamba wanawake wengi aidha watahitaji au wanataka kutafuta kazi.

Rais Dallin H. Oaks, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza, amesema kwamba kwa wanawake, uchaguzi si kati ya aidha familia au elimu na kazi. “Muda muafaka ndio tunaopaswa kuchagua,” alisema. “Na tunatafuta mwongozo wa kiungu wa Bwana na mafundisho ya watumishi Wake katika kufanya hilo.”<sup>3</sup>

Panga kupata elimu, na panga kuwa na familia. Unaweza pia kupanga kuwa na kazi. Katika yote haya, fokasi yako inapaswa kuwa kwenye kufuata mpango wa Baba wa Mbinguni na kutafuta mapenzi Yake.

### MUHTASARI

1. “Familia: Tangazo kwa Ulimwengu,” familyproclamation.lds.org.
2. Ona *Kwa Nguvu ya Vijana* (2011), 9.
3. Dallin H. Oaks, shughuli ya uso kwa uso na Mzee Oaks pamoja na Mzee Ballard (shughuli ya vijana wakubwa waseja ulimwenguni kote, Nov 19, 2017), broadcasts.lds.org.

Kwenye [lds.org/go/41961](https://www.lds.org/go/41961), kijana mkubwa anashiriki hadithi yake ya kutokuwa na uhakika ikiwa anapaswa kufokasi kwenye kazi yake au familia yake. Ona kile Rais Russell M. Nelson alichomwambia.

## Unafikiria Nini?

“Unasema nini wakati marafiki zako wanapokosa kuamini kwamba mambo kama Ono la Kwanza yanaweza kutokoe?”

Wasilisha majibu yako na, ukipenda, picha ya ubora wa hali ya juu kabla ya Mei 15, 2019, kwenda [liahona.lds.org](https://www.lds.org) (bofya “Wasilisha Makala” au Maoni). Au tuma jibu lako kwa barua pepe na picha yako kwenda [liahona@ldschurch.org](mailto:liahona@ldschurch.org). Jumuisha jina lako kamili na majina ya kata na kigingi chako (au tawi na wilaya)

Majibu yanaweza kuhaririwa kwa ajili ya urefu au ufafanuzi.




**Na David Dickson**  
Magazeti ya Kanisa

**K**rismasi mara nyingi hupata umakini wakati inapofikia mapumziko. Hata hivyo bila matukio ya muda mrefu uliopita tunayo sherehekea kila Pasaka, Krismasi isingekuwapo.

Rais Gordon B. Hincley (1910–2008) aliwahi kufundisha, “Hapangukuwapo na Krismasi kama isingekuwapo Pasaka. Mtoto Yesu wa Bethlehemu angekuwa kama mtoto mwingine tu bila Kristo wa kukombo wa Gethsemane na wa Kalvari, na ushindi wa kweli wa Ufufuko.”<sup>1</sup>

Hapa kuna baadhi ya tamaduni chache ambazo ungeweza kufikiria kuongeza kwenye usherehekeaji wako wa mapema.



**1**

**Nenda Kaimbe Nyimbo za Furaha**

Ukiachilia mbali tafsiri ya ajabu ajabu kuhusu kulungu na kibwengo, Krismas ni kuhusu Yesu Kristo. Pasaka ni wakati muafaka kwa ajili ya muziki kuhusu Mwokozi, na ndiyo, hata kama ukiimbwa mbele ya milango ya jirani zako.

Kama umeishiwa na mawazo, angalia kipengele cha “mada” cha kitabu cha nyimbo za kanisa kwenye “Pasaka” na “Upatanisho” kwa ajili ya nyimbo. Wimbo wowote unaomsifu Yesu Kristo ni sahihi kwa ajili ya nyimbo za furaha za Pasaka.



**2**

**Msamehe Mtu**

Ni mara ngapi umekuwa na shukrani kwa zawadi ya toba? Pasaka inatoa fursa ya kuweka mawazo zaidi kwenye jinsi tunavyotoa roho sawa na hiyo ya msamaha kwa wengine.

Yesu alifundisha: “Kwa hiyo, ninawaambia, kwamba mnapaswa kusameheana ninyi kwa ninyi. . . .

“Mimi, Bwana, nitamsamehe yule nitakaye kumsamehe, lakini ninyi mnatakiwa kuwasamehe watu wote” (Mafundisho na Maagano 64:9–10).

Jjulize: Ni nani unayehifadhi hisia mbaya dhidi yake? Omba kwa ajili ya nguvu ili kumsamehe mtu huyu, na mwache Mwokozi asaidie hisia hizo za uchungu kutoweka.



**3**

**Vaa sura ya Kuigiza, Kucheza au Ugizaji mwingine**

Unaweza kuandaa igizo la Pasaka. Mfano rahisi unaweza kuwa usomaji wa maandiko kwa ajili ya jioni ya familia nyumbani au tamasha la kuimba pamoja na jumua.

# Jaribu Baadhi ya Tamaduni Mpya za Pasaka





4

### Tembelea Makaburi ya Wapendwa Wako

Kwa sababu ya Yesu Kristo, kifo kimepoteza uchungu wake (ona 1 Wakorintho 15:55).

Tumia muda kutembelea makaburi ya wapendwa wako kutafakari habari hii njema.

Unaweza hata kusoma kwa sauti baadhi ya maandiko unayoyapenda ambayo yanahusiana na Ufufuo wakati ukitembelea makaburi haya. machache (kati ya maandiko *mengi*) ya kuzingatia kwa ajili ya hili ni 1 Wakorintho 15:20–22; Alma 11:42–44; na Mafundisho na Maagano 88:14–16



5

### Kuwa Bora Zaidi

Pasaka inaheshimu matukio ya Gethsemane, kilichotukia msalabani, Mwokozi kufufuka kutoka wafu siku ya tatu, na kisha kuhudumu Kwake kwa siku 40 kabla ya kupaa mbinguni.

Kwa kuongezea, muda mfupi baada ya kupaa mbinguni, Yesu Kristo aliwatokea Wanefi na kuwahudumia (ona 3 Nefi 11–28). Hayo ni mengi ya kusherehekea!

Kwa nini usipanue msimu wako wa Pasaka? Acha nafsi yako ifurahie kwa muda mrefu katika miujiza ya Pasaka. Fanya juhudi za makusudi kuwa zaidi kama Kristo kipindi cha siku

40 baada ya Pasaka. Kwa ajili ya msukumo, fikiria mwaliko ufuatao kutoka kwa Rais Russell M. Nelson: “Weka wakfu sehemu ya muda wako kila wiki ili kujifunza *kila kitu* Yesu alichosema na kufanya kama ilivyoandikwa katika Agano la Kale, kwani Yeye ni Yehova wa Agano la Kale. Jifunze sheria Zake kama zilivyoandikwa katika Agano Jipya, kwani Yeye ni Kristo wake. Jifunze mafundisho Yake kama yalivyoandikwa katika Kitabu cha Mormoni, kwani hakuna kitabu cha maandiko ambacho kwacho kazi Yake na huduma Yake vimefunuliwa wazi. Na jifunze maneno Yake kama yalivyoandikwa katika Mafundisho na Maagano, kwani anaendelea kufundisha watu Wake katika kipindi hiki cha maongozi ya Mungu.”<sup>2</sup>

### Tamaduni Zako Zinasubiri

Mzee Dieter F. Uchtdorf wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili amefundisha, “Kujua siku muhimu zaidi katika historia, lazima turudi nyuma kwenye jioni ile karibu miaka 2000 iliyopita katika Bustani ya Gethsemane wakati Yesu Kristo alipopiga magoti kuomba na kujitoa Yeye Mwenyewe dhabihu kama malipo ya dhambi zetu.”<sup>3</sup>

Matukio muhimu zaidi katika historia yana thamani kutengewa muda wa kutafakari kila mwaka. Tamaduni hutusaidia kufanya hivyo, iwe ni zile zilizopo kwenye orodha hii au yoyote ile utakayochagua.

Ni kipi utaongeza mwaka huu? ■

#### MUHTASARI

1. Gordon B. Hinckley, “Maajabu na Hadithi ya Kweli ya Krismasi,” *Ensign*, Des. 2000, 5.
2. Russell M. Nelson, “Manabii, Uongozi, na Sheria Takatifu” (worldwide devotional for young adults, Jan. 8, 2017), [broadcasts.lds.org](http://broadcasts.lds.org).
3. Dieter F. Uchtdorf, “Tazama Mtu!” 107–10 *Liahona*, Mei. 2018, 108.

*Pasaka hii, tumia muda mwingi zaidi kukumbuka zawadi kuu kuliko zote iliyowahi kutolewa.*

# Onyesho Kuu la Upendo wa Mungu

Na Mzee M. Russell Ballard

Kaimu Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

Mungu huonyesha upendo wake kwetu kwa kutoa mwongozo tunaohitaji ili kundelea na kufikia uwezekano wetu. Yeye anayejua mengi kutuhusu sisi, na uwezekano wetu wa milele ametupatia ushauri mtakatifu na amri katika vitabu Vyake vya mwongozo—maandiko matakatifu. Tunapoelewa na kufuata maelekezo haya, maisha yetu yana lengo na maana. Tunajifunza kwamba Muumba wetu anatupenda na anataka sana furaha yetu. Katika onyesho lisiloweza kufananishwa la upendo huu mtakatifu kwetu, Yeye alimtuma Mwana Wake wa Pekee, Yesu Kristo.

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanaye wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

“Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye” (Yohana —173:16).

Yesu alizaliwa katika ulimwengu. Aliishi maisha makamilifu na, kwa kufanya hivyo, alitegeneza njia kwa ajili yetu kufuata. Yeye aliwafundisha wanafunzi Wake: “Mimi ni nuru ya ulimwengu: yule ambaye ananifuata mimi hatatembea gizani, bali atapata nuru ya uzima” (Yohana 8:12).


Tunaweza kuanza kuelewa kina cha upendo wa Kristo kwetu tunapofikiria kwamba Yeye alikuwa tayari kufanya upatanisho na kuteseka kwa maumivu ya dhambi zetu, “Mateso ambayo yaliyosababisha [yeye], hata Mungu, mkuu kuliko wote, kutetemeka kwa sababu ya maumivu, na kutoka damu kwenye kila kinyweleo, na kuteseka mwili na roho” (Mafundisho na Maagano 19:18).

Pasaka hii, acha tutoe shukrani za kipekee kwa Mungu kwa ajili ya Upatanisho na Ufufuko wa Mwanaye mpendwa, Yesu Kristo. Kwani ndani Yake, Kwake, na kupitia Kwake, hali hii ya muda ya maisha ya kufa inaweza kufanywa ya kudumu, uwepo mkamilifu, ambao maneno hayawezi kuelezea shangwe yetu.

Maajabu yote ya asili ni tazamo la mara moja la nguvu Yake takatifu na onyesho la upendo Wake. Bado muujiza mkuu wa miujiza yote unatusubiri. Utatokea wakati, kwa nguvu Yake, tutatoka kwenye kifo na kaburi kwenda kwenye ulimwengu mpya ambao hautapita, ambapo, ikiwa tutastahili, tutakuwa Naye na baba Yetu wa Mbinguni milele na milele. ■

*Kutoka katika hotuba ya mkutano mkuu wa Aprili 1988.*

Alimfanyia kazi baba yake  
**uuzaji magari**  
mapema miaka ya 1950 na  
alikuwa **muuzaji wa**  
**kiwango cha juu.**



Alizaliwa Oktoba 8,  
1928, huko  
**Jijini Salt**  
**Lake, Utah.**



Alisoma  
**Chuo Kikuu**  
**cha Utah.**

Rais

# M. RUSSELL BALLARD



Alitumikia  
umisionari wa  
muda wote huko  
**Uingereza.**



Alitumikia kama  
**rais wa**  
**misheni**  
katika Misheni ya  
Kanada Toronto  
kuanzia 1974  
mpaka 1977.



Alikutana na mke  
wake, Barbara  
Bowen, Chuo  
Kikuu cha Utah  
**“Siku ya**  
**Dansi.”**



Alimuoa  
**Barbara**  
**Bowen**  
katika Hekalu la  
Salt Lake mnamo  
Agosti 28, 1951.



**Babu:**  
Mzee Melvin J.  
Ballard wa Akidi  
ya Mitume Kumi  
na Wawili



**Babu:**  
Mzee Hyrum Mack  
Smith wa Akidi ya  
Mitume Kumi na  
Wawili



Ana watoto **7**,  
wajukuu **43**,  
vitukuu **91.**

Aliidhinishwa kwenye  
**Akidi ya**  
**Mitume Kumi**  
**na Wawili**  
mnamo Oktoba 6, 1985.



Alitengwa kama  
**Rais**  
**Mkaimu**  
wa Akidi ya Mitume  
Kumi na Wawili  
mnamo  
Januari 14, 2018.

Baada ya mkutano  
mkuu wa Oktoba 1980,  
aliandika zaidi ya  
**barua 600**  
za kutia moyo kwa  
waumini waliokuwa  
wakihangaika na  
shuhuda zao.


Hutunza **biskuti ya Oreo**  
iliyofungwa kwenye meza yake kama  
ukumbusho wa mvulana ambaye  
alikuwa amefanya safari ndefu kwenda  
kwenye kambi ya wakimbizi, alipokea  
kifurushi cha biskuti, na akatoa ya  
kwanza kwa Rais Ballard.



## KURASA ZA ZIADA KWA AJILI YA WATOTO

Tumia *Rafiki* mpya vizuri. Kama huna watoto nyumbani kwako, unaweza:

- Kushiriki *Rafiki* na familia ambayo haipokei *Liahona*.
- Mpe rafiki au jirani.
- Mpatie kiongozi au mwalimu wa Msingi.



VIJANA WAKUBWA  
UNAHITAJI USAIDIZI  
KWA MAAMUZI  
MAKUBWA?

42

VIJANA  
KUTAFUTA AMANI  
KWA AJILI YAKO NA  
WENGINE

52

PASAKA  
TAMADUNI MPYA

62

KANISA LA  
YESU KRISTO  
LA WATAKATIFU  
WA SIKU ZA MWISHO



Aprili 2019

Sehemu ya watoto ya *Liahona*, inayochochishwa na Kanisa La Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

# Rafiki



Hadithi ya  
**PASAKA**

Ona kurasa 4-6



Na Rais  
Russell M. Nelson

# ZAWADI Kuu ya Mungu

Siku moja mimi na Dada Nelson tuliona samaki wa Skitropiki kwenye bwawa la samaki. Samaki wenye rangi za kung'aa na maumbo na ukubwa tofauti walienda mbele na nyuma. Nilimuuliza mfanyakazi aliyekuwa karibu, "Nani huwalisha samaki hawa wa kupendeza?"

Alijibu, "Mimi."

Kisha niliuliza, "Je, samaki wamewahi kukushukuru?"

Alijibu, "Bado!"

Baadhi ya watu ni kama samaki hao. Hawamtambui Mungu na wema Wake kwao. Ingekuwa vema kiasi gani ikiwa tungejua zaidi juu ya upendo wa Mungu na kudhihirisha shukrani Kwake.

## Shukrani kwa ajili ya Yesu Kristo.

Mungu alimtuma Mwana Wake, Yesu Kristo, kutusaidia. Alifanya hivyo kwa sababu anatupenda sana.

Yesu Alikuwa **kutukombo**.

Kwa sababu ya **Upatanisho** Wake, tunaweza kufufuka baada ya kufa.

Kwa sababu ya Upatanisho Wake, tunaweza kurudi kuishi na Baba wa Mbinguni milele.

Yesu alielezea:

"Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima:

Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi: Naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele (Yohana 11:25-26).

Huu ndio ujumbe wa kupendeza wa Pasaka. ●

*Kutoka "Shukrani Ziwe kwa Mungu,"  
Liahona, Mei 2012, 77-80.*



## Yesu ni Mwokozi Wangu

Yesu alifufuka asubuhi ya Pasaka. Soma sentensi kujua kile Yeye alichofanya kwa ajili yetu. Paka rangi mwale wa jua baada ya kusoma kila sentensi. Kisha paka sehemu iliyobaki ya picha.

Yesu aliteseka Gerhsemane na pale msalabani kutuokoa kutokana na dhambi zetu.

Yesu alikufa na kufufuka ili kutuokoa kutokana na kifo.

Yesu alitupaio sakramenti ili kutusaidia sisi kumkumbuka Yeye.

Yesu Kristo alitufundisha kuwasamehe wengine.

Yesu alituonyesha jinsi ya kuwa wakarimu.

Kwa sababu ya Yesu, sote tutafufuka baada ya kufa.

# Hadithi ya Pasaka



Yesu aliwapenda rafiki Zake. Yeye aliosha miguu yao.  
Kisha Aliwapa sakramenti. Aliwaambia wamkumbuke Yeye.  
Aliwaambia wapendane.




Baadaye, Yesu  
alikwenda Bustanini.  
Aliomba kwa ajili yetu  
sote. Alihisi maumivu  
ya magonjwa yetu.  
Alihisi maumivu ya  
dhambi zetu.



Watu wenye hasira walimchukua Yesu. Walimuumiza. Alikufa msalabani kwa ajili yetu. Rafiki Zake waliuweka mwili Wake katika kaburi.



Siku tatu baadaye, rafiki Zake walirudi. Kaburi lilikuwa tupu! Malaika waliwaambia, “Amefufuka.” Yesu alikuwa hai tena! Kwa sababu ya Yesu, sisi sote tutaishi baada ya kufa.



Yesu ananipenda. Ninaweza kuifanya Pasaka kuwa maalumu  
kwa kumkumbuka Yeye. ●

*Soma kuhusu asubuhi ya Pasaka katika Mathayo 28.*

# Nikirudi Kwake

*Kwa furaha* ♩ = 90-96

Maneno na music na Sally DeFord

F C Dm B<sup>b</sup> C F

1. M - chu - nga a - pe - nda ko - ndo' Na wa - ki - po - te - a Ye -  
 2. Bwa - na a - tu - pe - nda wo - te Na ni - ki - mu - a - cha Ye -  
 3. A - na - ni - o - nye - sha nji - a Ni - ta - ka - vyo - i - shi Ha -

C<sup>7</sup> Am Dm Gm C<sup>7</sup>

ye hu - wa - ta - fu - ta A - wa - i - ta wo - te Na  
 ye hu - ni - ta - fu - ta U - si - ku, m - cha - na Ni -  
 ta ni - ki - ko - se - a A - ta - ni - sa - me - he Hi -

F Dm Gm C<sup>7</sup> A A<sup>7</sup> Dm

wa - na - m - si - ki - li - za Wa - m - ki - mbi - li - a Na -  
 ta - m - fu - a - ta Bwa - na Ni - ta - e - nda kwa - ke Na  
 vyo ni - ta - m - si - ki - za Ni - ta - tu - bu dha - mbi Na

B<sup>b</sup> C<sup>7</sup> F Dm B<sup>b</sup> C<sup>7</sup> F

ye hu - wa - ku - mba - ti - a Wa - ki - ru - di kwa - ke  
 a - ta - ni - ku - mba - ti - a Ni - ki - ru - di kwa - ke  
 a - ta - ni - fu - ra - hi - sha Ni - ki - ru - di kwa - ke

© 2019 na Sally DeFord. Haki zote zimehifadhiwa.

Wimbo huu unaweza kunakiliwa kwa ajili ya mahitaji, yasiyo ya kibiashara ya matumizi kanisani ama nyumbani.

Notisi hii lazima ijumuishwe katika nakala inayotengenezwa.

## Na Jane McBride

Imetokana na tukio halisi

“Fanya lile lililo jema” (2 Wakorintho 13:7).

“Nataka umwangelie mdogo wako,” Mama alisema. “Mimi na baba yako tunakwenda kumsaidia mgonjwa.”

Nilitazama juu nikisimama kufagia sakafu ya nyumba yetu ndogo na kutikisa kichwa kwa kukubali. Mama alikuwa rais wa Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama, na mara nyingi alikwenda kuwatembelea akina dada katika kata yetu.

“Asante, Arlyn,” Mama alisema, akibusu paji la uso wangu. “John amelala. Na kuna unga wa mkate unaumuka juu ya kaunta. Tafadhali usiuguse.”

Nilitazama kupitia upenyo wa mlango pale yeye na Baba walipoendesha gari la kukokotwa na farasi kuelekea chini kwenye njia yetu ya vumbi. Nilijisikia fahari kwamba Mama aliniamini.

Nilipokuwa nikifagia jikoni, nilisimama kuangalia unga wa mkate. Nilisubiri kwa shauku Mama auoke usiku. Kwa kawaida tulikula mkate freshi uliookwa ukiwa na jemu iliyotengenezwa nyumbani. Lakini tuliishiwa jemu miezi mitatu iliyopita.

Jemu! Wazo lilinipa njaa ya kitu kitamu. Nilitazama juu kwenye chupa ya sukari, juu kabisa ya rafu. Nilijua Mama alikuwa akiitunza kutengeneza jemu nyingine zaidi.

Lakini kadiri zaidi nilivyofikiria kuhusu sukari, ndivyo nilivyohisi njaa. Hatimaye, nilivuta kiti karibu na rafu na kufika juu. Vidole vyangu vilikuwa karibu viguse chupa ya sukari. Niliivuta karibu kwenye ukingo wa rafu. . . .

Na kisha chupa ilitoleza kutoka kwenye rafu! Nilijaribu kuidaka, lakini ilidondoka kwa kishindo kikubwa katikati kabisa ya unga wa mkate. Sukari ilimwagika kote kwenye mkate na kwenye rafu na juu ya sakafu.

“Jamani!” Nilipiga kelele. Kitendo hicho kilimwamsha mdogo wangu. Alianza kulia. *Mimi* nilitaka kulia pia. Ni nini mama atasema kuhusu jambo hili?



# Uaminifu wa Kupendeza



Baada ya kumbembeleza John, nilijitahidi kadiri niwezavyo kuondoa sukari. Nilivuta chupa kutoka kwenye unga na kuiosha. Nilifuta sukari kutoka kwenye kaunta na sakafuni. Lakini hakuna ambacho ningeweza kufanya kuondoa sukari kutoka kwenye unga.

Nilifikiria kuhusu kurudisha chupa juu ya rafu. Pengine Mama asingegundua ilikuwa tupu. Lakini nilijua kwamba hilo halikuwa sawa. Hivyo niliweka chupa juu ya meza na kumsubiri Mama na Baba warudi nyumbani.

Walipofika nyumbani, Mama aligundua chupa ya sukari mara moja.

Nilivuta pumzi ndefu. “Nilitaka tu kuonja sukari. Lakini niligonga chupa kutoka kwenye rafu. Nilijaribu kuisafisha, lakini sikuweza kuitoa kutoka kwenye unga wa mkate.” Maneno yalitoka kwa kasi pale nilipokuwa nimetazama chini sakafuni.

Mama alikuwa kimya kwa muda.

“Nisamehe,” Nilinong’ona.

Mama alishusha pumzi. “Sawa, nadhani mkate utakuwa mtamu kupitiliza usiku wa leo,” alisema Nilitazama juu. Alinipa tabasamu kidogo. “Asante kwa kutuambia kilichotokea.”

Tulipokula mkate wa sukari usiku ule, Mama na Baba pamoja na mimi tulizungumza kuhusu uaminifu.

“Sote tunafanya makosa mengi katika maisha,” Baba alisema. “Lakini tunapokuwa waaminifu na kujaribu kutubu, Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo wanafurahi. Daima tutabarikiwa kwa kuwa wakweli— hata kama inaonekana vigumu mwanzoni.”

Bado nilikuwa na huzuni kwamba nilimwaga sukari. Nilijua yawezekana tusingekuwa na jemu nyingi mwaka huu kwa sababu ya kosa langu. Lakini nilikuwa na furaha nilisema ukweli. Hiyo ilikuwa ni hisia nzuri ambayo hakuna kiasi cha sukari kingeweza kuileta. ●

*Mwandishi anaishi huko Colorado, Marekani.*



“Kutii amri takatifu kunaleta baraka, kila mara! Kuvunja amri takatifu huleta kupoteza baraka, kila mara!”

**Rais Russell M. Nelson, “Acha Imani Yako Ionekane,” *Liahona*, Mei 2014, 30.**

# Mzee Bednar Anazuru India

Mzee David A. Bednar alisafiri na mke wake, Susan Bednar, ili kushiriki ushuhuda wa Yesu Kristo pamoja na waumini wa Kanisa huko India. India ni mojawapo ya nchi kubwa ulimwenguni. Na karibuni itakuwa na hekalu lake la kwanza!



Mzee na Dada Bednar walikwenda jiji la Rajahmundry. Mtume hajawahi kufika huko awali.



Watoto waliweza kusalimiana kwa mikono na Mzee Bednar.



Katika mkutano kwenye jiji la Hyderabad, msichana huyu alipata nafasi ya kumuuliza Mzee Bednar swali.



"Kadiri kwa wingi ninavyosafiri ulimwenguni, ndivyo ninavyozuru mataifa mengi, ndivyo ninavyopata watu wengi zaidi ninaobarikiwa kujifunza kutoka kwao, ndivyo zaidi ninavyokuta kwamba ulimwenguni kote watu ni kama wanafanana!"





Kila mmoja alikuwa na furaha kusikia ushuhuda wa mtume wa Mungu!



## OANISHA TEMBO

India ina takriban tembo 30,000. Ni jozi ngapi zinazofanana unaweza kupata hapa chini? Ni aina gani ya baadhi ya wanyama unaowapenda sana ambao Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo waliumba?






# MANIABI na MITUME wetu

Yesu Kristo anaongoza Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho kupitia manabii na mitume. Soma kuhusu wao hapa chini. Kisha **kata na uondoe picha kwenye ukurasa wa R23** na uzigandishe mahali pake katika chati. Weka gundi juu ya kila picha ili uweze kuziunua kwa ajili ya kusoma kwele zilizoko chini!


- Alisafisha duka la ufundi realio kama kazi yake ya kwanza
- Alikuwa mwanasheria na hakimu wa juu wa Mahakama ya Utah
- Alikuwa rais wa Chuo Kikuu cha Brigham Young



### Rais Dallin H. Oaks

Mshauri wa kwanza katika Urasis wa Kwanza

- Alikuwa daktari mpsuaji wa moyo
- Alijifunza lugha nyingi, ikiwemo Kichina
- Ana watoto kumi: 9 mabinti na 1 wa kiume



### Rais Russell M. Nelson

Rais wa 17 wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho


- Alicheza mpira wa kikapu akiwa shule ya upili
- Alijifunza fizikia kutoka kwa baba yake kwenye ubao wa chaki wa familia yao
- Alikuwa rais wa Chuo cha Ricks, sasa Chuo Kikuu cha Brigham Young-Idaho



### Rais Henry B. Eyring

Mshauri wa Pili katika Urasis wa Kwanza


- Alipewa jina la utani la "askofu" alipokuwa chuoni kwa sababu ya viwango vyake vya juu
- Alikuwa mfunyabiashara wa magari
- Alitumikia kama mmisionari huko Uingereza na kama rais wa misheni huko Toronto, Kanada



### Rais M. Russell Ballard

Kaimu Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alikuwa mwenzwa mmisionari wa Mzee Cook huko Uingereza
- Alifanya kazi kwenye Mfumo wa Elimu wa Kanisa
- Alikuwa rais wa Chuo Kikuu cha Brigham Young



### Mzee Jeffrey R. Holland

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili


- Alikuwa mkimbizi mara mbili alipokuwa mitoto
- Alikuwa rubani wa ndege
- Hufurahia kuteleza kwenye theluji na watoto wake pamoja na wajukuu



### Mzee Dieter F. Uchtdorf

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

- Alikuwa mlinzi kwenye timu yake ya mpira ya shule ya upili
- Baada ya kutumikia misheni huko Ujerumani, alimbatiza baba yake kuwa muumini wa Kanisa
- Alikuwa rais wa Chuo cha Ricks wakati kilipokuwa Chuo Kikuu cha Brigham Young-Idaho



### Mzee David A. Bednar

Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili



- Alipata ushuhuda baada ya kusoma maandiko na kuomba pamoja na kaka yake mkubwa
- Alimwona mkewe mtarajiwa kwenye onyesho la vipaji katika shule ya upili.
- Alitumikia kama kiongozi wa Kanisa huko Ufilipino na Visiwa vya Pasifiki



### Mzee Quentin L. Cook

*Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili*

- Alioka mkate wa nyumbani kwa ajili ya familia yake changa
- Alishiriki katika tamasha la Mlima Cumorah huko New York akiwa kijana aliyebelehe
- Alifanya kazi kama mwana-sheria kabla ya kuitwa kama Mfume



### Mzee D. Todd Christofferson

*Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili*

- Alitumikia kama mmisionari na baadaye kama rais wa misheni ya Japani
- Alianzisha biashara ya kutengeneza na kuuza vifaa vya mazoezi
- Alitumikia kama askofu wa Kanisa lote



### Mzee Gary E. Stevenson

*Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili*

- Alikulika katika shamba la kufugia ng'ombe huko Idaho, Marekani
- Alitumikia kama mmisionari na rais wa misheni huko Ufaransa
- Anazungumza Kifaransa, Kireno, Kihispania, na Kiingereza



### Mzee Neil L. Andersen

*Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili*

- Anapenda wanyama, ikijumuisha pengwini
- Hupenda kukutana na watu katika kila nchi
- Ana rekodi ya historia ya familia inayorudi nyuma mpaka kwa Dragon Gong wa kwanza miaka 837 Baada ya Kristo.



### Mzee Gerrit W. Gong

*Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili*

- Alikuwa rais wa misheni huko New York, Marekani
- Kauli mbiu yake ni "Ni watu ndio wenye umuhimu mkubwa"
- Aliweka wakfu jengo la kwanza la Watakatifu wa Siku za Mwisho huko Jamhuri ya Cheki



### Mzee Ronald A. Rasband

*Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili*

- Anatokea Brazil na alitumikia kama mmisionari huko na kama rais wa misheni ya Urusi
- Alijifunza kuhusu Kanisa pamoja na familia yake kama mvulana mdogo
- Alianza kujiandaa kwa umisio-onari alipokuwa na miaka 12



### Mzee Ulisses Soares

*Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili*

Angalia jibu lako kwenye [lds.org/prophets-and-apostles](https://lds.org/prophets-and-apostles).

# Koti Lililopotea

**Na Sheila Kindred**

Imetokana na hadithi ya kweli

*“Mimi, Bwana, nitamsamehe yule nitakaye kumsamehe, lakini ninyi mnatakiwa kuwasamehe watu wote” (Mafundisho na Maagano 64:10).*

“**M**ama koti langu halipo!” Brad alisema. Ilikuwa ni muda wa kwenda nyumbani kutoka kanisani, lakini Brad hakuliona koti lake juu ya chanja.

“Una uhakika hapo ndipo ulipolitundika?” Mama aliuliza.

“Ndiyo. Lilikuwa hapo hapo.” Koti la Brad lilikuwa rangi iliyong’aa ya samawati na nyekundu. Ilikuwa ni vigumu kulikosa.

“Labda lilihamishwa. Acha tuangalie kuzunguka jengo,” Baba alisema.

Mama, Baba, na Brad walitawanyika kuangalia kwenye vyumba tofauti. Walitafuta kwenye kisanduku cha vitu vilivyopotea na kupatikana, ndani ya chumba cha ibada, ndani ya chumba cha Brad cha Shule ya Jumapili, ndani ya chumba cha msingi, na juu ya kila chanja ya koti. Walitafuta hadi maliwatoni, lakini hawakulipata koti.

“Labda mtu amelichukua kwa bahati mbaya. Nina uhakika watalirudisha wiki ijayo mara tu watakapogundua siyo la kwao,” Baba alisema.

“Kwa sasa, unaweza kuvaa koti lako la zamani,” Mama alisema.

Brad alichukia. Hakupenda koti lake la zamani. Lilikuwa jembamba, limepauka, na dogo





sana kwake. Alipenda jinsi koti lake jipya la samawati na nyekundu lilivyomfanya aonekane kama shujaa mkubwa.

“Pengine mtu aliona koti langu lilivyo zuri na kuliiba,” Brad aliwaza. Hilo lingewezaje kutokea kanisani? Kila mmoja pale alipaswa kuwa mwaminifu. Brad asingeweza kumwacha mwizi yule apotee nalo. Alikuwa na mpango. Jumapili ijayo, angetazama kwa makini kuona nani alikuwa amevaa koti lake. Kisha angelikwapua kwa nyuma na kupiga kelele, “Simama, mwizi!” Wangejuta kwa nini walilichukua.

Brad alipata shida kuisubiri Jumapili ili kutimiza mpango wake. Lakini Jumapili iliyofuata ilikuwa na joto sana kwa watu kuvaa makoti, kadhalika na Jumapili iliyofuatia.

Jumapili baada ya hiyo, Brad aliwaangalia kwa mashaka wavulana katika darasa la msingi, akijiuliza nani aliiba koti lake. Je, ni yule mvulana mrefu? Au pengine alikuwa ni msichana. Alihisi kama hakuweza kumwamini yeyote. Brad hakupenda hisia ile.

Baada ya ibada Brad aliharakisha kuzunguka jengo, akitazama familia zikivaa makoti yao. Lakini hakuona

koti lake popote. Aliangalia hata kwenye sanduku la vitu vilivyopotea na kupatikana . . . lakini hakukuwa na koti. Litakuwa wapi?

Njiani kurudi nyumbani, Brad alifikiria mpango mpya. Angesali. Alijua Baba wa Mbinguni angeweza kupata vitu vilivyopotea. Usiku ule Brad aliomba na kusema, “Baba wa Mbinguni, tafadhali niambie nani alichukua koti langu. Nalitaka.”

Brad alisubiria jina au sura ya mwizi kuja akilini. Lakini badala yake alianza kumfikiria rafiki yake Carl. Brad mara nyingi alikaa karibu na Carl katika darasa la Msingi. Walitaniana na kucheka pamoja mara nyingi. Lakini Carl hakuwepo kanisani kwa wiki kadhaa. Brad alimkosa.

Vipi kama *Carl* alikuwa amechukua koti lake? Pengine Carl aligopa kuja kanisani sasa kwa sababu alidhani Brad asingekuwa rafiki yake tena. Brad alitaka Carl aje kanisani tena. Ikiwa Carl alikuwa amechukua koti lake, Brad aliamua, asingempigia kelele. Angemsamehe.

Brad alipanda kitandani, akijiskia vizuri.

Jumapili iliyofuata katika darasa la Msingi, Carl hakuwepo, lakini mvulana mgeni alikuwepo. Alikuwa amevalia tai yenye mistari myekundu na samawati.

“Tai nzuri,” Brad alisema, akiketi karibu na mvulana mgeni. “Inakufanya uonekane kama shujaa mkubwa.”

Mvulana alitabasamu.

Brad alitabasamu pia. Hakuwa akiwatafuta wezi tena. Alikuwa akitafuta marafiki. ●

*Mwandishi anaishi Iowa, Marekani.*

# Hujambo kutoka Estonia!



Sisi ni Margo na Paolo. Mwaka huu tunasafiri kuzunguka ulimwengu kujifunza kuhusu watoto wa Mungu. Jiunge nasi tunapozuru Estonia!



Hii ni Tallinn, mji mkuu wa Estonia. Umekuwepo kwa miaka 800! Estonia ina nyika nyingi, kama miti na sehemu teketeke. Kwa kweli, zaidi ya nusu ya Estonia imefunikwa na msitu. Watu wengi wa Estonia hupenda kutumia muda kwenye vitu vya asili.


Hivi ndivyo unavyosema "hujambo" kwa Kiestonia:

Teres!

Na hivi ndivyo unavyosema jina la Kanisa:

Viimse Aja Pühade Jeesuse Kristuse Kirik

Estonia iko Ulaya ya kaskazini. Ina visiwa zaidi ya 2,000. Takriban watu milioni 1.3 wanaishi Estonia.





Je, nini ni kwa ajili ya chakula cha usiku Estonia? Labda nguruwe au samaki wa achali na viazi, kabeji, malai chachu, na mkate mwe-usi. Hiyo huitwa sandwichi ya sprati.



Kanisa katika Estonia ni dogo lakini imara. Kuna takriban waumini elfu moja wa Kanisa. Hekalu lao la karibu liko Helsinki, Finland.



Je, unapenda kuimba katika darasa la Msingi? Kila baada ya miaka mitano, Waestonia hukusanyika kwenye sherehe kubwa kusherehekea nchi yao kwa kuimba na kucheza.

**Je, unatokea Estonia? tuandikie!  
Tungependa kusikia kutoka kwako.**

Asante kwa kutalii Estonia pamoja nasi. Tutaonana wakati mwingine!



### **Kutana na wamisionari wawili kutoka Estonia!**



Usiku mmoja nilipotaka kwenda kulala, mwanasesere wangu haukuonekana. Niliutafuta lakini sikumpata. Niliomba. Kisha nilimpata mwanasesere wangu na kuwa na ndoto nzuri.

**Bianka J., miaka 7**



Familia yetu inapenda kuwa-tumikia wengine. Kutumikia hutusaidia kuhisi Roho Mtakatifu, ambaye hutupatia hisia nzuri ya amani. Mimi na dada yangu hutengeneza zawadi kwa ajili ya wengine kwa sababu tunataka wao wahisi kupendwa.

**Piibe J., miaka 10**

# Kujihisi MPYA



## Na Jessica Larsen

Imetokana na hadithi ya kweli

### Estonia

**N**ina jambo la kustaajabisha!” *Emma* (Mama) alisema wakati alipomchukua *Rasmus* kutoka shule. Wali-tembea pamoja kwenye mitaa yenye majengo yenye rangi nzuri yaliyo kwenye mstari.

“*Rosolje* kwa ajili ya chakula cha usiku?” *Rasmus* alibashiri kwa matumaini. Walikuwa wameila wiki iliyo-pita kwenye mwaka wake wa saba wa kuzaliwa. Lakini mara zote angeweza kula kachumbari nyingi ya kiazzi sukari na mbatata pamoja na samaki wa maji chumvi aliyetengenezwa kwa achali!

*Emma* alitikisa kichwa kwa tabasamu. “Nilikutana na wasichana wawili kwenye basi asubuhi ya leo. Wami-sionari. Wanakuja kutembelea usiku huu kuzungumza kuhusu Kanisa lao.

*Rasmus* alitazama juu kwa udadisi. Hakuwahi kukutana na wamisionari kabla.

Alikuwa chumbani kwake akicheza na kigari chake

wakati wamisionari walipokuja. “*Tere! Tere!* Habari!” walimsalimia *Emma* pale walipoelekea ndani. Walivua buti zao nzito na kuvaa malapa ya ndani ambayo *Emma* alitunza kwa ajili ya wageni. *Emma* aliwaongoza kwenye kochi la rangi ya machungwa. Lakini *Rasmus* alibaki nyuma mlangoni.

Mwanamke mrefu alimuona na kutabasamu. Beji yake nyeusi ilisema *Öde Craig* (Dada Craig). “Mama yako alitumbia ulikuwa na siku ya kuzaliwa,” alisema. “Tumekuletea kitu.” Alitoa kadi ndogo. *Rasmus* aliingalia kwa karibu.

Ilikuwa picha ya mwanaume. Alikuwa amevaa joho jeupe, na mikono yake imenyooshwa.

“Unajua huyo ni nani?” *Öde Craig* aliuliza.

*Rasmus* hakujuua jina la mwanaume yule. Hakuwahi kuona picha hii awali. Lakini mwanaume yule alionekana mkarimu na mwenye nguvu. “Nadhani ni mfal-me!” *Rasmus* alisema.

Wamisionari wote wawili walitabasamu. “Ndiyo, Yeye ni mfalme! Yeye ni Mfalme wa Wafalme! Jina lake ni Yesu Kristo.” Öde Craig alitoa kitabu chenye jalada la samawati. “Na hiki ni kitabu kinachofundisha kuhusu Yeye, *Mormoni Raamat*. Kitabu cha Mormoni.”

Yeye na *Em*a walianza kusoma Kitabu cha Mormoni kila siku kabla hajaenda shule. Wakati wa shule, Rasmus na darasa lake walifanya matembezi ya kufurahia asili na kulala usingizi kidogo. Baada ya shule, yeye na *Em*a mara nyingi walikutana na wamisionari. Walizungumza na wamisionari kuhusu kile walichosoma kwenye Kitabu cha Mormoni. Wakati mwingine *Em*a alitupatia kila mtu chakula *kringel*, mkate wa kusokota wa mdalasini. Mwisho wa wiki yeye na *Em*a waliendesha baiskeli au kuwa na mandari ufukoni. Wakati mwingine walifanya matembezi marefu msituni au pembeni mwa mto walioupenda sana.

Kwenye moja ya matembezi hayo ya msituni, *Em*a alimwambia kwamba alitaka kubatizwa. Rasmus alitabasamu. Wamisionari walikuwa wamuomba *Em*a kuomba kuhusu ikiwa abatizwe au la. Ilionekana kama vile alikuwa amepata jibu lake!

“Na ninajua wapi nitabatizwa,” alisema kwa tabasamu. “Unaweza kubahatisha?”

Rasmus aliwaza kuhusu somo la wamisionari kuhusu ubatizo. Walikuwa wameonyesha picha ikimwonyesha Yesu Kristo pamoja na Yohana Mbatizaji ndani ya mto. . . .

“Mto!” alitamka ghafla kwa mshangao. “Mto wetu tunaoupenda sana.”



Wiki moja baadaye, Rasmus alisimama kwenye ukingo wa mto pamoja na wamisionari na baadhi ya watu wengine kutoka kanisani. *Em*a alikuwa tayari kubatizwa. Alikwenda chini kabisa ya maji, kama vile Yesu alivyofanya. Alipotoka juu, alikuwa akita-basamu. Rasmus alitaka kukumbuka wakati huu siku zote—maji yenye rangi ya samawati, maua meupe ya kondeni ndani ya nyasi za kijani, na tabasamu la mama yake.

“Kubatizwa kuna hisia gani?” aliuliza baadae, wakati kila mmoja alipokuwa akila biskuti wamisionari walizoleta.

“Ya kupendeza,” alimwambia. “Nilitaka kubaki ndani ya maji siku zote. Najihisi Mpya kabisa!” Alimkumbatia kwa nguvu.

“Kwa ajili ya siku yangu ya kuzaliwa itakayofuata, ninitaka kubatizwa, kama vile wewe na Yesu,” alimwambia.

“Nataka kuwa mpya pia!” ●

*Mwandishi anaishi Texas, Marekani.*





**Na Reyna I. Aburto**

Mshauri wa Pili katika Urais  
Mkuu wa Muungano wa  
Usaidizi wa Akina Mama

# Nitamwona Yeye Tena



**N**ilikulia huko Nicaragua. Nilipokuwa mdogo, nilifanya kila kitu pamoja na kaka yangu mkubwa. Tulienda shuleni pamoja. Tulienda dukanani pamoja. Tulikuwa na maisha yenye vituko vyote kwenye ua wetu wa nyuma. Tulikuwa wenye furaha.

Kisha, nilipokuwa na miaka tisa, jambo la kuhuzunisha lilitokea. Kaka yangu alifariki kwenye tetemeko la ardhi. Mwanzoni haikuonekana halisi kwamba hakuwepo. Niliwahi kudhani kwamba angebisha kwenye mlango wetu wa mbele. Ange-tuambia kwamba alikuwa mbali mahala fulani. Niliwahi kuduwaa mlangoni, nikitamani hilo litokee. Nilitaka sana kumuona tena.

Baada ya muda, ilikuwa kidogo angalau. Bado nili-endelea kumkosa kaka yangu, lakini niliweza kuhisi furaha tena.

Wakati huo, sikuwa muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Lakini nilipokuwa mkubwa, nilijifunza kuhusu Kanisa na kubatizwa. Siku moja nilikuwa nikiosha vyombo vyangu. Ilikuwa ni wakati wa Pasaka. Nilikuwa nikifikiria juu ya Ufufuo na kumfikiria kaka yangu.

Ghafla hisia iliniijia. Nilikumbuka ndoto ya mchana niliyokuwa nayo kuhusu kaka yangu. Niligundua



kwamba haikuwa ya kipuuzi hata kidogo! Iliku-ja kutoka kwa Roho Mtakatifu, kunifariji na kunio-ngoza. Siku moja kaka yangu kweli atafufuka. Na nitamwona tena.

Ikiwa mtu unayempenda amefariki, ni SAWA kuwa-kosa na kuhisi huzuni. Zungumza na familia yako au mtu mzima unapohisi uko tayari kufanya hiyo. Omba kwa Baba wa Mbinguni kuhusu jinsi unavyohisi. Anaweza kukusaidia kuhisi amani tena.

Katika hali yoyote, kumbuka kwamba Yesu Kristo anakupenda. Wakati wa Pasaka tunakumbuka dhabihu Yake kwa ajili yetu. Kwa sababu Yake, sisi sote tutafufuka na tunaweza kuishi na familia zetu milele. ●



## Kadi za Faraja

Kata na uondoe kadi hizi. Ungeweza kuzikunja katikati au kuzitumia kwa kuweka alama kitabuni. Zitunze katika maandiko yako au mahali pengine ili uweze kuzitazama wakati unapohisi huzuni, upweke, au woga.



“Sitawaacha ninyi  
yatima: Naja kwenu.”

Yohana 14:18



“Naye atafuta kila chozi  
katika macho yao.”

Ufunuo 21:4



“Changamkeni, na  
msiogope, kwani Mimi  
Bwana nipo pamoja  
nanyi, na nitasimama  
karibu yenu.”

Mafundisho na Maagano 68:6



# Onyeshwa na Eleza

Napenda kutazama hekalu

**Rebecca C., miaka 9, Aragua, Venezuela**



Siku moja tulingia katika gari, halingeweza kuwaka. Tukaangalia injini, lakini bure. Nilihisi kwamba ninapaswa kusali. Kwa hiyo nilisali. Dakika chache baadaye gari liliwaka. Ninashukuru kwamba Baba wa Mbinguni daima anaweza kunisaidia.

**Brooklyn B., miaka 9, Quetzaltenango, Guatemala**



Miaka miwili iliyopita mvulana mgeni alijiunga na darasa letu shuleni. Alikuwa si mkarimu kwa wengine. Kila mmoja alianza kumchukia na kutokuwa mkarimu kwake. Ilionekana kumfanya awe na huzuni, hivyo sikufanya kile wengine walichofanya. Rafiki zangu kadhaa waligundua na kufuata mfano wangu. Naamini kwamba nilifanya kile Mungu anataka nifanye, nitakuwa mwenye furaha na salama. Naamini kwamba nikiwa na ujasiri na kuzungumza mawazo yangu, nitapata marafiki ambao watanipenda jinsi nilivyo.





**Vestina K., age 11, Vilnius, Lithuania**



Ninapenda kucheza mpira na watoto wadogo na kuwafundisha mbinu mpya. Ni njia mojawapo ninayopenda kutumikia.

**Sasha K., age 11, Moscow, Urusi**

Tumia picha hizi  
kujaza chati kwenye  
kurasa R12–R13.



# Wapendwa Wazazi,

**Mwezi huu,** *Rafiki* ina hadithi na shughuli kuisaidia familia yako kusherehekea Pasaka. Tunatumaini familia yako itafurahia kufikiria kuhusu Pasaka kipindi chote cha mwezi!

- “Zawadi Kuu ya Mungu” (R2)—Ujumbe wa Pasaka kutoka kwa Rais Russell M. Nelson
- “Yesu Ni Mwokozi Wangu” (R3)—Shughuli ya kupaka rangi kuhusu Upatanisho na Ufufuo wa Yesu.
- “Hadithi ya Pasaka” (R4–R6)—Kielelezo cha hadithi ya maandiko
- “Nitakaporudi Kwake” (R7)—Wimbo mpya wa kupendeza kuhusu toba
- “Kujihisi Mpya” (R18)—Hadithi kuhusu mvulana kutoka Estonia ambaye anajifunza kuhusu Yesu
- “Nitamuona Yeye Tena” (R20)—Ushuhuda wa Ufufuo wa dada Reyna I. Aburto

Tafadhi andika kutujulisha jinsi familia yako ilivyotumia hadithi na shughuli hizi.

Kuwa na Pasaka yenye baraka!

*Rafiki*

## **New Friend**

**50 E. North Temple Street,  
Room 2393  
Salt Lake City, UT 84105 USA  
liahona@ldschurch.org**



**Tafuta Liahona iliyofichwa ndani!**

## **YALIYOMO**

- R2** Kutoka kwa Urais wa Kwanza: Zawadi Kuu ya Mungu
- R4** Hadithi za Maandiko: Hadithi ya Pasaka
- R7** Muziki: Nikirudi Kwake
- R8** Uaminifu wa Kupendeza
- R10** Mitume kote Ulimwenguni: Mzee Bednar Anazuru India
- R12** Manabii na Mitume Wetu
- R14** Kofi Lililopotea
- R16** Hujambo kutoka Estonia!
- R18** Kujihisi Mpya
- R20** Nitamwona Yeye Tena
- R22** Onyesha na Sema
- R23** Picha za Manabii na Mitume